# KUCHUNGUZA TAMATHALI ZA USEMI KATIKA MASHAIRI YA MAGAZETINI: UCHUNGUZI KIFANI WA MASHAIRI YA UKIMWI KATIKA MAGAZETI YA KISWAHILI

**OMARI MTUNGUJA KOMBO**

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SHARTI PEKEE LA KUTUNUKIWA DIGRII YA UZAMILI (M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2014**

## UTHIBITISHI

Mimi Profesa T.S.Y.M. Sengo ninathibitisha kuwa nimesoma tasinifu hii iitwayo ***Kuchunguza Tamathali za Usemi katika Mashairi ya Magazetini: Uchunguzi kifani wa Mashairi ya UKIMWI katika Magazeti ya Kiswahili*** na ninapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digrii ya M.A. Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Sheikh, Daktari, Professa T.S.Y. SENGO

**(Msimamizi)**

Tarehe

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

**TAMKO**

Mimi **Omari Mtunguja Kombo**, ninathibitisha kuwa tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

……………………………………………..

Sahihi

……………………………………………..

Tarehe

## TABARUKU

Ninapenda kuitabaruku kazi hii kwa wazazi kwa wazazi wangu, wake zangu na watoto wetu wapendwa.

## SHUKURANI

Kazi hii ya utafiti ni matokeo ya mchango na ushirikiano kati yangu na watu wengine wakiwemo walimu wangu. Kwa kuwa sio rahisi kuandika kwa kina mchango wa kila aliyenisaidia kukamilisha kazi hii, wafuatao wanastahili shukrani za kipekee. Kwanza napenda kumshukuru Mungu kwa kunijalia nguvu na uelewa kipindi chote cha masomo yangu hata kukamilika kwa kazi hii.

Pia napenda kutoa shukurani zangu za pekee kwa msimamizi wangu wa tasinifu hii, sheikh, daktari, professa, T.S.Y. Sengo kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya utafiti huu. Hakusita wala kuchoka kunishauri na kuirekebisha kazi hii katika hatua zote mpaka ilipokamilika. Usaidizi wake hauwezi kukisiwa wala kulipwa. Ninachoweza kusema ni asante sana professa, Mungu akubariki na kukujalia afya njema na maisha marefu.

Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa familia yangu nikianza na wake zangu Tatu Mwokeachao Omar na Mariamu Mwiduchi Omar. Ninawashukuru sana kwa uvumilivu wenu hasa katika kipindi ambacho nilikuwa mbali na nyumbani nikikazana katika kufanikisha utafiti huu.

Pia, ninapenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Bwana Nyuni Ndaro ambaye amekuwa bega kwa bega na mimi katika hatua zote muhimu za utafiti huu. Kila mara alinitia moyo kwamba nikazane na Mwenyezi Mungu ataniwezesha kumaliza masomo yangu. Mwisho ninapenda kumshukuru Mwalimu Mohamed Omary kwa kuisoma kazi hii mara kadhaa na kunipatia maoni yaliyonifungulia njia ya kukamilisha kazi hii.

## IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia matumizi ya lugha ya tamathali za usemi katika mashairi ya magazetini. Ili kukamilisha lengo hili kuu madhumuni mahususi matatu yalitimizwa. Madhumuni hayo yalihusu kubainisha tamathali za usemi, dhamira na dhima za tamathali za usemi katika kujenga dhamira mbalimbali katika mashairi ya magazetini. Mtafiti ametumia mbinu za uchambuzi wa kimaudhui, usaili na upitiaji wa nyaraka katika kukusanya data za utafiti. Mikabala ya kifasihi na ule wa kimaelezo ndio iliyotumika katika kuchambua data za utafiti wetu.

Kwa ujumla utafiti umeweza kukusanya data ambazo zimeweza kujibu maswali ya utafiti wetu ambapo imethihirika kwamba, mashairi ya magazetini yamesheheni matumizi ya tamathali mbalimbali za usemi. Pia imebainika kwamba tamathali hizo za usemi zinatumika kujenga dhamira mbalimbali na mwisho tamathali za usemi zimebainika kuwa na dhima mbalimbali za kifani na kimaudhui katika kujenga na kuwasilisha dhamira mbalimbali kuhusiana na masuala ya UKIMWI kwa jamii ya Kitanzania.

Mwishoni mwa utafiti kumetolewa mapendekezo kwa wadau mbalimbali wa mashairi ya magazetini kuhusiana na namna bora za kuimarisha mashairi hayo ili yaendelee kutekeleza wajibu wake kwa jamii. Pia, tumetoa mapendekezo kwa ajili ya tafiti za baadaye katika uwanja wa mashairi ya magazetini.

## YALIYOMO

Uthibitishi ..... ii

Hakimiliki. ..... iii

Tamko………. ..... iv

Tabaruku …….. ..... v

Shukurani.. ..... vi

Ikisiri….. ..... vii

Yaliyomo..... viii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ..... 1**

1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti ..... 1

1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti ..... 5

1.3 Malengo ya Utafiti ..... 6

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti ..... 6

1.3.2 Malengo Mahususi ..... 6

1.3.3 Maswali ya Utafiti ..... 7

1.4 Umuhimu wa Utafiti ..... 7

1.5 Mipaka ya Utafiti ..... 9

1.6 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi wake ..... 9

1.7 Mpango wa Tasinifu ..... 10

**SURA YA PILI: UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA ..... 12**

2.1 Utangulizi ..... 12

2.2 Ufafanuzi wa Dhana Mbalimbali ..... 12

2.2.1 Dhana ya Ushairi ........ 12
2.2.2 Ushairi wa Kiswahili ........ 13
2.2.3 Dhana ya Shairi ........ 14
2.2.4 Tamathali za Usemi ........ 15
2.2.4.1 Sitiari ........ 15
2.2.4.2 Ishara ........ 15
2.2.4.3 Taswira ........ 16
2.3 Utalii wa Kazi Tangulizi ........ 16
2.3.1 Ushairi kwa Ujumla ........ 16
2.3.1.1 Dhamira katika Mashairi ........ 16
2.3.1.2 Fani katika Mashairi ........ 23
2.4 Mashairi ya Magazetini ........ 26
2.5 Hitimishi ........ 29
2.6 Mkabala wa Kinadharia ........ 30
2.6.1 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ........ 30
2.6.2 Nadharia ya Ufeministi ........ 32
2.6.3 Nadharia ya Simiotiki ........ 37
2.7 Hitimishi ........ 38

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........ 39**

3.1 Utangulizi ........ 39
3.2 Eneo la Utafiti ........ 39
3.3 Umbo la Utafiti ........ 39
3.4 Watafitiwa ........ 40

3.4.1 Uteuzi wa Watafitiwa ........ 41
3.5 Vyanzo vya Data ........ 42
3.5.1 Data za Msingi ........ 42
3.5.2 Data za Upili ........ 42
3.6 Mbinu ya Ukusanyaji wa Data ........ 42
3.6.1 Uchambuzi wa Kimaudhui ........ 43
3.6.2 Usaili ........ 43
3.7 Uchambuzi wa Data ........ 44
3.8 Usahihi wa Mbinu za Utafiti ........ 45
3.8.1 Kuaminika kwa Matokeo ya Utafiti ........ 45
3.9 Maadili ya Utafiti ........ 46
3.10 Hitimishi ........ 46

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI ........ 48**

4.1 Utangulizi ........ 48
4.2 Tamathali za Usemi katika Mashairi ya Magazetini ........ 48
4.2.1 Taswira ........ 48
4.2.2 Sitiari ........ 55
4.2.3 Takriri ........ 61
4.2.4 Tafsida ........ 67
4.2.5 Tashibiha ........ 70
4.2.6 Ishara ........ 75
4.3 Dhamira katika Mashairi ya Magazetini ........ 79

5.3.1 UKIMWI na Umalaya ........ 79

5.3.2 Chanzo Cha UKIMWI ........ 82

4.3.3 Unyanyapaa ........ 83

4.3.4 Kinga ya UKIMWI ........ 86

4.3.5 Hitimishi ........ 88

4.4 Dhima ya Tamathali za Usemi katika Kujenga Dhamira ........ 88

4.4.1 Dhima za Kimaudhui ........ 88

4.4.1.1 Kumfikirisha Msomaji ........ 89

4.4.1.2 Kuhamasisha Jamii ........ 91

4.4.1.3 Kufafanua Jambo ........ 93

4.5 Dhima za Tamathali za Usemi Kifani ........ 97

4.5.1 Kupamba Lugha ........ 97

4.5 2 Tamathali za Usemi na Vipengele Vingine vya Kifani ........ 98

4.5.3 Hitimishi ........ 99

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHI NA MAPENDEKEZO ........ 101**

5.1 Utangulizi ........ 101

5.2 Muhtasari wa Tasinifu ........ 101

5.3 Hitimishi ........ 103

5.4 Mapendekezo ........ 106

5.4.1 Mapendekezo kwa Watunzi wa Mashairi ........ 106

5.4.2 Mapendekezo kwa Wachapaji ........ 107

5.4.3 Mapendekezo kwa Tafiti za Baadaye ........ 107

**MAREJELEO………. ........ 108**

**VIAMBATANISHO ........ 116**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Ushairi wa Kiswahili ni miongoni mwa tanzu za fasihi ambazo zina historia ndefu katika kuwako kwake Uswahilini. Kimani (1983) anaeleza kwamba, Utenzi wa *Tambuka* au kwa jina lake la pili, *Chuo cha Herekali* ni utenzi maarufu sana katika historia ya ushairi wa Kiswahili. Utenzi huu ni wa kwanza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili, ingawa inaaminika kwamba kabla ya utenzi huu kuandikwa na Mwego bin Athumani katika 1728, kulikuwa kuna mashairi mengi mengine ya Kiswahili. Katika kufanya hivi, bwana Mwego, aliyeishi Pate Kisiwani, akawa ametufungulia historia ya ushairi wa Kiswahili. Utenzi huu unasimulia habari za Fumo Laiti Nabahani, Sultani wa Pate wa wakati huo. Pia utenzi huu unahusisha vita vya miezi minane iliyotokea Syria kati ya Waarabu na wenyeji wa Byazantine kwa ajili ya dini ya Kiislamu.

Kama inanavyosadikiwa, mashairi yalikuwa mengi sana kabla ya utenzi huu kuandikwa. Kasoro ni kwamba washairi wa siku hizo hawakuyahifadhi mashairi yao katika maandishi. Ilikuwa bado ni jadi ya Waswahili kuhifadhi tungo zao vichwani kutokana na uwezo wao wa kuhifadhi Quraani.  Waislamu walipofika, waliwakuta wenyeji wakiwa na utamaduni wao, wakawafunza kuandika kwa hati za Kiarabu ambazo wenyeji waliziongezea herufi na kuzifanya hati za Kiswahili. Wenyeji wakaanza kuandika na kuhifadhi utamaduni wao kwa njia hii, ndipo akazuka Mwego bin Athumani na kuandika utenzi wake.

Maelezo haya juu ya historia ya ushairi wa Kiswahili, yanaonesha kwamba ushairi wa Kiswahili wa hapo kale haukuandikwa na kuhifadhiwa katika maandishi kwa

kuwa utaalamu wa kusoma na kuandika haukuwepo katika jamii ya wakati huo. Kwa hivyo, ushairi uliokuwapo ni ushairi simulizi, hasa nyimbo. Hata hivyo, ushairi simulizi ndiyo uliozusha ushairi andishi wa Kiswahili mara baada ya utaalamu wa kuandika na kusoma ulipoletwa na Waislamu wa tapo la Mtume Muhammad (SAW). Jambo hili laonesha kwamba, ushairi andishi wa Kiswahili una sifa nyingi za ushairi simulizi kwa sababu ndicho chanzo chake.

Kimsingi, Waarabu waliukuta Ushairi wa Kiswahili wakautumia kwa kuandika tenzi, mashairi, kasida na duwa kwa lugha ya Kiswahili baada ya wao kujifunza Kiswahili na hati za Kiswahili zilizofanana na za Kiarabu (Mansour, 2013; Omary, 2011). Hivyo ni kusema kwamba, mashairi ya Kiswahili ya zamani yalihifadhiwa vichwani na kutongolewa kwa midomo kila ilipohitajika. Dhima mojawapo kuu ya Ushairi wa Kiswahili ni kuimbika ili uelimishe na huku ukiburudisha. Hii ndiyo kanuni ya kwanza na iliyo muhimu sana katika Ushairi wa Kiswahili (Kimani, 1983; Massamba, 1983).

Maelezo hayo yanatuonesha kwamba Ushairi wa Kiswahili ulianza na nyimbo za Waswahili ambazo wamekuwa wakiziimba karne na karne. Kauli kwamba asili ya ushairi wa Kiswahili ni fasihi ya Kiarabu na Dini ya Kiislamu zinatokana na chuki za Kikoloni, za Kidini na kibinafsi. Chuki si tabia ya Wasomi. Ushairi wa Kiswahili una kwao (Sengo, 2009). Hii inadhibitishwa na utafiti uliofanywa na Mulokozi na Sengo (1995) ambao nao walihitimisha kwamba, Ushairi wa Kiswahili unatokana na nyimbo za Kiafrika ingawa na wao wanakiri kuwa fasihi ya Kiarabu na Dini ya Kiislamu zimetoa mchango mkubwa katika kuathiriana na fasihi ya Kiswahili. Waislamu wageni walipokuja Pwani ya Afrika ya Mashariki, walifundisha Dini ya

Kiislamu na ustaarabu wake ambao ulifuatwa na Waswahili wengi na kuwa sehemu muhimu ya utamaduni wao. Kwa hali hiyo, ikawa ni jambo la kawaida kwa ushairi na aina nyingine ya fasihi ya Waswahili iliyokuwapo wakati huo kusawiri utamaduni wa Uswahilini. Waswahili walikuwa na ushairi wao ambao uliimbwa katika hadhara kulingana na matukio maalumu. Kimani (1983:131) anasema:

> *Tungo za zamani na za siku hizi zinatungwa kufuatana na matukio au majira: mvua au ukame, njaa au shibe, au nyakati Kama vile za vita, amani, mabadiliko ya siasa (na kwa hivyo kufunza siasa mpya ya nchi) na hata kuwashutumu au kuwasifu viongozi. Tungo nyingine zinatungwa kwa nia ya kuwavunja moyo maadui walio tayari kushambulia. Mfano mzuri wa tungo za aina hiyo ni zile zilizotungwa na Muyaka bin Haji-Al Ghassani*.

Kwa mantiki hii ushairi wa Kiswahili unaonekana kuanza tangu pale mwanadamu alipoanza kuwasiliana kwa kutumia lugha. Hii inaonekana katika nukuu hapo juu ambapo tunaelezwa kwamba ushairi wa Kiswahili uliimbwa kwa lengo la kueleza juu ya masuala mbalimbali ambayo yanaonekana kutokea mara kwa mara katika jamii za zamani na jamii za siku hizi.

Ushairi wa Kiswahili uliendelea kutekeleza dhima zake katika vipindi tafautitafauti vya maisha ya jamii ya Waswahili. Kwa mfano, Mulokozi (1982) anaeleza kwamba, Ushairi wa Kiswahili ulitumika kama silaha muhimu ya kupinga utawala wa Kikoloni kwa kuelezea madhila yanayofanywa na Wakoloni dhidi ya wananchi. Kwa kufanya hivyo, washairi waliwataka wakoloni kuondoka nchini na kuwaachia wananchi nchi huru ili wajitawale wenyewe. Mfano mzuri ni ule wa kipindi cha utawala wa Wareno ambapo utawala huo ulipewa onyo kali na washairi la kutakiwa kuondoka nchini. Shairi la *Mzungu Migeli* ndilo linalothibitisha hoja hii kwamba:

*Mzungu Migeli*
*Mzungu Migeli Umuongo*
*Mato yako yana tongo*
*Kwani kuata mpango*
*Kwenda Kibanga uani*
(Kitogo, 2002).

Hiki ni kipande cha ubeti wa shairi ambalo halijulikani lilitungwa na nani lakini liliimbwa na wananchi katika kipindi cha utawala wa Wareno kwa nia ya kuwakumbusha kuwa wanatakiwa kuondoka nchini na kuwaachia wananchi nchi yao waiongoze wao wenyewe. Kipande hiki cha shairi ni sehemu ya ushairi simulizi ambacho hakikuwahi kuandikwa katika kipindi hicho, ndiyo maana mtunzi wake hakupata kutambulikana. Mashairi ya wakati wote huo yalitungwa kwa namna ambayo itaweza kuimbika kwa sababu hakukuwa na maandishi na hivyo kuliimba shairi ni kulihifadhi. Shairi linapoimbwa mara kwa mara hukaa kichwani kwa mwimbaji au waimbaji na hivyo kuzoeleka katika jamii. Kwa hivyo, ili shairi liweze kukaa kichwani kwa msomaji kwa harakaharaka ni lazima liwe na mapigo ya vina na urari wa mizani (Omari, 2009; Omary, 2011).

Mashairi ya Kiswahili yaliendelea kufanya kazi ya kuelimisha na kuburudisha jamii katika vipindi mbalimbali ambapo mashairi mengi yaliandikwa katika magazeti kama vile *Baragumu*, *Mambo Leo*, *Uhuru*, *Mzalendo* na kadhalika. Mutembei (2009) anaeleza kwamba, mashairi yanayoandikwa magazetini yana nafasi kubwa katika kuelimisha jamii juu ya mambo yanayotokea katika jamii yao na namna ya kukabiliana nayo. Kwa mfano, anaeleza kwamba ugonjwa hatari wa UKIMWI ulipoingia nchini na kusababisha vifo vya wananchi wengi, washairi walitumia kalamu zao kutungia mashairi katika magazeti kwa nia ya kuihamasisha jamii

kuufahamu ugonjwa huo ili wachukue hatua stahiki za kukabiliana nao. Vilevile, anaendelea kueleza kwamba, mashairi yanayoandikwa katika magazeti yana nguvu kubwa ya kuleta mabadiliko katika jamii.

Mashairi ya magazetini yana mchango mkubwa katika kujenga na kuimarisha utamaduni wa jamii. Hata hivyo, hakuna utafiti wa kina ambao tayari umekwishafanyika kwa nia ya kuonesha ushairi huo unatumia lugha ya aina gani na lugha hiyo, ina dhima gani katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa. Utafiti wetu umefanywa ili kuchambua matumizi ya lugha hasa ile ya kitamathali katika mashairi ya magazetini na kisha kuchunguza dhima ya tamathali hizo kwa jamii inayohusikahusika, hivyo, kuziba pengo la utafiti

## 1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti

Mashairi ya magazetini kwa taarifa tulizozipata yalianza kuandikwa tangu pale magazeti hayo yalipoanza kutolewa katika kipindi cha ukoloni wa Waingereza na kuendelea (Khalifan, 2013). Hata hivyo, katika kipindi hicho, magazeti mengi hayakutoa fursa kwa watunzi wa mashairi ya Kiswahili kuchapishiwa mashairi yao yaliyoikosoa serikali ya kikoloni na badala yake washairi walitakiwa kuandika mashairi ambayo yaliisifu serikali ya kikoloni (Kitogo, 2002). Kasi ya kutunga na kuchapisha mashairi katika magazeti iliongezeka mara tu ulipopatikana uhuru wa Tanganyika mnamo mwaka 1961, ambapo, washairi kama Saadan Kandoro, Mzee Waziri Kijana, Komba, Sudi Andanenga na wengine wengi waliandika mashairi yaliyojaa dhamira mbalimbali. Miongoni mwa dhamira zilizotia fora katika mashairi hayo ni zile zilizohusu ujenzi wa jamii mpya pamoja na siasa za ujamaa na kujitegemea (Khatibu, 1987).

Ingawa, mpaka kufikia sasa, mashairi ya magazetini yanaendelea kuchapishwa, ni utafiti mchache mno ambao umekwishafanyika kwa nia ya kuyachunguza mashairi hayo. Miongoni mwa uchachefu huo ni kazi ya Mutembei (2009), ya Chaligha (2011) na ya Khatibu (1987). Hata hivyo, watafiti hawa hawakuwa na lengo la kuchunguza matumizi ya lugha ya kitamathali katika mashairi ya magazetini, jambo ambalo linaonesha kuwapo kwa pengo la kiutafiti linalohitaji kushughulikiwa. Katika kushughulikia pengo hili la kiutafiti, utafiti huu umefanywa kwa kuchunguza matumizi ya lugha ya kitamathali katika mashairi ya magazetini kupitia magazeti yaliyoteuliwa.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu moja, na madhumuni mahususi matatu ambayo kukamilika kwake ndio kukamilika kwa utafiti wetu.

### 1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu, ni kuchunguza matumizi ya lugha ya kitamathali katika mashairi ya magazetini ya *Mzalendo*, *Nipashe*, *Majira*, *Uhuru* na *Mtanzania* yanayozungumzia ugonjwa wa UKIMWI.

### 1.3.2 Malengo Mahususi

Utafiti huu umekamilika baada ya kutimizwa kwa malengo mahususi yafuatayo:

(a) Kuainisha tamathali za usemi zinazojitokeza katika mashairi ya UKIMWI ya magazetini kupitia magazeti yaliyoteuliwa.

(b) Kubainisha dhamira mbalimbali zinazowasilishwa na lugha ya kitamathali katika mashairi ya UKIMWI ya magazetini kupitia magazeti yaliyoteuliwa.

(c) Kufafanua dhima ya lugha ya kitamathali ya mashairi ya magazetini katika kuibua dhamira za mashairi ya UKIMWI ya magazetini kupitia magazeti yaliyoteuliwa.

### 1.3.3 Maswali ya Utafiti

(a) Ni tamathali zipi za usemi zinazojitokeza katika mashairi ya UKIMWI ya magazetini kupitia mashairi yaliyoteuliwa?

(b) Matumizi ya lugha ya kitamathali katika mashairi ya UKIMWI ya magazetini yanawasilisha dhamira gani kwa jamii?

(c) Ni nini dhima ya lugha ya kitamathali ya mashairi ya UKIMWI ya magazetini katika kuibua dhamira za mashairi ya magazetini kupitia magazeti yaliyoteuliwa?

## 1.4 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kitaalimu na hivyo unatoa umuhimu katika maeneo ya taaluma; utafiti huu umeshakuwa rejeleo muhimu kwa wanafunzi na walimu wanaofundisha fasihi ya Kiswahili. Wanafunzi, kwa sasa wanaweza kutumia utafiti huu kwa ajili ya kukuzia maarifa yao ya nadharia ya Ushairi wa Kiswahili kwa kuelewa kwamba, Ushairi wa Kiswahili umeenea na kuandikwa na watu wengi waliojifunza na kuupenda; mfano hawa waliochapisha katika magazeti. Wanafunzi wa ngazi ya uzamili watatumia matokeo ya utafiti huu na kuwapatia maeneo mapya ya kufanyia utafiti katika taalimu ya fasihi ya Kiswahili.

Kwa upande wa walimu wa fasihi ya Kiswahili na fasihi kwa Kiswahili, watauona umuhimu wa utafiti huu, utakapowasaidia kuandaa maalumati ya kuwafundishia

wanafunzi wao. Pia, watautumia utafiti huu katika kuimarisha utafiti zaidi, ambao wataufanya katika tanzu za fasihi na vijitanzu vya ushairi wa Kiswahili kama nyimbo.

Kwa upande wa maadili, utafiti huu unaonesha kwamba, ushairi wa Kiswahili umepiga hatua kubwa ya maendeleo katika kufunza maadili. Hii inatokana na kutumika kwa tungo nyingi na baadhi kuimbwa na kusomwa katika magazeti na katika shughuli za kijamii kama vile; harusi, misiba, mahafali ya kuhitimu masomo, kupongeza watumishi baada ya kupandishwa vyeo na kadhalika.

Kwa upande wa utamaduni, utafiti huu una umuhimu mkubwa katika kuendeleza na kudumisha mema ya utamaduni wa Mtanzania, kwa kuwa katika ushairi wa magazetini huelezwa mambo ambayo yanatokana na utamaduni wa jamii ya Watanzania. Maadili na mafunzo mema yanayofundishwa katika mashairi ya magazetini, ni muhimu katika kuendeleza utu, heshima, adabu, ukarimu, umoja, amani na mshikamano miongoni mwa Watanzania.

Kwa upande wa sera za maendeleo, utafiti huu umesaidia kuibua masuala kadhaa ya kisera ambayo yanahitaji kuimarishwa kwa kutungiwa sera muafaka zitakazosaidia kuiletea jamii maendeleo. Miongoni mwa sera hizo ni kama ile ya Utamaduni na Lugha ambamo ndani mwake mnazungumzwa maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Kutokana na utafiti huu, watunga sera wameelekezewa maeneo mapya ya kuimarishwa ili kuikuza lugha ya Kiswahili, fasihi yake na utamaduni wa Mtanzania. Mzee Sengo, hivi sasa yumo mbioni kutafuta fedha zake mwenyewe, kuitisha kikao

cha Waswahili wenyewe, awakabidhi lugha yao wailee na watumiaji waendelee kuitumia vizuri bila ya kuiviza.

Kwa upande wa wasanii wanaotunga mashairi yao na kuyachapisha katika magazeti watauona utafiti huu kama changamoto ya wao kuendelea kutunga mashairi mengi zaidi na kuyachapisha katika magazeti. Wasanii wataona kuwa kumbe mashairi yao ni muhimu sana katika kufunza mambo mbalimbali kwa jamii ndio maana hata watafiti wanayashughulikia mashairi hayo.

## 1.5 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umeshughulikia matumizi ya lugha ya kitamathali katika mashairi ya magazetini tu. Hii inatokana na ukweli kwamba, matumizi ya lugha katika kazi za fasihi ni kipengele kipana mno ambacho hakiwezi kushughulikiwa katika utafiti wa ngazi wa shahada ya Uzamili na kukamilika kwa ukamilifu wake. Kwa kulifahamu hilo, ndipo kikachaguliwa kipengele cha tamathali za usemi peke yake katika ushairi wa magazetini. Magazeti yaliyohusishwa katika utafiti huu ni matano tu ambayo ni *Mzalendo*, *Nipashe*, *Majira*, *Uhuru* na *Mtanzania*.

## 1.6 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi wake

Mtafiti wa utafiti huu amekumbana na vikwazo, kikubwa kikiwa ni kukosa ushirikiano na wakuu wa kazi kuhusu muda. Mtafiti ni mtumishi wa serikali mwenye wajibati nyingi kwa mwajiri wake na hivyo kutakiwa kukamilisha kazi za mwajiri wake kwa wakati. Hali hii ilimfanya kutopata muda wa kutosha kushughulikia utafiti huu na kuumaliza kwa muda uliopangwa. Tatizo jingine ni lile linalohusiana na uhaba wa fedha za kufanyia utafiti. Mtafiti hakupata udhamini wa aina yoyote na hivyo kulazimika kutenga sehemu ya mshahara wake kwa ajili ya kujisomesha. Hili

ni tatizo kubwa kwa watumishi wa Umma, kukosa kupangiwa taratibu za kuongezewa viwango vya visomo kwa manufaa ya maendeleo ya taifa.

Ili kutatua vikwazo hivyo, mtafiti alifanya kila lililowezekana kuhakikisha kwamba, utafiti wake unakamilika kwa wakati. Hili liliwezekana baada ya yeye kutatua kikwazo cha muda kwa kutumia muda wake mwingi wa wakati wa usiku katika kuandika ripoti ya tasinifu yake. Badala ya kulala saa mbili usiku kama ilivyokuwa kawaida yake alilazimika kulala saa sita ya usiku ili kuweza kufidia muda alioukosa mchana kwa ajili ya kufanya kazi yake ya utafiti. Saa nne alizozimega kutoka katika usingizi zilimwezesha kupiga hatua kubwa katika uandishi wa tasinifu na kisha kufanikiwa kukamilisha utafiti huu. Kuhusiana na kikwazo cha fedha, mtafiti alijitahidi kutenga kiasi kikubwa katika mshahara wake kwa ajili ya kukamilisha utafiti wake na hivyo kusimamisha miradi mingine ya maendeleo aliyokuwa akiifanya kupitia sehemu ya mshahara wake. Alifanya hivyo kwa sababu alifahamu kwamba, elimu ndio ufunguo wa maisha kwa mwanadamu.

## 1.7 Mpango wa Tasinifu

Tasinifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya kwanza inazungumzia utangulizi wa jumla kuhusiana na utafiti wetu. Mambo ambayo yanazungumzwa katika sura hii ni usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, madhumuni mahususi na maswali ya utafti. Mambo mengine ni mipaka ya utafiti, vikwazo na utatuzi wa vikwazo. Sura ya pili inawasilisha utalii wa kazi tangulizi kulingana na mada ya utafiti wetu. Kazi tangulizi zilizopitiwa ni pamoja na zile zilizotafiti ushairi wa Kiswahili kwa ujumla na kisha tukaeleza kazi tangulizi zilizotafiti mashairi ya magazetini. Sura ya tatu inazungumzia mbinu za utafiti zilizotumika katika

kukusanya na kufanya uchambuzi wa data za utafiti na kuifanya tasinifu ionekane kama ilivyo. Sura ya nne inawasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti ili kujibu maswali ya utafiti wetu. Sura ya tano ndio inatoa muhtasari, hitimishi na mapendekezo kwa ajili ya utafiti zaidi.

# SURA YA PILI

# UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Hii ni sura ambayo inafanya kazi ya kutalii kazi tangulizi ambazo zimeshughulikia mambo yanayohusiana na mada yetu ya utafiti. Kazi tangulizi husomwa na kuhakikiwa na mtafiti kwa nia ya kubaini pengo la kiutafiti ambalo linahitaji kujazwa ili kuendeleza na kukuza taaluma husika (Babbie, 1999). Kimsingi, tumeanza sura hii kwa kutoa ufanunuzi wa dhana mbalimbali ambazo zimetumika katika utafiti huu. Katika sura hii pia, tumefanya utalii wa kazi zilizotafiti ushairi wa Kiswahili kwa ujumla wake na kisha tukatalii zile ambazo zimetafiti mashairi na kazi nyingine za kifasihi katika magazeti. Lengo kuu la kufanya hivyo ni kutaka kupata picha kamili kuhushu utafiti katika ushairi wa Kiswahili, umefanyika katika maeneo gani huku tukihusianisha na mada yetu ya utafiti.

## 2.2 Ufafanuzi wa Dhana Mbalimbali

Dhana mbalimbali zimefafanuliwa katika sura hii ili kumpa msomaji wetu uelewa makini juu ya dhana husika pale anaposoma kazi hii. Dhana hizo ni:

### 2.2.1 Dhana ya Ushairi

Ushairi ni utanzu ambao una historia ndefu katika fasihi ya Kiswahili. Ingawa mpaka leo hakuna makubaliano kuhusu utungo wa kwanza wa kishairi uliandikwa lini, wataalamu wanakubaliana kuwa utanzu huu una historia ndefu. Wapo wataalamu wanaosema kuwa utungo wa kwanza uliotungwa ni utendi wa *Mwanayanga* unaodaiwa ulitungwa na Fumo Liyongo katika mwaka wa 1517 (Wamitila, 2008). Nao Warren na Wellek (1985) wanasema kuwa ushairi ni utungo utumiao mfumo

maalumu wa maneno katika kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Ujumbe unaweza kuwa wa furaha, huzuni au masimulizi ya hadithi fulani.

Haries (1962) anauona ushairi kama taaluma iliyokamilika katika kueleza ukweli wa maisha katika jamii husika. Raffel (1984) anashadidia hoja hii kwa kueleza kwamba, kukamilika kwa ushairi hutegemea mbinu anazozitumia mshairi katika kutunga mashairi yake. Mbinu za utunzi wa mashairi hutofautiana baina ya mwandishi mmoja na mwingine.

Pamoja na maelezo kwamba, ushairi ni taaluma, ushairi ni utungo wa mwanzo kabisa kuliko tungo nyingine zote katika fasihi simulizi. Sanka (1994) anaongeza kwamba, ushairi umekuwa chombo muhimu katika kuhifadhi historia, falsafa na utamaduni wa jamii. Anaendelea kuongeza kuwa, ushairi ni zao la jamii husika na hivyo huwa na sifa maalumu kulingana na muktadha lengwa kwa jamii husika.

Maelezo haya kwa ufupi, yanatoa mwanga wa kusukuma mbele utafiti wetu, kwa msingi kwamba ushairi unaelezwa kama ndio utanzu wa mwanzo kabisa kupata kutungwa na mwanadamu katika historia yake. Katika kila fasili iliyotolewa hapo juu kuhusu ushairi ni nini kuna mambo ya msingi yafaayo kuzingatiwa na hivyo hakuna fasili ya kubezwa na nyingine kukuzwa. Kwa mantiki hiyo basi, maana ya ushairi iliyotumika katika utafiti huu inatokana na kuchota mawazo kutoka katika fasili zilizotolewa hapo juu.

### 2.2.2 Ushairi wa Kiswahili

Oslon (1975) anaeleza kwamba, ushairi wa Kiswahili ni chombo cha kuhamasisha matarajio na matamanio ya Waswahili na jamii kwa ujumla katika kujiletea

maendeleo. Anaongeza kwamba, ushairi wa Kiswahili umechukua nafasi kubwa kama chombo cha mawasiliano baina ya wanajamii. Kwa mfano, kama mshairi haridhiki na namna jambo fulani lilivyo au lifanywavyo, hutunga shairi kuelezea jambo hilo.

Mulokozi na Sengo (1995) wanasema kwamba, ushairi wa Kiswahili ni sehemu ya historia ya Afrika Mashariki kwa msingi kwamba, ulikuwepo tangu enzi za usimulizi na kutolea mfano, tungo za Lyiongo zilizoanza kama masimulizi ya shujaa wa kihistoria na ukatungwa utendi kutokana na masimulizi hayo.

Wamitila (2008) anaeleza kwamba, ushairi wa Kiswahili una makundi mawili. Mashairi ya jadi au mapokeo ambayo yanatungwa kwa kuzingatia arudhi au kaida za utunzi wa mashairi kwa kuzingatia vina, mizani, idadi maalumu ya mishororo katika ubeti, vipande na kadhalika. Pili, kuna mashairi huru ambayo yanakiuka kaida hizo na badala yake kutegemea mbinu nyingine za kishairi kama uruwazaji wa kimuundo katika kuuwasilisha ujumbe wake. Kimsingi, ushairi wa Kiswahili kwa sasa umepiga hatua kubwa ya maendeleo kifani na kimaudhui na kwamba, mashairi ya Kisasa na Kimapokeo yote yanakubalika na kutumiwa na wanajamii wote kama chombo cha kuburudisha na kuadilisha jamii. Utafiti huu ambao unashughulikia tamathali za usemi katika mashairi ya magazetini umechambua mashairi ya aina zote hizi mbili yaani mashairi ya Kisasa na mashairi ya Kimapokeo.

### 2.2.3 Dhana ya Shairi

Shairi ni utungo wa sanaa ya lugha wenye mpangilio maalumu wa mishororo au wa kisauti wenye kutumia mbinu za lugha zenye mnato na mbinu nyinginezo za

kibalagha na kimtindo zinazomwezesha mtunzi kuwasilisha ujumbe kwa ufupi na kwa mkokotezo mkubwa unaoeleza kisa, hisia, tukio au hali kwa lugha ya mvuto. Uzito hasa wa shairi upo kwenye uwezo wake wa kuzigusa hisia na mkuruba au uhusiano wake wa karibu na muziki (Wamitila, 2008).

### 2.2.4 Tamathali za Usemi

Tamathali za Usemi ni semi fupifupi zilizojengwa kimafumbo kwa lengo la kuwasilisha dhamira kwa hadhira iliyokusudiwa kwa namna ya kuifikirisha hadhira hiyo katika kupata maana ya tamathali husika (Njogu na Chimerah, 1999). Tamathali za usemi zipo nyingi mno ila kwa uchache tunataja zifuatazo: sitiari, ishara, taswira, picha, chuku, jazanda, tashibiha, tashihisi, tanakali sauti, tabaini, kejeli, vijembe, takriri na kadhalika. Katika utafiti huu tumeteua chache tu kama zinavyobainika katika sura ya nne ya tasinifu hii.

#### 2.2.4.1 Sitiari

Sitiari ni uhamishaji wa maana toka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine. Vikoa vya maana vinavyohusika katika uhamishwaji huu huwa vinatofautiana angalau kwa sifa moja ya msingi ya semantiki. Kinachohamishwa ni tabia au umbo au kazi ya kitu kwa kukihusisha na tabia au umbo au kazi ya kitu kingine (Kahigi, 1995).

#### 2.2.4.2 Ishara

Senkoro (1982:36) anasema kwamba: Ishara ni dhana au mawazo mbalimbali yanayotumiwa na washairi na wanafasihi katika kazi zao kuwakilisha vitu, dhana au mawazo mengine. Katika tasinifu hii tunaongelea juu ya ishara zinazopatikana katika

magazeti teule na kuonesha, kwa msaada wa nadharia ya Simiotiki na Mwitiko wa Msomaji zinawakilisha au zinaeleza nini katika muktahda wa kijamii.

#### 2.2.4.3 Taswira

Taswira ni picha wanayoipata wasomaji wa kazi ya fasihi wasomapo kazi husika, taswira hupatikana kutokana na ishara, sitiari, tashibiha na pengine uhalisiamazingaombwe (Senkoro, 1982). Kwa mfano, usomapo mashairi teule unakutana na matumizi mengi ya lugha ya Ishara na Taswira.

## 2.3 Utalii wa Kazi Tangulizi

Katika sehemu hii tumefanya utalii wa kazi ambazo tayari zimekwishafanyika mpaka hivi sasa kwa nia ya kuona watafiti watangulizi wanazungumza nini kuhusiana na ushairi wa Kiswahili. Hivyo, tumeona ni vema tuanze kueleza kazi tangulizi kuhusiana na ushairi wa Kiswahili kisha aina nyingine za mashairi na ndipo tukaishia katika kueleza juu ya kazi tangulizi katika mashairi ya magazetini.

### 2.3.1 Ushairi kwa Ujumla

#### 2.3.1.1 Dhamira katika Mashairi

Dhamira ni mawazo makuu ambayo mwandishi au mtunzi wa kazi ya fasihi anataka hadhira yake iyapate baada ya kuisoma au kusikiliza kazi yake hiyo (Njogu na Chimerah, 1999). Ushairi kama tulivyosema ni utanzu mkongwe kuliko tanzu nyingine za fasihi ya Kiswahili. Wapo wanataalimu ambao wamefanya utafiti na kueleza, namna ushairi unavyotumika kama chombo cha kuelezea masuala ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni katika jamii. Katika sehemu hii tunafaya

tathimini ya kazi za wanataalimu hao ili kuweza kuhusianisha na malengo ya utafiti wetu.

Omary (2011) alifanya utafiti katika tungo za Kezilahabi na kueleza kwamba, Kezilahabi ni bingwa wa kueleza masuala ya kisiasa katika mashairi yake yasiyofuata urari wa vina na mizani. Aliyasema haya pale alipokuwa akijibu hoja ya Frolova (2003), kwamba Kezilahabi hazungumzii siasa katika *Karibu Ndani* (1988). Anaendelea kueleza kwamba, matumizi ya lugha ya kisitiari, mafumbo na ishara ndiyo yaliyotawala katika tungo za kishairi za Kezilahabi na kupitia lugha hiyo ndimo masuala ya kisiasa huelezwa na kufafanuliwa. Mawazo haya ni muhimu na yanatoa mchango mkubwa katika kusukuma mbele utafiti huu. Ingawa utafiti wa Omary (2011) haukuwa na lengo la kuchambua tamathali za usemi katika tungo za kishairi za Kezilahabi, lakini umetupatia mwanga, kuwa ni katika matumizi ya lugha ya kitamadhali ndipo dhamira hufichwa na kuwasilishwa na watunzi wa mashairi kwa hadhira. Tumeutumia ufahamu huu katika kuchunguza matumizi ya lugha ya kitamathali katika mashairi ya magazetini na kisha tukaeleza dhima ya tamathali hizo katika kuwasilisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa.

Omari (2009) katika tasinifu yake ya Uzamivu kuhusu mashairi ya bongo fleva anasema kwamba; mashairi ya bongo fleva yana matumizi makubwa ya lugha ya kitamathali. Anaongeza kwamba, hata nyimbo za mapenzi ambazo ndizo zilizotawala katika aina hiyo ya mashairi nazo hueleza mapenzi hayo kwa kutumia lugha ya kitamathali. Mawazo haya tunakubaliana nayo na tunaungana nayo mkono kwa kuwa ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti huu. Kwa hakika, mawazo haya yanatuonesha kwamba, matumizi ya lugha ya kitamathali hayakwepeki katika

mashairi hasa ikizingatiwa kwamba, ushairi ni sanaa inayotumia lugha ya mkato katika kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Ni katika matumizi ya lugha ya mkato ndimo ambapo tamathali za usemi hupatikana. Kutokana na mawazo haya tumeyasoma mashairi katika magazeti yaliyoteuliwa kwa makini na kisha tukaweza kubainisha tamathali za usemi zilizotumika kuwasilishia ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa.

Msuya na Lupokela (2010) wanaeleza kwamba, ushairi ni muhimu pia katika kueleza masuala ya kisiasa na malezi katika jamii. Wanaeleza kwamba: Viongozi wengi wa kisiasa wanaahidi mambo ambayo hawayatekelezi jambo ambalo linaonesha kwamba hawana maadili ya uongozi. Wanadondoa sehemu ya shairi la *Ndiyo Mzee* lililoimbwa na Prof. Jay (Joseph Haule) katika ubeti ufuatao:

*Cha kwanza nitakachofanya nitafuta umasikini*
*Wanafunzi mkafanyie "pratical" mwezini*
*Kwenye mahospitali nitamwaga dawa kama mchanga*
*na nitafungua akaunti kwa kila mtotomchanga …*

*Je! Wananchi mmesikia? (Ndio mzee)*
*Kuwa huyu jamaa hatufai (ndiyo mzee)*
*Hatumtaki aondoke zake (ndiyo mzee)*
*Tunahakikisha hatumchagui (ndiyo mzee)*
*Kwa sababu huyo jamaa ni mnafiki (ndiyo mzee).*

Hapa Professa Jay (Joseph Haule) anaeleza kwamba, wanasiasa walio wengi hawana maadili mema ya uongozi ndio maana wanawadanganya wananchi kuwa watawafanyia mambo fulani ya kuwaletea maendeleo halafu hawawatekelezei. Mawazo haya ni muafaka katika kusukuma mbele utafiti wetu kwa msingi kwamba, katika ubeti huu ambao umedondolewa hapo juu tumeweza kuona matumizi ya lugha ya kitamathali hasa tamathali ya usemi inayojulikana kama takriri. Ingawa halikuwa lengo la Msuya na Lupokela (2010) kueleza kwa kina juu ya matumizi ya lugha ya

kitamathali katika mashairi waliyohakiki, wametusaidia kupata uelewa kwamba, tamathali za usemi hasa takriri hutumika kwa ajili ya kutoa msisitizo juu ya jambo fulani ambalo msanii anataka jamii ilifahamu na kulipatia uzito jambo hilo katika maisha yao ya kila siku. Mawazo haya yalitufanya tukawa makini katika ukusanyaji wa data, kiasi kwamba tusipitiwe tukaacha kuona matumizi ya takriri katika mashairi ya magazetini, kupitia mashairi yaliyoteuliwa.

Samwel (2010) anaeleza kwamba, mashairi ya mapenzi yanabeba ujumbe kuhusiana na masuala ya kijamii na kisiasa. Anasema hivi kwa sababu baadhi ya wanataaluma, wanajamii, waandishi wa habari na wanaharakati wanadai kwamba, mashairi ya Bongo Fleva yanazungumzia mapenzi kuliko mambo mengine ya msingi. Kwa maoni yake anauona mtazamo huo kuwa ni:

> *Kama hakimu aliyetoa hukumu ya kifungo kwa mshitakiwa bila kumpa nafasi ya kumsikiliza kwa makini. Hii inatokana na ukweli kwamba nyimbo hizo za mapenzi za Bongo fleva, zaidi ya hicho kinachoonekana kuwa ni upotoshaji, zinabeba dhamira muhimu sana ikiwemo siasa na matatizo ya kijamii* (Samwel, 2012:17).

Dondoo hili linathibitishwa kupitia nyimbo mbalimbali kama vile *Baby Gal* ambapo anadondoa hivi:

*Kila ninachofanya unaona hakifai*
*Baby gal mimi nifanyeje?*
*Nimefanya mambo mengi nikuridhishe weee*
*Lakini gal …. Niweje*
*Nifanye kitu gani uelewe*
*Nifanye jambo gani uridhike*
*Baby gal*

*Ulitamani mwenye simu mkononi*
*Ooh nami nikanunua*
*Ulitamani mwenye dread kichwani*
*Ooh kama nywele nilifuga*
*Kama gari, fedha, nyumba nilikupatia*
*Lakini bado penzi letu liliyumba.*

Wimbo huu unawasawiri wengi wa wanasiasa ambao ndoto zao si kunona majimbo yao yanapata maji, shule na kadhalika, bali ni kuona wanapata nafasi walizozitaka ili waishi maisha bora (Madaso, 2009). Mawazo haya ni muafaka katika kusukuma mbele utafiti wetu wa sasa kwa sababu umeonesha kwamba, wimbo ama shairi linaweza kuandikwa kulenga jambo fulani mfano, mapenzi lakini ndani yake kukawa na masuala ya kisiasa. Hili litawezekana kutokana na uwezo wa mhakiki katika kufahamu vipengele mbalimbali vya matumizi ya lugha ya kitamathali. Watu wengi hutoa mahitimishi kwamba, mashairi ya muziki wa Bongo fleva yanazungumzia mapenzi kwa kiasi kikubwa kuliko masuala mengine ya msingi katika jamii. Bila shaka kauli hii hutolewa na watu ambao hawana ujuzi wa kuweza kutambua na kuchambua matumizi ya lugha ya kitamathali yanayojitokeza katika mashairi hayo. Kwa hakika, kama wangekuwa na ujuzi wa kuyafahamu mambo hayo basi wasingethubutu kutoa kauli kama hizo. Kutokana na kulifahamu hili, tumekuwa makini sana katika kukusanya data na kufanya uchambuzi wa kina kuhusiana na tamathali za usemi katika mashairi ya magazetini ili nasi tusijetukawa kama wale ambao hawafahamu kuwa katika mashairi kuna matumizi ya lugha ya kitamathali na lugha hiyo ina nafasi kubwa katika kuwasilisha dhamira mbalimbali kwa jamii.

Alhabib (2012) amefanya utafiti kuhusiana na taswira katika nyimbo za taarab. Katika utafiti wake huo amebainisha kwamba, wasanii wa nyimbo za taarab hutumia taswira kuchora na kuwasilisha masuala yahusuyo maisha katika jamii. Miongoni mwa mambo hayo ni rushwa, unyanyasaji wa kijinsia, ubaguzi, udini, ukabila, njaa, maradhi na ujinga. Kwa maelezo yake, mambo haya ni adui mkubwa wa maendeleo ya jamii na umma kwa ujumla. Tunaungana mkono kwa asilimia mia kwa mia na

mawazo ya Alhabib (2012), kuwa matumizi ya lugha ya taswira yanasawiri kikwelikweli hali halisi ya maisha ya jamii. Mawazo haya yanasukuma mbele utafiti wetu kwa msingi kwamba, taswira ni kipengele kimojawapo kati ya vipengele vingi vya tamathali za usemi. Hivyo basi, katika utafiti wetu tumekutana na matumizi ya lugha iliyojaa taswira na kisha kuzichambua taswira hizo kama zinavyoonekana katika sura ya nne ya tasinifu hii.

Khalifa (2012) anasema, Ushairi wa Kiswahili unamsawiri mwanamke katika mtazamo hasi ukimlinganisha na mwanaume kwa kiasi kikubwa ingawa yapo mashairi machache yanayomsawiri mwanamke katika mtazamo chanya. Kimsingi, tunakubaliana na mawazo ya Khalifa (ameshatajwa) kwa kuwa ni ya kweli na masuala ya jinsia hujitokeza pia katika mashairi ya magazetini. Khalifa (ameshatajwa) aliweza kupata matokeo haya ya utafiti kutokana na ukweli kwamba, alichunguza vipengele vya tamathali za usemi vinavyojitokeza katika mashairi aliyoyatafiti. Mawazo haya tumeyachukuwa na kuyatumia katika utafiti wetu ili kuona kwamba, katika mashairi ya magazetini kunajitokeza tamathali gani za usemi na tamathali hizo zina dhima gani katika kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kwa jamii husika.

Ismail (2010) anaeleza kwamba, mashairi hutumika kwa kiasi kikubwa kama chombo cha kuelimisha jamii kuhusiana na haki za binadamu. Anaeleza:

> *Ushairi wa Kiswahili umekuwa mstari wa mbele katika kutetea haki za binadamu kutokana na madhila yanayomkabili binadamu. Ingawa kwa kiasi kikubwa haibainishi kitu gani kifanyike ili kuondokana na madhila haya lakini ukweli ni kwamba muziki wa Bongo Fleva unaonesha jamii ilivyo na inakoelekea*.

Tunaokubaliana kwa asilimia mia kwa mia na mawazo haya kwa kuwa yanasukuma mbele utafiti wetu. Mawazo anayoyatoa Ismail (ameshatajwa) yana ukweli ambao unaweza kuaminiwa kitaaluma, kwa sababu tunapochunguza matumizi ya lugha ya kitamathali katika mashairi hayo ndipo tunapoona kwamba, mashairi hayo yanatoa ujumbe wa kutetea haki za wananchi. Mawazo na ufahamu huu tumeuchukua na kuufanyia kazi katika utafiti wetu.

Bulaya (2010) katika utafiti wake kuhusu nyimbo za Bongo Fleva anafafanua kwamba, ushairi ni sanaa inayotumika kujadili matatizo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni yanayoikabili jamii. Anathibitisha maelezo yake kwa kutolea mfano, mashairi ya *Ndiyo Mzee* na *Siyo Mzee* yaliyoandikwa na Professa Jay. Mawazo haya ni sahihi kabisa na tunaungana nayo mkono kwa asilimia mia kwa mia. Tunasema hivyo kwa sababu ni dhima ya kazi yoyote ile ya fasihi kusawiri hali halisi ya maisha katika jamii. Mawazo haya yanatoa mwanga wa kusukuma mbele utafiti wetu kwa kuwa ni kutokana na matumizi ya lugha ya kitamathali katika mashairi ya msanii huyo ndipo ambapo hali halisi ya maisha ya jamii inapowasilishwa. Katika utafiti wetu tumechunguza kwa kina namna ushairi wa Kiswahili wa magazetini unavyosawiri hali halisi ya maisha ya jamii kutokana na utumizi wa lugha ya kitamathali inayopatikana katika mashairi hayo.

Arinaitwe (2011) alifanya utafiti katika kuchunguza jinsi nyimbo za Wanyakole zinavyosawiri janga la UKIMWI katika jamii ya Wanayankole huko nchini Uganda. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kwamba, nyimbo za Wanyankole zinachukua nafasi kubwa katika kutoa elimu kwa umma juu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na vile vile, kuhamasisha wananchi kupima kwa hiari ili

kufahamu mustakabali wa afya zao. Mawazo ya Arinaitwe (ametajwa) ambayo pia yanaungwa mkono na Low (2011) ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti huu kwa msingi kwamba, unadokeza kuwa ushairi hutumika kuhamasisha wananchi katika kutekeleza ama kutotekeleza jambo fulani. Hata hivyo, ingawa mtafiti huyu hakuwa na lengo la kuchambua kwa kina matumizi ya lugha ya kitamathali lakini amedokeza kwamba, uhamasishwaji wa wananchi juu ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI hutolewa kupitia lugha ya sitiari, ishara, picha, taswira, tashibiha na tashihisi. Hii inatuonesha kwamba, utafiti wetu haukuwa mbali na utafiti wa Arinaitwe (ameshatajwa) ingawa wetu umejikita zaidi katika kuchunguza matumizi ya lugha ya aina hiyo kwa kina zaidi katika mashairi ya magazetini. Baada ya kuangazia dhamira sehemu inayofuata itaangazia fani katika mashairi.

#### 2.3.1.2 Fani katika Mashairi

Fani ni ule ufundi wa kisanaa anaoutumia mtunzi katika kuisana kazi yake. Fani inajumuisha vipengele vya matumizi ya lugha, wahusika, mandhari, muundo na mtindo katika kazi za fasihi (Wamitila, 2008). Omari (2008) anaeleza kwamba, ushairi hutungwa kwa kutumia lugha mseto na hasa kuchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza na hata lugha za makabila. Hali hii huufanya ushairi kuwa ni chombo hai cha kuwasilishia ujumbe kwa jamii husika. Tunasema hivi kwa sababu, maisha ya kila siku katika jamii hufanywa huku watu wakichanganya lugha katika mawasiliano yao ya kila siku. Huu ndio uhalisia wa maisha. Tunakubaliana kwa asilimia mia kwa mia na mawazo haya kwa msingi kwamba, suala la kuchanganya lugha, halijitokezi katika mashairi ya vitabuni peke yake bali hata katika mashairi ya magazetini. Katika utafiti wetu tumeonesha ni kwa vipi uchanganyaji wa lugha unasidia kujenga matumizi ya lugha ya kitamathali katika mashairi ya magazetini.

Vile vile, kunako miaka ya 1970 kuliibuka mgogoro wa ushairi ambapo kundi la wanapokeo liliwashutumu wanausasa kwamba, wana nia ya kuua ushairi wa Kiswahili kutokana na kuepuka kwao kanuni za utunzi wa ushairi. Wanausasa nao waliwaona wanamapokeo kama watu ambao hawakuutakia mema Ushairi wa Kiswahili kwa kuwa walizingatia mambo ambayo yanaufanya Ushairi wa Kiswahili kudumaa badala ya kuendena na mabadiliko ya jamii (Kezilahabi, 1977; Njogu na Chimerah, 1999). Mzozo huo ulianza pale Kezilahabi alipoandika Diwani ya *Kichomi* (1974). Mayoka (1984) akaandika kwamba, Kezilahabi haandiki ushairi bali anaandika kitu kingine kabisa kisichofanana na ushairi. Mayoka (ameshatajwa) anasema, ushairi wa Kiswahili ni lazima ufuate urari wa vina na mizani kwa kuwa ndio uti wa mgongo wa Ushairi wa Kiswahili. Mawazo haya hayatofautiani na yale ya Kandoro (1978). Hata hivyo, ilitambulika mapema kwamba, kutatokea mgogoro wa Ushairi wa Kiswahili katika kuupinga uandishi wa aina hii ndio maana Topan (1974: xi) akaandika kwamba:

> *Kezilahabi anaufuata mtindo mpya wa kuandika mashairi ya Kiswahili. Na hii ndio njia ya kwanza ya kukuza fasihi ya Kiswahili kwa kuiletea mtindo mpya wa kutunga mashairi*.

Topan (ameshatajwa) anauona utunzi wa Kezilahabi kuwa ni moja ya mambo ambayo yanapaswa kuigwa na kupongezwa na kila anayeitakia mema fasihi ya Kiswahili na maendeleo yake. Mawazo haya yanaonesha kwamba, Topan (ameshatajwa) anaona kwamba, mabadiliko katika nyanja za uchumi, siasa, utamaduni, elimu-taaluma na kadhalika hulazimu fani mbalimbali nazo kubadilika ili kuendana na mabadiliko hayo. Hili linathibitika pale anaposema:

> *Ulikuwa wakati hapo zamani ambapo mshairi wa Kiswahili alikuwa mwenyeji wa mwambao na visiwani*

> *tu. Hivyo, mashairi ya siku hizo yaliandikwa, kufuatana na mila, desturi na sheria za Kipwani. Mawazo yaliyomo huma pia yalihusu maisha na utamaduni wa Kimwambao.*

Mawazo haya kwa hakika yanasukuma mbele utafiti wetu kwa msingi kwamba, yanaona mbababadiliko katika jamii ni mambo ambayo husababisha aina mbalimbali za fani za fasihi nazo kubadilika. Mabadiliko ambayo yaliletwa na Kezilahabi hayakuishia katika kutunga mashairi yasiyofuata urari wa vina na mizani peke yake bali hata katika matumizi ya lugha. Kezilahabi ana matumizi makubwa ya sitiari, ishara, picha, taswira, tanakali sauti na vipengele vingine vya kitamathali. Mabadiliko aliyoyaleta Kezilahabi yamewafikia mpaka washairi wa mashairi ya magazetini na nasi tumeyachambua mashairi hayo na kuweza kuonesha matumizi ya vipengele mbalimbali vya lugha ya kitamathali katika mashairi hayo kama inavyoonekana sura ya nne ya tasinifu hii.

Jilala (2008) alichunguza matumizi ya sitiari katika muziki wa kizazi kipya na kuonesha namna sitiari hizo zinavyowasilisha ujumbe kwa jamii husika. Jilala (tumeshamtaja) amefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kuonesha na kuibua sitiari kutoka katika mashairi ya muziki wa kizazi kipya na kuzitolea ufafanuzi. Sitari hizi zimekuwa na manufaa makubwa katika utafiti huu kwa kuwa tumezitumia kwa minajili ya kutofautisha na kulinganisha na zile zinazotumiwa katika mashairi ya magazetini. Hata hivyo, utafiti wake haukuwa mpana kwa maana ya kuweza kueleza matumizi ya lugha kwa mawanda yake na badala yake umechunguza kipengele kimoja tu cha matumizi ya lugha katika mashairi ya muziki wa kizazi kipya. Utafiti wetu umekuzwa zaidi kwa kuchunguza kwa kina matumizi ya lugha ya kitamathali katika mashairi ya magazetini.

## 2.4 Mashairi ya Magazetini

Mashairi ya magazetini bado hayajafanyiwa utafiti wa kutosha na watafiti wa fasihi ya Kiswahili hususani wale wanaohusika na ushairi. Hata hivyo, wapo baadhi ya watafiti wachache ambao wameshughulikia kazi za sanaa zinazopatikana katika mashairi ya magazetini. Miongoni mwa watafiti hao ni Kitogo (2002), alifanya utafiti kuhusu mchango wa mashairi ya Saadan Kandoro katika maendeleo ya siasa nchini Tanzania. Katika utafiti wake huu alikusanya mashairi ya Saadan Kandoro ambayo yaliandikwa katika magazeti ya *Mambo Leo* na *Baragumu* kisha akayafanyia uchambuzi na kuandika tasinifu yake ya Uzamili. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kwamba, kandoro ametoa mchango mkubwa katika maendeleo ya siasa hapa nchini hasa kuhusiana na siasa za kabla ya Uhuru, wakati wa Uhuru, Ujamaa na Kujitegemea na kipindi cha utandawazi. Utafiti uliofanywa na Kitogo (2002) ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti wetu kwa sababu umetusaidia kufahamu kwamba, ushairi wa magazetini una mchango mkubwa katika kuhamasisha maendeleo mbalimbali ikiwemo siasa katika jamii. Hata hivyo, Kitogo (2002) hakuzungumzia matumizi ya lugha ya kitamathali katika utafiti wake kwa sababu haikuwa sehemu ya madhumuni yake. Utafiti wetu umekwenda mbali zaidi na kuweza kuchunguza matumizi ya lugha ya kitamathali katika mashairi ya magazetini.

Mutembei (2009) alifanya utafiti juu ya mchango wa mashairi ya Kiswahili katika kueleza na kufafanua masuala ya UKIMWI, ugonjwa hatari unaosababisha vifo vya Watanzania wengi. Utafiti huu ulihusisha mashairi ya Kiswahili kwa ujumla na yale yaliyoandikwa magazetini tangu 1986 mpaka 2006. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba, ushairi wa magazetini una nguvu kubwa katika kufafanua na

keleza mambo yanayohusiana na ugonjwa huo wa UKIMWI. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na namna jamii ilivyoupokea ugonjwa huo, namna ya kujikinga na unyanyapaa kwa wagonjwa. Kwa hakika, tunakubaliana kwa asilimia mia kwa mia na maelezo ya Mutembei (2009) kwamba, mashairi ya magazetini yana mchango mkubwa katika kueleza mambo hayo yanayohusiana na ugonjwa hatari wa UKIMWI. Kwa ufahamu wetu, masuala haya yanaelezwa katika ushairi huo kupitia lugha ya kitamathali ambayo imechunguzwa katika utafiti wetu. Mutembei (2009) hakwenda mbali katika kueleza namna lugha ya kitamathali inavyotumika kuibua dhamira mbalimbali jambo ambalo utafiti huu umelishughulikia kwa kina na kufanikiwa kuonesha, namna ambavyo lugha ya kitamathali ilivyo na umuhimu mkubwa katika kuwasilisha ujumbe wa mashairi ya magazetini.

Mtafiti mwingine ambaye ametafiti kazi za magazetini ni Chaligha (2011) ambaye alitafiti masuala ya kijinsia katika katuni zinazochorwa katika magazeti mbalimbali hapa nchini. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kwamba, lugha inayoaandikwa kwa ajili ya kufafanua picha ya katuni ina matumizi makubwa ya lugha ya kishairi. Lugha hiyo ya kishairi imesheheni sitiari, mafumbo, picha, taswira, ishara, tashibiha na tashihisi. Matokeo ya utafiti huu yametupatia mwanga wa kufahamu kwamba, lugha ya mashairi ya magazetini ina utajiri mkubwa wa tamathali za usemi. Utafiti wa Chaligha (2011) haukwenda mbali zaidi katika kuchambua vipengele vya lugha ya tamathali za usemi zaidi ya kuvidokeza tu. Utafiti wetu umezama katika kina kirefu cha mashairi ya magazetini na kutazama ni tamathali gani za usemi zinazojitokeza katika mashairi hayo na kisha dhima ya tamathali hizo za usemi katika kuibua dhamira.

Khalifan (2013) alifanya utafiti katika ngazi ya Uzamivu kuhusu siasa katika ushairi wa Saadan Kandoro. Katika utafiti wake huo alidokeza kwamba, baadhi ya mashairi ya Kandoro aliyoyatumia aliyatoa katika magazeti ya *Baragumu* na *Mambo Leo*, aliyoyapata katika Maktaba Kuu ya Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam katika kitengo chake cha East Afrikana. Anaendelea kueleza kwamba, mashairi hayo yalikuwa na umuhimu mkubwa katika kumwezesha kukamilisha malengo ya utafiti wake na kuonekana kama ulivyo. Katika utafiti wake huo alifanya uchambuzi wa vipengele vya matumizi ya lugha kama vile sitiari, taswira, tanakali sauti, marudirudio, uchanganyaji wa lugha na vipengele vingine. Hata hivyo, kwa kuwa lengo lake halikuwa kuchunguza vipengele hivyo aliishia kuvigusiagusia tu. Utafiti wetu umefanikiwa kuvieleza kwa kina vipengele vya lugha ya kitamathali inayojitokeza katika mashairi ya magazetini.

Khatibu (1987) alikusanya mashairi yaliyohusu Azimio la Arusha kutoka katika magazeti mbalimbali na kuyachambua. Uchambuzi wake ulilenga kubaini mtazamo wa waandishi wa mashairi hayo juu ya Azimio la Arusha. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kwamba, wapo watunzi ambao wanaliona Azimio la Arusha kuwa limefanikiwa katika kuwaletea wananchi maendeleo na wengine wanaliona Azimio hilo kuwa halina tija wala faida yoyote kwa jamii na badala yake liliongeza umasikini.Mawazo haya tunakubalina nayo kutokana na ukweli kwamba, kila mwandishi wa mashairi ya magazetini anao mtazamo wake kuhusu Azimio la Arusha na kwamba, kuyatoa mawazo aliyonayo kama ilivyo ni sahihi kabisa na mawazo aliyoyatoa yanapasa kuheshimiwa. Hata hivyo, utafiti wa Khatibu (ameshatajwa) haukwenda mbali zaidi katika kueleza ni kwa vipi watunzi hao wameweza

kuwasilisha mawazo hayo waliyoyatoa. Hapa tuna maana kwamba, wametumia lugha ya aina gani katika kuwasilisha kazi zao. Utafiti wetu umekwenda mbali zaidi na kufanikiwa kuonesha vipengele vya matumizi ya lugha ya kitamathali ambayo ndiyo iliyotumika katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa na kama ilivyokusudiwa. Tumefanya hivyo kwa kuchunguza masuala ya UKIMWI katika mashairi ya magazetini.

Kezilahabi (1983) anaeleza kwamba, ushairi wa magazetini ulipata umaarufu sana katika miaka ya 1970 kutokana na mgogoro wa ushairi wa Kiswahili uliowahusisha wanausasa na wanamapokeo. Anaeleza kwamba, wahariri wa magazeti husika walitoa kipaumbele kwa mashairi ya kimapokeo kuliko yale ya kisasa kwa sababu wengi kati ya wahariri hao walikuwa ni wapenzi wa mashairi ya kimapokeo. Mawazo ya Kezilahabi yana ukweli ambao unaweza kuaminiwa kitaaluma na hivyo tunayaunga mkono kwa asilimia mia moja. Hata hivyo, Kezilahabi hakwenda mbali katika kuchambua mashairi hayo kwa kuwa haikuwa sehemu ya madhumuni mahususi ya utafiti wake. Utafiti wetu umekwenda mbali zaidi na kufanikiwa kubainisha vipengele vya tamathali za usemi katika mashairi yahusuyo UKIMWI magazetini na kisha kuonesha dhamira mbalimbali kutoka katika tamathali hizo na baadaye tukaonesha dhima ya tamathali za usemi katika kuibua dhamira husika.

## 2.5 Hitimishi

Katika sehemu hii tumeweza kufanya utalii wa kazi tangulizi ambazo zimefanywa katika maeneo makubwa mawili. Kwanza ni zile ambazo zimefanywa katika eneo la ushairi wa Kiswahili kwa ujumla wake na baadae tukahamia katika kazi tangulizi

katika mashairi ya magazetini. Kwa hakika, katika utalii huu hatujapata bahati ya kukutana na utafiti hata mmoja ambao umechunguza vipengele vya tamathali za usemi katika mashairi ya magazetini katika ngazi yoyote ile ya kitaaluma. Utafiti huu ulifanywa ili kuziba pengo hili la kiutafiti na kwa hakika tumefanikiwa kukamilisha utafiti wetu na kujaza pengo hili lililokuwa wazi. Sehemu inayofuata inafafanua nadharia zilizotumika katika utafiti huu.

## 2.6 Mkabala wa Kinadharia

Sehemu hii inatoa maelezo kuhusu nadharia zilizotumika katika utafiti huu. Nadharia ni mawazo au muongozo ambao huelekeza namna jambo fulani linavyopaswa kufanyika au ingepaswa lifanyike, kama tayari lilikuwa limeshafanywa pasipo kuzingatia muongozo huo husika (Kothari, 2008). Utafiti huu umeongozwa na nadharia za Mwitiko wa Msomaji, Simiotiki na Ufeministi.

### 2.6.1 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Nadharia ya mwitiko wa msomaji ni nadharia ya kifasihi inayojikita katika kumwangalia msomaji (hadhira) na uzoefu wake wa kazi za kifasihi, tofauti na nadharia nyingine zinazojikita katika msingi wa kumwangalia mwandishi, maudhui na fani katika kazi za fasihi. Nadharia ya mwitiko wa msomaji iliasisiwa na Hans Robert James, Wolfgang Iser na Harald Invennrich mwishoni mwa miaka ya 1960 na 1970. Waasisi wote wa nadharia hii ni Wajerumani. James alijihusisha kwa kiasi kikubwa na upokezi wa kiujumi kuhusiana na fasihi katika misingi ya ujumi upokezi kuliko wenzake. Mwananadharia huyu anasema kuwa kazi ya kifasihi inapaswa kutazamwa kulingana na mila na desturi au utamaduni wa msomaji, kwani msomaji ana uhuru wa kutafsiri kama aonavyo kutokana na uzoefu wake na si

kutokana na uzoefu wa mwandishi. James anaendelea kusema kuwa kazi ya fasihi inajikita katika ishara na taswira mbalimbali. Kwa hiyo kutokana na ishara na taswira hizo matini za kifasihi haina maana moja ina maana zaidi ya moja (Wamtila, 2002).

Nadharia hii ilipata mashiko mwishoni mwa miaka ya 1960 na mwanzoni mwa miaka ya 1970. Lakini kwa hakika nadharia hii ilikuja kuenea zaidi baada ya wataalamu Hans Robert Jauss na Wolfgang Iser ambao walikuwa ni Maprofesa katika Chuo Kikuu cha Constance Ujerumani, kutoa tafsiri zao za maandishi zilizosisitiza uchunguzi mpya kuhusu usomaji na upokezi wa matini za kifasihi miaka ya 1980. Wafuasi wengine wa nadharia hii ni pamoja na Stanley Fish, Roland Barthes, Norman Holland na wengineo (Wamitila, 2002). Dai kubwa la Stanley Fish kama mfuasi wa nadharia hii ni kwamba, sanaa ya maneno ni kazi iliyo wazi na isiyochanganuliwa kwa sayansi ya kimaabara ambayo inaweza kuifunga na kutoruhusu uhuru wa mawazo. Kazi za kisanaa huwa zinaonesha athari ya mwandishi na jinsi athari hizo zinavyofasiriwa kwa namna tofautitofauti kutokana na msomaji mwenyewe (Wafula na Njogu, 2007). Wolfgang Iser na Stanley Fish huiona kazi ya matini huwa na mapengo mengi ambayo yanamlazimisha msomaji kuyaziba. Katika kuyaziba, msomaji atajikuta ametunga matini nyingine mpya inayotokana na matini ile asilia. Kwa hiyo, jukumu kubwa la msomaji ni kuisoma kazi kwa ufuatiliaji wa hali ya juu na hatimaye kufasili kazi hiyo kutokana na uzoefu pamoja na uwezo wake.

Nadharia hii humsaidia mtafiti kupata maana mbalimbali za matini husika ya kifasihi kulingana na mtazamo wake yeye binafsi kama msomaji wa matini hayo na pia mtazamo wa watafitiwa wake. Kazi ya fasihi kwa kawaida huwa haina maana moja

kwani kila msomaji anaweza kuibua maana kutoka katika kazi ya fasihi kulingana na ufahamu na uzoefu alionao katika maisha kuhusiana na kile kinachoelezwa katika kazi ya fasihi.

### 2.6.2 Nadharia ya Ufeministi

Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007) Ufeministi ni dhana inayoelezea hali na tendo la wanawake wanaodai haki ya kujieleza katika jamii mbalimbali na wanaume wanaounga mkono jitihada za wanawake hao. Ni dhana inayopinga mfumo dume na kujaribu kutatua matatizo yanayowakabili wanawake katika jamii ambazo zinaongozwa na mfumo dume katika maisha yake ya kila siku.

Mackinnon (1991) anaeleza kuwa nadharia ya Kifeministi ilianza mwanzoni mwa miaka ya 1792 huko Ulaya, hususani katika nchi za Uingereza na Marekani. Katika kipindi hicho wanawake hawakuthaminiwa katika jamii zao na walikuwa ni watu waliokuwa katika daraja la chini. Vile vile, wanawake hawakuhusishwa katika shughuli mbalimbali za kijamii, kisiasa na kiuchumi kama vile kupiga kura au kuchaguliwa katika uongozi, kumiliki mali, kupata elimu, kuajiriwa na kadhalika. Mwanamke alionekana kama kiumbe anayestahili kufanya kazi za jikoni na za nyumbani kwa ujumla. Kazi zake ni kama vile kupika, kuosha vyombo, kufua nguo za familia nzima, kusafisha nyumba, kumhudumia mume na kulea watoto (Moore, 1988). Kwa mujibu wa Moore (ameshatajwa) anaiona hali hii kuwa ni unyanyasaji dhidi ya mwanamke.

Nadharia ya Kifeministi ilianza kuzungumzwa katika karne ya 19 na kushika kasi katika miaka ya 1960 na 1970 (Macknnon, 1991). Katika kipindi hiki Wanawake wa

nchi za Magharibi, yaani Marekani na mataifa ya Ulaya walianza kuzungumzia matatizo yanayowakabili wananchi wa tabaka la chini wakiwemo wanawake. Matatizo hayo yalikuwa ni ya kiuchumi, kisiasa na kijamii (Wafula na Njogu 2007).

Wamitila (2002) anaeleza kuwa baadhi ya kazi za mwanzo kuyafafanua masuala ya wanawake kinadharia ni *A Vindization of the right of a woman* (1792) ya Mary Wollstonecraft. Pia kazi nyingine ni *The Second Sex* (1952) ya Simone de Beauvior ambaye alikosoa na kushambulia baadhi ya asasi zinazochangia katika kumdhalilisha au kumdunisha mwanamke, kama vile dini, ndoa na utamaduni. Kwa mujibu wa Wamitila (ameshatajwa), Simone de Beauvior anaeleza kuwa utamaduni anamokulia mwanamke unachangia katika kumdidimiza katika hali ya unyonge. Utamaduni huo unamfanya na kumlazimisha kukubali kuwa yeye ni kiumbe duni. Baada ya kukubali hali hiyo, mwanamke anaishia kuwa chombo cha mfumo wa jamii cha kuendeleza utamaduni huo. Mfano, ndoa ni asasi mojawapo ya kiutamaduni inayoendeleza ukandamizaji wa wanawake ambayo inamjenga kwenye imani na uwezo mkubwa alionao mwanaume na kuishia kumuangalia mwanamke kama chombo cha starehe.

Wamitila (2002) anandelea kueleza kuwa uhakiki wa kifeministi wa Kimarekani unahusishwa na kazi ya Mary Ellman, *Thinking about Woman*. Dhamira ya kimsingi ya mwandishi huyu ilikuwa ni kuangaza jinsi wanawake walivyosawiriwa kwa namna mbalimbali katika kazi zilizoandikwa na wanaume. Mwandishi huyu alimulika pia jinsi baadhi ya waandishi wa kike walivyouendeleza usawiri huo hasi wa wanawake katika kazi zao. Hali hii ilitokana na wao kukulia kwenye jamii zilizotawaliwa na itikadi ya kiume au “ubabedume” na kuishia kufyonza baadhi ya mitazamo kumhusu mwanamke ambayo inaakisiwa kwenye kazi zao.

Ntarangwi (2004) anasema kuwa nadharia ya Kifeministi ni siasa kutokana na ukweli kwamba inaelekeza kubadili uhusiano uliopo kati ya wanaume na wanawake. Uhusiano ambao umeranda katika nyanja nyingi za maisha kama vile familia, elimu, kazi, siasa, utamaduni na hata mambo ya starehe na anasa. Hivyo basi, ni nadharia inayotaka kuelekeza wanajamii namna ya kuishi, kutenda, na jinsi watakavyokuwa siku za usoni.

Kwa upande wa fasihi, Ntarangwi (keshatajwa) anasema kuwa nadharia ya ufeministi imekuja kwa azma ya kusoma upya kazi za fasihi ili kusisitiza vipengele vilivyopuuzwa na wahakiki wengi ambavyo hawangeviona kwa sababu walikuwa wanafanya kazi katika nadharia za kijadi zilizomtukuza mwanaume. Ntaragwi (2004) anaeleza kuwa, baadhi ya mambo yanayozungumzwa na muungano huu ni kuunda upya uhalisia wa mwanamke kwa kupanga na kudhihirisha miundo ya kijadi ambayo inamtukuza mwanaume na kumkandamiza mwanamke.

Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007) nadharia ya Kifeministi inaongozwa na misingi kadhaa, nayo ni kutumia fasihi kama jukwaa la kuelezea kwa uyakinifu hali ya mwanamke, kusawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na kupigania jamii mpya yenye msingi katika amali za kibinadamu. Misingi mingine ni kuhamasisha utungaji wa kazi za kisanaa zenye wahusika wa kike wanaoweza kuigwa ambao hawategemei wanaume ili wajulikane, huzindua mwamko kwa upande wa wanawake jinsi wanavyojiona na huvumbua na kuziweka wazi kazi za fasihi zilizotungwa na wanawake.

Kimsingi, nadharia ya Kifeministi imegawanyika katika makundi kadhaa: Miongoni mwa makundi hayo ni “Radical Feminism”, “Marxist Feminism”, “Cultural

Feminism” na “Political Feminism” (Moore, 1988). Tukianza na kundi la kwanza ambalo ni Radical Feminism (Wanaujinsia wenye msimamo mkali) wao wanadai kwamba, ndoa ndio taasisi ya kwanza inayohusika katika kunyanyasa na kumnyonya mwanamke. Ni katika ndoa ndipo mwanamke anafanywa kuwa chombo cha starehe na mtumishi wa mwanaume pasipo malipo huku mwanaume akienda kazini na kulipwa mshahara. Kwa maoni yao ili haki sawa ipatikane baina ya mwanamke na mwanaume basi ni lazima mwanamke aache uhusiano na mwanaume (Eisenstein, 1979). Kwa maneno mengine suala la ndoa kati ya mwanamke na mwanaume lisiwepo na kama mwanamke anahitaji mtoto atumie uzazi wa chupa.

Kwa upande wa Marxist Feminism (Wanaujinsia wa Kimarx) wanadai kwamba jamii imeundwa kwa matabaka mawili, tabaka la walionacho na lile la wasionacho. Wanawake waliowengi wanaingia katika tabaka la wasionacho kutokana na mfumo dume uliotawala katika jamii. Njia pekee ya kuwaokoa wanawake kutoka katika mfumo huu ni serikali kuingilia kati na kuundesha uchumi pamoja na kutoa huduma muhimu kwa watu wote. Sekta binafsi ikiachwa itoe huduma hizo ni wazi kwamba mwanamke ataendelea kuwa duni (Leacock, 1981).

Cultural Feminism (Wanaujinsia wa Kiutamaduni), kwa upande wao wanadai kwamba, suala la mwanamke kujipamba na kujipodoa ni la asili na ni haki ya mwanamke kufanya hivyo (Leacock, 1981). Haki hii ya mwanamke isije ikachukuliwa kama ni sababu ya kumuona mwanamke kama chombo cha kumstarehesha mwanaume na hivyo kumgandamiza mwanamke.

Kwa upande wa Political Feminism (Wanaujinsia wa Kisiasa), wao wanadai kwamba wanaume ndio waliotawala katika nafasi muhimu za uongozi huku mwanamke

akiachwa nyuma. Kutokana na hali hii masuala ya wanawake pamoja na haki zao hayazungumzwi na kuundiwa mikakati madhubuti ikilinganishwa na yale yanayowahusu wanaume (Leacock, 1981). Kwa mantiki hiyo, ni lazima wanawake washirikishwe katika uongozi kwa kupewa nafasi sawa na wanaume ndiyo masuala ya wanawake yatapewa kipaumbele katika miradi ya maendeleo.

Kimsingi, makundi yote haya yanaijenga nadharia ya Ufeministi kuonekana kuwa ni imara katika kutatua matatizo ya wanawake na kuleta usawa katika jamii. Nadharia hii inatusaidia kuelewa kwamba, mwanamke si chombo cha starehe kwa mwanaume kwani wote ni wanaadamu na wanapaswa kuwa na hadhi iliyosawa katika jamii. Ubora mwingine wa nadharia hii ni kwamba imeweza kuainisha sababu zinazofanya mwanamke aonekane kiumbe duni katika jamii. Sababu kubwa kuliko zote ni kwamba, mfumo dume uliotawala katika jamii ndio uliosababisha mwanamke kutazamwa kama kiumbe duni.

Kwa upande wa mapungufu ya nadharia hii, ni kuwa, madai kwamba ndoa ndiyo taasisi inayofanya mwanamke anyanyasike na aonekane kama chombo cha starehe na hivyo kutokuwepo kwa ndoa kutaepusha mwanamke kunyanyasika si sahihi sana. Taasisi ya ndoa imeundwa katika jamii kutokana na misingi ya utamaduni wa jamii na hivyo kuondoa utamaduni huu si kazi rahisi kwa sababu ndiyo ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla.

Nadharia hii imetusaidia katika kutimiza madhumuni mahususi ya pili juu ya dhamira zinazowasilishwa na matumizi ya lugha ya kitamathali katika mashairi ya magazetini. Kwa mfano, mwanamke anaonekana kulaumiwa kuwa ndiye anayetumika katika kusambaza na kueneza UKIMWI katika jamii. Kupitia nadharia

hii tumeweza kubainisha sababu kuu zinazofanya mwanamke kulaumiwa juu ya kuenea kwa UKIMWI. Nadharia nyingine ya uhakiki wa kifasihi ni Simiotiki.

### 2.6.3 Nadharia ya Simiotiki

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Simiotiki katika uchambuzi wa data. Inaelezwa kwamba Simiotiki ni neno la Kiyunani lenye maana ya Ishara, Picha na Taswira. Kwa ujumla nadharia hii inahusika na ishara pamoja na uashiriaji katika kazi ya kifasihi (Wamitila, 2002). Nadharia hii inawazesha mhakiki kutambua picha na Ishara mbalimbali zinazojitokeza katika kazi ya kifasihi na kuzitolea maana.

Wamitila (2002) anaeleza kwamba, katika lugha kuna vitu viwili ambavyo ni kitaja (a signifier), yaani umbo ambao alama inachukua na kirejelee kiwakilishwayo na alama hiyo. Maelezo haya yanatupatia uelewa kwamba, kuna kitaja na kirejelee ambapo mahusiano ya viwili hivyo ni ya kubuni tu, yaani hutegemea utamaduni wa jamii husika. Inawezekana kabisa kukawa hakuna mahusiano ya moja kwa moja baina ya kitaja na kirejelee, lakini kama wanajamii wamekubaliana juu ya matumizi yake basi hutumika na kuelewana baina yao.

Barthes (1994) anataja kwamba, nadharia ya Simiotiki inahusiana sana na utengenezwaji wa misimbo mbalimbali katika kazi ya fasihi. Misimbo hiyo ni ule wa Kimatukio, Kihemenitiki, Kiseme, Ki-ishara na Kirejelezi. Aina hizi za misimbo hutumika katika kufanya uchambuzi wa kazi za kifasihi mashairi ya magazetini yakiwa ni mojawapo. Misimbo hii imetusaidia katika kufanya uchambuzi wa matumizi ya lugha ya kitamathali itumiwayo na washairi wa magazetini. Kwa kawaida lugha ya kitamathali huwa ni ya picha, ishara, mafumbo na taswira ambazo

huweza kuchambuliwa vizuri kwa kutumia nadharia ya Simiotiki. Nadharia hii husaidia kuweka bayana dhamira zilizofichwa katika lugha ya kuficha na kutumia misimbo badala ya kueleza mambo kwa wazi. Hivyo, madhumuni mahususi ya kwanza ya utafiti huu yamekamilika kutokana na msaada wa nadharia ya Simiotiki.

## 2.7 Hitimishi

Sura hii imepitia kazi tangulizi ambazo zinahusiana na mada ya utafiti na kuweza kubainisha pengo la utafiti. Kazi zilizopitiwa ni zile zinazohusu dhamira na fani katika ushairi wa Kiswahili kwa ujumla. Kisha zikafuatia kazi zilizotafiti mashairi ya magazetini. Mwishoni mwa sura hii kumefafanuliwa nadharia ambazo zimetumika katika kuwezesha kuchambuliwa kwa data za utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Kothari (2008) anaeleza kwamba mbinu za utafiti ni uti wa mgongo wa utafiti wa kitaaluma. Kwa kulitambua hilo, sura hii inawasilisha mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti. Vile vile, sura hii inawasilisha mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa katika utafiti ikiwemo maadili ya utafiti. Sura inaanza kuwasilisha vipengele hivyo kama ifuatavyo:

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika katika jiji la Dar es Salaam ambapo Maktaba kama za Chuo Kikuu Huria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili na Makavazi yake ndizo zilizotumika katika kukusanyia data za utafiti. Kimsingi, maktaba hizi zimesaidia kutupatia magazeti mbalimbali yaliyotupatia data za utafiti. Kitengo cha East Afrikana katika maktaba ya Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam kina hazina kubwa ya magazeti ambayo ndiyo tuliyoyatumia kwa ajili ya kukusanya data za utafiti huu. Vilevile, watafitiwa wa utafiti wetu wanapatikana katika jiji la Dar es salaam. Watafitiwa hawa wameelezwa katika sehemu ya uteuzi wa watafitiwa.

## 3.3 Umbo la Utafiti

Umbo la utafiti ni ramani inayochorwa kuonesha sura nzima ya utafiti inavyopaswa kuwa tangu katika ukusanyaji wa data mpaka uandishi wa tasinifu nzima (Kothari, 2008; Babbie, 1999; Yin, 1994). Kuna aina mbalimbali za umbo la utafiti na katika utafiti huu tumetumia uchunguzi kifani. Uchunguzi kifani ni aina ya umbo la utafiti, ambalo humpa mtafiti uhuru wa kuteua jambo moja mahususi ambalo atalichunguza

kwa undani na kulitolea mahitimishi muafaka (Creswell, 2009; Robson, 2007). Good (1966) anaeleza kwamba, uchunguzi kifani ni mbinu nzuri ya utafiti kwa sababu ni ya uhakika inayomuwezesha mtafiti kupata taarifa muhimu na sahihi kwa kutumia muda na gharama ndogo ikilinganishwa na mbinu nyingine. Vile vile, uchunguzi kifani humuwezesha mtafiti kuuelewa muktadha mzima wa jambo analolitafiti na hivyo kuwa rahisi kwake kukamilisha malengo ya utafiti wake. Mbinu ya uchunguzi kifani inamsaidia mtafiti kujibu maswali kama vile nini? kwa nini? kwa sababu gani? Kivipi? Na kadhalika (Kothari, 2009). Katika utafiti wetu tumeteua magazeti ya *Uhuru*, *Nipashe*, *Majira*, *Mtanzania* na *Mzalendo* na kushughulikia mashairi yanayopatikana katika magazeti hayo.

## 3.4 Watafitiwa

Watafitiwa hurejelea idadi ya watu, na vitu ambavyo mtafiti anavitumia kama watafitiwa wa utafiti wake. Newman (2006) anafasili watafitiwa kama mkusanyiko wa watu/vitu katika hali na mazingira tofauti ambavyo ndivyo hutoa data za utafiti husika. Watafitiwa katika utafiti huu ni magazeti matano yanayoandika mashairi ya Kiswahili. Magazeti hayo ni *Uhuru*, *Nipashe*, *Majira* na *Mzalendo* na *Mtanzania*. Sababu kubwa ya kuteua magazeti matano ni ili kutuwezesha kupata data ya kutosha, kwa sababu si kila toleo la gazeti huwa linakuwa na mashairi. Wakati mwingine gazeti fulani linatoa shairi au mashairi na lingine halitoi. Hivyo basi, kwa kuteua magazeti matano tumeweza kukusanya data ya kutosha kukamilisha madhumuni ya utafiti wetu. Pia, tuliteua watafitiwa kumi na kufanya nao usaili uliowezesha kukamilisha lengo mahususi la tatu la utafiti wetu. Watafitiwa hawa 10 wamepatikanaje na kutoka wapi imefafanuliwa katika sehemu inayofuata.

### 3.4.1 Uteuzi wa Watafitiwa

Babbie (1999) anaeleza kwamba, sampuli ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa katika jumla kuu ya watafitiwa, ambalo ndilo hutoa data za kuwakilisha kundi zima. Uteuzi wa watafitiwa ni kitendo cha kuteua washiriki, katika kundi kubwa la watafitiwa ili kupata idadi ndogo ya watafitiwa watakaotumiwa kutoa data za utafiti. Utafiti huu umetumia aina ya Sampuli Lengwa katika kukusanya data za utafiti. Sampuli Lengwa ni aina ya sampuli ambayo humwezesha mtafiti kuteua watafitiwa wake akiwa anatambua kwamba, watamsaidia kupata data anazozihitaji ili kujibu maswali ya utafiti (Kothari, 2009). Sampuli Lengwa ilitumika kuteua magazeti 5 ambayo yametumika katika kutupatia data za utafiti. Tumeyateua magazeti haya kwa sababu tunafahamu kwamba, hutoa mashairi katika matoleo yake mara kwa mara ingawa katika baadhi ya matoleo huwa hakuna mashairi. Sampuli lengwa imetusaidia kutumia muda wetu vizuri katika ukusanyaji wa data kwa kutopoteza muda kusoma magazeti mengi ambayo mengine hayatoi mashairi.

Vile vile, tumetumia Sampuli lengwa kuwapata watafitiwa 10 waliotupatia data za kukamilisha lengo kuu la utafiti wetu. Watafitiwa hawa ni wasomaji wa mashairi katika magazeti teule. Pia, tumetumia sampuli Nasibu kutupatia data katika mashairi ya magazeti tuliyoyateua. Kila tulipokuwa tukisoma shairi na kukutana na kitu tunachokitaka katika shairi husika basi tulikidondoa katika daftari maalumu la kukusanyia data kwa ajili ya kufanyiwa uchambuzi. Mashairi katika magazeti yote yaliyoteuliwa yalipewa nafasi sawa ya kutoa data za kukamilisha madhumuni mahususi ya utafiti huu.

## 3.5 Vyanzo vya Data

Kimsingi, kuna vyanzo vikuu viwili vya kupata data za utafiti wa kitaaluma kama huu. Vyanzo hivyo vinajumuisha data za msingi na data za upili. Maelezo ya kina kuhusiana na vyanzo hivi yanatolewa hapa chini kama ifuatavyo:

### 3.5.1 Data za Msingi

Data za msingi ni halisi na hazijawahi kukusanywa na mtafiti yeyote yule kwa madhumuni ya kujibu maswali ya utafiti yanayojibiwa katika utafiti huu (Kodhari, 2008). Ni data ghafi na ndio kwanza zinakusanywa kwa mara ya kwanza ili kujaza pengo la utafiti lililoachwa na watafiti tangulizi. Data za msingi katika utafiti huu zimekusanywa kutoka katika mashairi yanayopatikana katika magazeti ya *Mzalendo*, *Uhuru*, *Nipashe*, *Majira* na *Mtanzania*.

### 3.5.2 Data za Upili

Data hizi ni zile ambazo tayari zimekwishakusanywa na watafiti wengine kwa minajili ya kujibu maswali ya utafiti wao. Data hizi zinapatikana katika vitabu, makala, majarida, tasinifu, tovuti na wavuti. Young (1984) anaieleza mbinu hii kuwa ni ya kukusanyia data mezani bila kuwatafuta/kuwafuata watafitiwa na kuwahoji ama kuwasaili. Data hizi zilikusanywa kutoka katika machapisho ambayo yalihusiana na mada ya utafiti huu. Machapisho hayo ni pamoja na tasinifu, vitabu, makala, majarida, wavuti na tovuti.

## 3.6 Mbinu ya Ukusanyaji wa Data

Utafiti huu umetumia mbinu za uchambuzi wa kimaudhui na usaili katika kukusanya data za utafiti. Mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui inaelezwa hapa chini kama ifuatavyo:

### 3.6.1 Uchambuzi wa Kimaudhui

Mbinu hii hujulikana kama *Content Analysis* kwa Kiingereza. Uchambuzi wa kimaudhui ni mbinu ambayo inampa mtafiti fursa ya kusoma andiko husika kwa utulivu na umakini kisha akaweza kubaini data ambazo zinasaidia kujibu maswali ya utafiti wake (Leininger, 1985). Mtafiti aliitumia mbinu hii kukusanyia data kutoka mashairi yaliyopo katika magazeti teuliwa na baada ya hapo kila alipoona shairi ama ubeti au kipande cha msitari wa shairi kinachohusiana na mada ya utafiti alikinukuu katika shajara maalumu na kisha kuendelea tena kusoma kazi nyingine. Kwa kufanya hivyo, mtafiti pamoja na wasaidizi wake waliweza kunukuu/kudondoa baadhi ya beti, mshororo ama kipande cha mshororo kwa ajili ya kukitumia baadaye katika uchambuzi wa data. Ukirejelea sura ya nne ya tasinifu hii, utaona kwamba, yapo madondoo kadhaa ambayo yametumiwa na mtafiti katika kujenga ama kushadidia hoja fulani kwa minajili ya kujibu maswali ya utafiti. Madondoo hayo yalikusanywa katika kipindi cha ukusanyaji wa data. Kothari (2008) anaeleza kwamba mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui ni nzuri na haipotezi muda katika ukusanyaji wa data. Mbinu hii ni ya haraka hasa pale mtafiti anapotulizana na kusoma andiko husika basi huwa rahisi kumpatia data muafaka kwa minajili ya utafiti wake.

### 3.6.2 Usaili

Usaili ni mbinu ya kukusanya data za msingi kwa njia ya mazungumzo ya ana kwa ana kati ya mtafiti na mtafitiwa wake. Kothari (2008) anaeleza kwamba, mtafiti huandaa dodoso ambalo ndani mwake mna maswali ya kuwauliza watafitiwa wake kwa nia ya kupata data ambazo zitakamilisha malengo ya utafiti wake. Katika kutumia mbinu hii, tuliandaa maswali katika dodoso na kuyatumia katika

mazungumzo yetu na wasomaji wa mashairi ya magazetini katika Jiji la Dar es Salaam. Mbinu hii inatoa fursa ya mtafiti kuuliza maswali mengi kadiri awezavyo na hivyo kupata maelezo ya kina kuhusiana na utafiti wake kutoka kwa mtafitiwa. Hata hivyo, mbinu hii hutumia muda mrefu sana tangu kuanza mpaka kumaliza usaili na mtafitiwa mmoja kabla ya kwenda kwa mtafitiwa mwingine. Mtafiti na wasaidizi wake walijitahidi kuwarudisha watafitiwa katika mada ili kuepuka kutumia muda mrefu kujadili mambo yasiyohitajika katika utafiti.

## 3.7 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti (Bogdan na Biklen, 1992, Taylor na Bogdan 1984). Jambo hili limeweza kufanyika kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo. Mbinu hii humruhusu mtafiti kulisoma shairi fulani kwa minajili ya kuelewa maudhui, falsafa, mtazamo, na fani ya shairi. Baada ya kuyafahamu hayo mtafiti hutumia njia ya maelezo katika kuzichambua data hizo na kuzifanya rahisi kueleweka kwa msomaji. Uchambuzi wa data za utafiti huu ulifanywa kwa namna ifuatayo:

Hatua ya kwanza ilikuwa ni kupanga data zilizokusanywa kulingana na madhumuni mahususi ya utafiti. Hatua ya pili ikawa ni kuunda mada kuu na mada ndogo ndogo kwa kila dhumuni mahususi la utafiti. Lengo kuu la kuunda mada kuu na ndogondogo ilikuwa ni kurahisisha kazi ya uchambuzi wa data. Pia, uundwaji wa mada hizo humuongoza mtafiti katika kuzingatia mambo ya msingi ya kuchambua na kutopoteza muda kuchambua mambo yasiyohitajika. Hatua ya tatu ilikuwa ni kuanza kazi ya kuchambua data kwa kuzidondoa na kuzitolea maelezo yanayohusiana na

mada ya utafiti. Uchambuzi ulianza kwa kudondoa beti za mashairi kutoka katika magazeti teule na kuzitolea ufafanuzi kimaelezo. Kwa nia ya kuziimarisha data hizi, data zilizokusanywa kwa njia ya usaili zilitumika kusisitiza na kuimarisha data za mashairi ya magazetini.

### 3.8 Usahihi wa Mbinu za Utafiti

Utafiti wa Kitaaluma hufanywa kwa kuzingatia kanuni/mbinu mbalimbali zinazokubalika ili kuufanya kuwa ni utafiti usioeleza mambo ya uongo yasiyo na ukweli wa aina yoyote. Utafiti huu umetumia mbinu za uchambuzi wa kimaudhui na usaili katika kukusanya data za utafiti. Kila mbinu kati ya hizi ina mapungufu na uimara wake. Hivyo, mapungufu ya mbinu moja yaliimarishwa na uimara wa mbinu nyingine na kusaidia kupatikana kwa data sahihi zilizowezesha kutimia kwa lengo kuu la utafiti huu. Mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo ndiyo iliyotumika katika kuchambua data za utafiti huu. Mbinu hii ni sahihi katika uchambuzi wa matini za kifasihi kama yalivyo mashairi ya magazetini. Utafiti huu haukuhusisha data za kimahesabu kwa hiyo zilihitaji maelezo tu na siyo chati na majedwali katika uchambuzi. Nadharia za Mwitiko wa Msomaji na Simiotiki ndio zilizoongoza uchambuzi wa data za utafiti huu. Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ilitupatia uhuru wa kuchambua data kutokana na uzoefu tulionao katika maisha na katika taalimu ya fasihi ya Kiswahili. Nadharia ya Simiotiki ilikuwa ni muafaka katika uchambuzi wa tamathali za usemi kama vile ishara, picha na taswira.

#### 3.8.1 Kuaminika kwa Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huaminika pale ambapo taratibu zote za utafiti zimefuatwa kama ilivyoainishwa katika pendekezo la utafiti lililowasilishwa na kujadiliwa katika

semina kabla mwanafunzi hajaruhusiwa kukusanya data za utafiti wake (Babbie, 1999). Utafiti huu umefuata taratibu zote muhimu za kufanyika kwa utafiti wa kitaalimu. Mbinu na nadharia zote za utafiti zilitumiwa kama inavyopasa, na pale mtafiti alipopata ugumu alikwenda kwa msimamizi wake na kufanya mashauriano yaliyoifanya kazi hii kuonekana kama ilivyo sasa.

## 3.9 Maadili ya Utafiti

Maadili ni neno pana linalorejelea kuheshimu taratibu, miiko, mila na desturi zinazoongoza maisha au jambo/shughuli fulani katika jamii (Kumar, 1999). Utafiti kama ilivyo kwa mambo mbalimbali katika jamii una miiko yake ambayo inapaswa kuzingatiwa. Utafiti huu umefanywa kwa kuzingatia miiko yote ya utafiti. Madondoo yote yanayojitokeza katika utafiti huu yamefanywa kwa usahihi na kwamba yote yamedondolewa katika kazi zilizoteuliwa na si vinginevyo. Watafitiwa waliomba idhini ya kufanyiwa usaili na pindi walipokubali ndipo usaili ukafanyika. Kwa wale ambao hawakuwa tayari kusailiwa; hawakulazimishwa kushiriki katika usaili kwa kuheshimiwa utashi wao. Pia, watafitiwa wote walitaarifiwa kuwa, utafiti huu ulikuwa ni wa kitaaluma usiokuwa na lengo la biashara na nia za kisiasa.

## 3.10 Hitimishi

Sura hii imewasilisha mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti zilizosaidia kujibu maswali ya utafiti na kuwezesha kukamilika kwa lengo kuu la utafiti. Mbinu hizo za utafiti zimekuwa ndio dira na muongozo unaoifanya kazi hii kuonekana kama ilivyo. Vipengele vilivyowasilishwa katika sura hii ni pamoja, na eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, watafitiwa na uteuzi wake. Vipengele vingine ni vyanzo vya data za msingi na upili, mbinu za ukusanyaji wa data; uchambuzi wa

kimaudhui na usaili. Kipengele kingine ni cha uchambuzi wa data ambampo mkabala wa kimaelezo ndio uliotumia kuchambua data za utafiti huu. Sura inayofuata inawasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii tunafanya uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti kwa nia ya kukamilisha madhumuni mahususi ya utafiti wetu. Uwasilishaji, uchamuzi na mjadala wa data za utafiti umefanywa kwa kuzingatia madhumuni mahususi ambapo tumeanza na dhumuni mahususi la kwanza kisha la pili na baadaye la tatu. Miongoni mwa yaliyowasilishwa katika sura hii mintaarafu dhumuni mahususi la kwanza ni tamathali za usemi zinazojitokeza katika mashairi ya UKIMWI ya magazetini. Tamathali hizo ni taswira, sitiari, takriri, tafsida, tashibiha na ishara. Kwa upande wa dhumuni mahususi la pili tumeeleza dhamira zinazojengwa na tamathali za usemi katika mashairi ya magazetini kama vile, UKIMWI na umalaya, chanzo cha UKIMWI, unyanyapaa na kinga ya UKIMWI. Katika dhumuni mahususi la tatu tumeonesha dhima za tamathali za usemi zilizotumika katika mashairi ya magazetini kifani na kimaudhui. Dhima hizo kwa upande wa maudhui ni kuhamasisha, kufafanua na mawasiliano huku za upande wa fani zikiwa ni kupamba lugha na kuongoza uteuzi wa vipengele vingine vya kifani katika utunzi wa shairi. Baada ya utangulizi huu ni vema sasa tuanze kuwasilisha data zinazohusiana na dhumuni mahususi la kwanza katika utafiti wetu kama ifuatavyo:

## 4.2 Tamathali za Usemi katika Mashairi ya Magazetini

### 4.2.1 Taswira

Taswira ni mbinu ya matumizi picha katika utungo na katika mawazo ya msomaji wa utungo huo (Mulokozi na Kahigi, 1979). Wataalamu hawa wanaeleza kuwa picha ni matumizi ya lugha yanayopambanuliwa na uteuzi mzuri wa maneno, uangalifu na

udhahiri wa maelezo yenye kuhusisha na kujumuisha dhana moja ili kuleta taswira na athari maalumu katika mawazo ya msomaji. Kwa upande wao Njogu na Chimerah (1999) wanasema kwamba, taswira ni lazima ijengwe kutokana na msingi wa ulinganifu baina ya dhana, jambo au chombo kinachorejelewa na taswira ile iliyochorwa. Senkoro (2011) anaeleza kwamba matumizi mazuri ya taswira hutegemea utunzi wa msanii wa kuweza kuchota mambo yanayomzunguka na jamii yake, na pia kutoka katika historia na sehemu nyingine za maisha azijuazo. Anaendelea kueleza kuwa taswira husaidia picha kuganda akilini na kunasisha ujumbe wa msanii kwa wasikilizaji au wasomaji husika. Senkoro (1988) anaendelea kueleza kuwa taswira zinaweza kugawanywa katika makundi matatu: taswira zionekanazo, taswira za mawazo na taswira za hisi. Ni ukweli usiopingika kwamba, aina hizi za taswira zilizoelezwa na Senkoro zinajitokeza kwa kiasi kikubwa katika mashairi ya magazetini yanayozungumzia masuala ya UKIMWI. Miongoni mwa taswira hizo ni hizi zifuatazo:

Katika shairi la “Ni mgeni gani” lililotungwa na Emmanuel Lutashobya, kunasemwa:

Nimepata mgeni, asokuwa na barua
Hakupiga hata honi, kwa ghafla akatua
Kwa tuli akakuneni, tunu hakuzikunjua
Fumbo hili kufumbua, huyu ni mgeni gani?

Kwa athari machoni, magonjwa kayaacheni
Kakimbia mitaani, huku akitambeni
Vita nikatangazeni, mgeni simtamani
Fumbo hili kufumbua, huyu ni mgeni gani?
Suluhisho kwa mgeni, apigwe vita nyumbani
Kwani hana maskani, usiku haonekani
Zawadize mikononi, zina maudhi mwilini
Fumbo hili kufumbua, huyu ni mgeni gani
(UHURU, Julai 9, 1982).

Katika beti hizi tatu mshairi anatupatia simulizi kuhusiana na mgeni ambaye amezitembelea kaya mbalimbali lakini mgeni huyu hafahamiki vizuri kwa wenyeji wake. Bila shaka mgeni anayezungumzwa hapa ni ugonjwa hatari wa UKIMWI. Mtunzi anaposema mgeni huyu hafahamiki vizuri kwa wenyeji ana maana kwamba, UKIMWI ulipoingia nchini Tanzania katika miaka ya 1980 kwa mara ya kwanza katika mkoa wa Kagera uliua watu wengi huku watu hao wakiwa bado hawafahamu hasa ni kitu gani ambacho kinawaua watu wao (Mutembei, 2009).

Vile vile, mtuzi wa shairi anaendelea kutupatia taswira ya ugojwa wa UKIMWI pale anapotueleza kuwa, mgeni aliyekuja hakutoa raarifa ya ujio wake kwa mwenyeji. Hii ina maana kwamba, ugonjwa wa UKIMWI humpata mtu bila kumpatia taarifa yoyote kama mtu huyo yeye mwenyewe, hakuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huo hatari katika maisha ya mwanadamu. Jambo la kuelewa hapa ni kwamba, UKIMWI ulipoingia hapa nchini kwa mara ya kwanza, jamii haikuwa inaufahamu na hivyo kutokuwa na ufahamu pia wa mbinu za kujikinga na ugonjwa huo. Badala yake wanajamii wengi walijikita katika kuamini kwamba, mtu anayeugua UKIMWI amerogwa na hivyo kutumia muda mwingi kwenda kwa waganga kwa ajili ya kumtafuta mrogaji kwa nia ya kupambana naye (Mutembei, 2009). Hata hivyo, hili halikuwa suluhisho, kwani watu wengi walipoteza maisha huku baadhi ya kaya nyingi hasa za mkoa wa Kagera, zikibakiwa na watoto peke yao kufuatia wazazi wao wote kufariki dunia.

Si hivyo tu bali pia, mtunzi wa shairi hili anatupatia taswira kwamba, UKIMWI ulikuwa ni tishio kubwa kwa mwanadamu katika miaka hiyo ya mwanzoni ya kuingia kwake. Hii ilisababishwa na wananchi pamoja na serikali yao

kutokuufahamu ugonjwa huo vizuri. Anasema haya katika ubeti wa pili wa shairi lake pale anaposema, “mgeni huyu ambaye ni UKIMWI ameingia mitaani huku akitamba na hakuna mtu wa kuweza kupambana naye.” Kwa kawaida, mgeni anapofika mahali kwa mara ya kwanza huwa anakuwa si mwenyeji wa mazingira ya eneo hilo, na hivyo kuhitajia muongozo wa mwenyeji au wenyeji wake anapotaka kwenda mahali popote ndani ya eneo hilo. Jambo la kushangaza ni kwamba, mgeni huyu ambaye ni UKIMWI amekuwa ni mwenyeji wa mazingira kuliko hata wenyeji wake. Kwa mantiki hiyo, amekuwa akimshambulia mwenyeji wake kwa namna anavyotaka na kuleta maafa makubwa kwa jamii.

Kimsingi, mwishoni mwa kila ubeti mshairi anatoa taswira ya kufanya jitihada katika kutafuta ufumbuzi wa kupambana na ugonjwa wa UKIMWI pale anapoitaka jamii kufumbua fumbo “mgeni huyu ni nani.” Taswira hii inakwenda mbali zaidi kwa kuwataka wanajamii wote na sio serikali peke yake kukaa chini na kuanza kutafakari juu ya mbinu ambazo watazitumia kupambana na ugonjwa hatari wa UKIMWI. Mshairi anafahamu kwamba, mapambano dhidi ya UKIMWI ni jukumu la wananchi wote na si mtu mmoja. Bila shaka ufumbuzi wa fumbo la mgeni huyu ni kitendawili ambacho mtegaji anahitaji kupewa mji kwanza ndio akitegue. Hata hivyo, kwa ushirikiano wa wanajamii wote kwa pamoja basi jibu la kitendawili limeweza kupatikana; mgeni huyo ni UKIMWI. Baada ya kutambulika UKIMWI umekuwa si tatizo kubwa kwa jamii ikilinganishwa na kabla ya kufahamika kwake. Hii inatokana na ukweli kwamba, katika miaka ya hivi karibuni kumegundulika mbinu za kujikinga na UKIMWI na wale ambao wameathirika hupatiwa dawa kwa ajili ya kurefusha maisha yao. Pia, elimu kuhusu UKIMWI imetolewa na inaendelea kutolewa kwa kasi

kubwa kwa wanajamii wote kupitia mbinu na njia mbalimbali kama vile, kufundishwa mashuleni, vyuoni, kupitia vyombo vya habari, matamasha, semina maofisini na katika mabonanza yanayofanyika katika jamii. Hata hivyo, pamoja na jitihada hizi zilizokwishafanyika na kuendelea kufanyika, bado jitihada zaidi zinatakiwa zifanywe na wadau wanaohusika kwa nia ya kuhakikisha kwamba, ugonjwa huu unatokomezwa katika jamii ya Watanzania. Tulipofanya usaili na afisa mmoja wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kuhusiana na suala hili alitueleza kwamba:

> Tume ya Taifa ya Kupambana na UKIMWI imetekeleza miradi mbalimbali ya kupambana na UKIMWI katika sehemu nyingi hapa nchini na kupata mafanikio makubwa katika suala hili. Miradi hiyo imekuwa ikihusu utolewaji wa elimu juu ya UKIMWI hususani namna ya kujikinga nao, namna bora ya kuishi na ugonjwa huo na namna ya kuwahudumia waathirika wa ugonjwa huu hatari. Miradi hii ambayo bado inaendelea kutekelezwa na tume inagharamiwa na serikali pamoja na wahisani wa maendeleo. Pamoja na hayo, tunakiri kwamba, magazeti ya kila siku na yale ya wiki katika nchi yetu yametoa mchango mkubwa katika harakati za kupambana na ugonjwa huu. Ninasema hivi kwa sababu magazeti hayo yamekuwa yakichapa mashairi ya washairi kutoka kila kona ya nchi, kwa nia ya kuhamasisha jamii kuufahamu na kuutokomeza ugonjwa wa UKIMWI.

Maelezo haya yanaonesha kwamba, kwa sasa UKIMWI si tishio kubwa kwa wananchi wa Tanzania kutokana na utekelezaji wa miradi ya utolewaji wa elimu inayohusu UKIMWI iliyofanywa na inayoendelea kutekelezwa na Tume ya Taifa ya UKIMWI. Pia, afisa wa tume hiyo anathibitisha kwamba, bado kunahitajika jitihada zaidi katika kupambana na UKIMWI. Wananchi pamoja na serikali yao wasifikiri kwamba, mapambano yamekwisha. Bado mapambano yapo na yataendelea kuwepo kila siku katika maisha ya jamii ya Watanzania na kwingineko duniani. Mwishoni mwa maelezo ya msailiwa hapo juu, anatoa shukurani zake za dhati kwa magazeti na

bila shaka, washairi ambao hutoa mashairi yao kwa nia ya kuhamasisha jamii katika kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya UKIMWI na kutoa rai kwamba, mapambano hayo yaendelee.

Kwa hakika washairi wa magazetini wanatunga mashairi ambayo kwayo hutujengea taswira mbalimbali. Kwa mfano katika shairi la "UKIMWI Shida Hatari" la John Coster Mpunga anatoa taswira kuwa, UKIMWI umeleta shida kwa jamii kwa kuinyima starehe inayostahiki katika maisha yao. Anasema:

Chanzo sio Afrika, bara letu la heshima
Nchi za Ulaya peka, walikoanza kukwama
Ndipo walipanganika, ili raha kutunyima
UKIMWI shida hatari, huua mamilioni

Wazungu walitamka, Afrika ya Wanyama
Jaa la kutupa taka, lenye wingi wa vilema
Mabinti wakawasaka, nia wapate kukwama
UKIMWI shida hatari, huua mamilioni
**(UHURU, Januari 5, 1990, John Coster Mpunga)**

Katika shairi hili tunapatiwa taswira kwamba, UKIMWI ni ugonjwa ambao umetengenezwa na mwanadamu ambaye ni Mzungu kwa nia ya kuwakosesha raha na starehe watu wa jamii ya Afrika. Raha inasemwa hapa ni ile ya kujamiiana ambayo kwayo ndio njia kuu ya maambukizo ya UKIMWI. Mshairi anatupatia taswira kuwa, Wazungu waliona kwamba, Mwafrika hastahili kupata starehe ya kujamiiana na hivyo kwa kufanya UKIMWI kuambukizwa kwa njia ya kujamiiana basi Mwafrika hatoipata starehe hiyo. Hili linathibitishwa na maelezo ya mshairi kwamba, Mzungu anawatazama Waafrika kama wanyama na kwamba, kujamiiana isiwe ni sehemu ya starehe baina yao bali iwe ni shubiri.

Taswira nyingine inayopatikana katika shairi hili ni kuwa, asili ya UKIMWI ni Ulaya na si Afrika. Mshairi anasema kwamba, ni Mzungu aliyeamua kukaa chini na kuunda ugonjwa wa UKIMWI na kuusambaza kwa Waafrika. Mawazo haya yanaelezwa pia na Mutembei (2009), anapofafanua visasili vilivyobuniwa na wanajamii kufuatana na kuanza kwa ugonjwa wa UKIMWI. Hata hivyo, kwa maoni yetu hatuoni mantiki kuwa, ugonjwa huu ulianzishwa na Mzungu eti kwa nia ya kuwakosesha Waafrika starehe hali ya kuwa hata Wazungu nao huambukizwa maradhi haya. Kimsingi, ipo mitazamo mbalimbali ambayo inaelza juu ya asili na chanzo cha UKIMWI. Kwa mfano, tulipofanya Usaili na Sengo Profesa wa fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kuhusiana na suala hili alitueleza kwamba:

> Kwa maoni yangu, UKIMWI ni adhabu kutoka kwa Muumba dhidi ya wale wote ambao hawazingatii mafundisho ya dini zao kuhusiana na makatazo ya Zinaa na Uasherati. Katika kizazi hiki ambacho UKIMWI umeenea, wamefanya zinaa na uasherati kuwa ni mambo ya kawaida na halali kufanywa na kila mtu tena wengine hufanya hadharani bila ya aibu yoyote. Ukitaka kufahamu kwamba hii ni adhabu kutoka kwa Muumba, we tazama njia kuu ya kuzuia maambukizi ya ugonjwa huu ni ipi? Bila shaka majibu yake yatakuonesha kwamba, ni Kuacha kufanya uzinzi na uasherati, halafu baadaye ndio zinafuatia njia nyingine kama kutumia kondomu, ambayo mimi ninaiona kuwa sio njia sahihi ya kuzuia UKIMWI bali ni ya kusambaza zaidi. Ninasema hivi kwa sababu watumiaji wa hizo kondomu wanatenda dhambi ya kuzini na kwamba, hawadumu katika kutumia zana hizo. Ushahidi wa kiutafiti unaonesha kwamba, wazinifu wanaotumia kondomu hufanya hivyo kwa muda mfupi tu wa mahusiano yao na wanapozoeana huacha kutumia kondomu. Anaye wafanya wasahau kutumia hiyo inayoitwa kondomu ni yule yule Muumba ambaye wao walimdharau na kujikita katika dhambi aliyoikataza.

Mawazo ya Sengo kuhusiana na taswira inayoeleza kwamba, UKIMWI ulianzishwa na Mzungu yana mashiko ambayo yanaweza kuaminiwa kidini na hata kijamii. Sengo ni muumini wa dini ya Kiislamu, lakini mawazo haya yanaaminiwa na

waumini wa dini mbalimbali duniani zisizokuwa Uislamu. Hata hivyo, tunakiri kwamba si madhumuni yetu kujadili kwa kina juu ya asili ya UKIMWI katika bara la Afrika na duniani kwa jumla, bali nia yetu kuu ilikuwa ni kufafanua taswira juu ya suala hili ambayo inajengwa kupitia shairi tulilolidondoa hapo juu. Hata hivyo, bado nafasi ya mjadala zaidi kuhusiana na suala hili unaweza kufanywa na watafiti wengine katika ngazi za elimu ya juu.

Katika sehemu hii tumetoa maelezo ya kina kuhusu taswira zinazojengwa na washairi wa mashairi ya magazetini kuhusiana na UKIMWI. Kwa nukta hii, yafaa kueleza kwamba, taswira zilizoelezwa zinakidhi madhumuni ya utafit wetu na ni vema sasa tutazame kipengele kingine ambacho ni sitiari kama kinavyojitokeza katika mashairi ya magazetini hasa yale yanayohusu UKIMWI.

### 4.2.2 Sitiari

Sitiari ni semi inayolinganisha vitu ama watu lakini bila ya kutumia viunganishi linganishi kama mithili ya, mfano wa, sawa na, kama na kadhalika. Tamathali hii hulinganisha vitu na watu wengine kama kwamba vitu na watu hao ni sawa kabisa (Senkoro 1982, Msokile 1992, na Wamitila 2003). Sitiari ni tamathali ya semi inayohusisha matendo, kitu au tabia ya vitu vyenye maumbile tofauti. Ulingaishio huo unazingatia misingi au sifa zinazopatikana katika vitu vyote viwili, lakini sifa hizo haziwi wazi kati ya kitu na kitu, kwa mfano □ maisha ni moshi□ katika sitiari hii maisha yamelinganishwa na moshi. Moshi ni kitu kinachodumu kwa muda mfupi sana toka pale unapojitokeza. Kwa hiyo, □ mtu’ ambaye amefichwa katika neno □ maisha□ anaishi kwa muda mfupi sana kama vile maisha ya moshi yalivyo. Mashairi ya magazetini hutumia sitiari za aina mbalimbali kwa nia ya kuvyaza

dhamira na kuziwasilisha kwa jamii iliyokusudiwa kwa namna iliyokusudiwa. Shairi liitwalo "UKIMWI tishio", linatupatia sitiari ambayo inajenga dhamira mbalimbali kwa yule anayesoma au kusikiliza shairi hilo. Hebu tutazame dondoo lifuatalo:

Limetupata ni pigo, janga hili la UKIMWI
Limechukua uzito, usiokuwa kifani
Wakubwa pia wadogo, kina mama ni huzuni
UKIMWI sasa tishio, la maisha duniani

Mapenzi hatari kwako, utaupata UKIMWI
Kumbuka Mzee kifo, wapenzi wakishazidi
Kulawiti nacho kifo, utavipata viini
UKIMWI sasa tishio, la maisha duniani

Ukishafahamu hayo, wajibika maishani
Uamuzi fanya leo, kunyoa au kusuka
Bado UKIMWI ni moto, ndugu zangu tambueni
UKIMWI sasa tishio, la maisha duniani
**(UHURU, Januari 27, 1993, Baraka Manyama)**

Katika beti mbili za mwanzo za shairi hili, mshairi ameanza kueleza mambo ambayo yanaweza kusababisa maambukizi ya UKIMWI kwa mwanadamu. Mambo hayo ni kama vile mtu kuwa na wapenzi wengi pamoja na kulawiti. Vile vile, anaeleza kwamba, UKIMWI unaweza kumpata mtu wa umri na rika lolote. Baada ya kuyasema haya kisha ndipo anatoa sitiari kwamba, "Bado UKIMWI ni moto, ndugu zangu tambueni." Sitiari hii inaufananisha UKIMWI sawasawa na moto. Bila shaka, moto pamoja na sifa zake unafahamika vizuri katika jamii. Moto una sifa ya kuteketeza kila kitu, hata vitu vigumu kama chuma na mawe huunguzwa kwa moto na kuyeyuka mpaka kuwa majivu kabisa. Hivyo basi, UKIMWI kufananishwa na moto tunapata uelewa kwamba, yeyote atakayepata UKIMWI atakuwa kana kwamba yupo katika tanuri tayari kwa ajili ya kuunguzwa na moto. Hili linaonekana pale ambapo tunamuona muathirika wa UKIMWI akishambuliwa na maradhi ya aina kwa

aina na kisha kukosa kabisa nguvu na mwili wake kuwa mithili ya mifupa mitupu isiyotamanika kutazamwa na wanadamu wenzake. Jambo hili huleta simanzi kubwa kwa watu wote wanaompenda aliyeambukizwa UKIMWI. Katika usaili tuliofanya na bwana Said Mlamali msomaji wa mashairi ya magazetini wa Magomeni Dar es Salaam, alitueleza kwamba:

> UKIMWI kufananishwa na moto mimi ninakubali kabisa kwa sababu ugonjwa huu si mchezo. Mtu ambaye amewahi kuuguza au kuwa na mgonjwa wa UKIMWI atakubaliana na mimi, kwamba UKIMWI ni moto kwa namna unavyomtafuna mgonjwa na kumuacha mifupa mitupu huku mwili mzima ukiwa umetapakaa vidonda. Ndugu yangu sikiliza, amini usiamini, UKIMWI ni ugonjwa hatari usiokuwa na huruma kwa mtu yeyote. Wewe tazama tu hata wale ambao wanatumia dawa za kuongeza siku za kuishi, hufika mahali dawa hizo zinashindwa kufanya kazi kutokana na makali ya moto wa UKIMWI na hatimaye wanapoteza maisha. Jambo la msingi ni kuieleza jamii ukweli huu kwamba UKIMWI ni moto na kwamba wachukue hatua stahiki kujikinga nao vinginevyo utawateketeza wote.

Mawazo haya ya bwana Said Mlamali yanashadidia sitiari, “UKIMWI ni moto” kwa namna stahiki kabisa. Kwa maoni yetu, tunakubaliana na mawazo haya kutokana na ukweli kwamba, ugonjwa huu ulipoingia ulikuwa ni hatari na tishio kwa maisha ya wanadamu kwa kiasi kikubwa sana na kusababisha vifo vya wanajamii wengi wasio idadi kamili. Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni, ugonjwa huu unaonekana kuwa sio tishio sana kwa maisha ya wanadamu na baadhi ya watu wakiutazama ugonjwa huu sawa na magonjwa mengine. Kwa mfano, ripoti ya afya ya Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa ya mwaka 2009 inaonesha kwamba, ugonjwa wa Malaria ndio unaongoza kwa kusababisha vifo vya watu wengi katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara Tanzania ikiwemo. Kwa hali hiyo UKIMWI sio ugonjwa unaoongoza kwa kuua watu wengi. Pamoja na maelezo haya, bado tunakiri kwamba, UKIMWI ni ugonjwa hatari na unapofananishwa na moto ni sahihi kabisa.

Vile vile, mshairi anatumia sitiari hii kwa nia ya kujenga dhana ya hofu na uoga kwa wananchi dhidi ya ugonjwa hatari wa UKIMWI. Hofu na woga vinajengwa kutokana na matumizi ya sitiari "UKIMWI ni moto." Kutokana na matumizi ya sitiari hii, baadhi ya wanajamii wanapokutana nayo huweza kuwa chachu ya wao kubadili tabia na mienendo yao kuhusiana na masuala ya ngono na hivyo kujihadhari kwa njia muafaka zilizopendekezwa na wataalamu wa afya na mafundisho ya dini. Kwa mantiki hii, vita na mapambano dhidi ya UKIMWI inafanikiwa na ndio maana katika kipindi hiki ugonjwa huu hautazamwi kuwa ni tishio la maisha ya mwanadamu kama ilivyokuwa katika miaka ya mwanzoni ya kuingia kwake katika jamii ya Watanzania na ulimwenguni kwa ujumla.

Kwa hakika, matumizi ya sitiari kuhusu ugonjwa wa UKIMWI yanajitokeza katika mashairi mengi ya magazetini. Shairi la "Nimejikwaa Kisiki", lililoandikwa na Mziwanda linaeleza hivi:

Nimejikwaa Kisiki, dole gumba mguuni
Kidole hakigusiki, uchungu hadi moyoni
Madhila hayasemeki, la kufanya silioni
Nitumie tiba gani, niipate afueni
**(UHURU, Novemba 21, 1990. M.M.S Mziwanda)**

Katika ubeti huu tunapatiwa sitiari ya UKIMWI kufananishwa na "Kisiki." Kisiki ni baki la mti uliokatwa na kubakizwa sehemu yake ikichomoza ardhini na yeyote atakayejikwaa katika kisiki hicho hupata uchungu mkali. Kwa mujibu wa ufahamu wetu, tunaiona sitiari hii kama inarejelea uchungu anaoupata mtu pale tu anapopata kufahamu, kwamba yeye ameathirika na ugonjwa huu hatari. Watu wengi ambao hawategemei kupewa majibu kuwa wameathirika, wanapopewa majibu kama hayo basi hupata mshituko pamoja na maumivu makali katika mioyo yao na baadhi yao

huwa hawawezi kuishi muda mrefu na hatimaye hufariki. Wengine hupata maumivu makali mioyoni mwao baada ya kupewa habari hizo za kuambukizwa UKIMWI na hata kuwaambukiza wengine kwa makusudi lakini baada ya kupata ushauri nasaha hupata matumaini ya kuendelea kuishi maisha marefu. Kwa mantiki hiyo, ni sawa na kusema kwamba, maumivu ya kujikwaa katika kisiki humpata mtu kwa muda mfupi na baadaye maumivu hayo huisha.

Mutembei (2009) alipotumia sitiari hii katika kazi yake alieleza kwamba, sitiari hii imetumika kwa nia ya kupunguza makali ya namna UKIMWI ulivyokuwa ukitazamwa hapo awali na ilivyo hivi sasa. Vilevile, anaongeza kwamba, sitiari hii ilitumika kuonesha kuwa, kuupata ugonjwa wa UKIMWI ni jambo la bahati mbaya na si la kukusudia. Kujikwaa katika kisiki ni jambo la bahati mbaya lisilodhamiriwa na mtu yeyote kwa sababu lina madhara kwa mwili wake. Kimsingi, tunakubaliana na mawazo haya kwa kiasi fulani, hasa tukirejelea pale tu UKIMWI ulipoingia katika nchi yetu. Watu wengi hasa wa mkoa wa Kagera waliupata ugonjwa huu kwa bahati mbaya kwa sababu walikuwa hawaujui. Hata hivyo, katika kipindi tulichonacho hivi sasa suala la kupata UKIMWI kwa bahati mbaya si la kiwango kikubwa kwa sababu jamii ina uelewa mkubwa kuhusiana na ugonjwa huu. Hivyo basi, tunaweza kueleza kwamba, sitiari hii inatoa ulewa mkubwa kuhusiana na ugonjwa wa UKIMWI ingawa ina mapungufu. Miongoni mwa mapungufu yake ni kwamba, kisiki kinaweza kung’olewa na kuondolewa mara moja pale itakapohitajika kufanywa hivyo, huku UKIMWI ukiwa bado haujapata tiba na kinga madhubuti ya kuutibu na kuuzuia.

Washairi wa magazetini hawakuishia hapo katika kuandika mashairi yenye kuelezea masuala yanayohusiana na ugonjwa wa UKIMWI kwa kutumia sitiari za aina mbalimbali. Kwa mfano, katika shairi lifuatalo tunaelezwa kwamba:

Tamatini nipo kibo, UKIMWI tuepukeni
Tusiamini vizibo, vya kuvalia mwilini
Tulitunze letu pambo, hadhi yetu kuthamini
Anayepata UKIMWI, duniani ni buriani
**(UHURU, Oktoba 23, 1990. Isaya Kibona).**

Katika shairi hili msanii anatumia sitiari "vizibo" kurejelea mipira ya kutumia wakati wa kujamiiana inayojulikana kwa jina la Kondomu. Wataalamu wa masuala ya afya wanaeleza kwamba, matumizi sahihi ya mipira hiyo husaidia kuzuia maambukizi ya magonjwa ya zinaa, UKIMWI nao ukiwepo. Kizibo kwa uelewa wetu wa kawaida, ni kitu ambacho hutumika kwa ajili ya kuzuidhia chombo cha kuhifa kinywaji au aina yoyote ile ya kitu au bidhaa isimwagike. Kwa mfano, kinywaji baridi aina ya soda hufunikwa kwa kutumia kizibo ili isiharibike au kuingiwa na wadudu aina ya bakteria ambao ni hatari kwa afya ya mwanadamu pindi atakapotumia kinywaji hicho. Hata hivyo, yapo mazingira ambayo kizibo cha soda kinaweza kufunguka na kupitisha hewa taratibu na mpaka soda hiyo inapomfikia mlaji inakuwa tayari imekwisha haribika. Bila shaka ndio maana mtunzi wa shairi hili anatueleza kwamba, "tusiamini vizibo, vya kuvalia mwilini" akiwa na maana kwamba, kondomu sio kinga thabiti ya UKIMWI. Tulipata fursa ya kufanya usaili na Adrian Michael msomaji wa mashairi ya magazetini katika maeneo ya Feri jijini Dar es Salaam kuhusiana na suala la kondomu kuwa ni kinga thabiti ya UKIMWI au la, naye akatueleza kama ifuatavyo:

> Mimi ninavyofahamu, kondomu ni kinga thabiti ya UKIMWI hasa ikitumiwa kwa usahihi na mhusika. Ninachofahamu pia ni kwamba, kufanya zinaa ndio dhambi lakini kutumia kondomu sio dhambi. Hapa ndipo ninapotafautiana na viongozi wangu wa dini, ambao wanaeleza kwamba, kutumia kondomu ni dhambi. Ninarudia tena, kuzini ndio dhambi lakini sio kutumia kondomu. Mimi ninatokea katika eneo la Makete ambayo ndiyo wilaya inayoongoza kwa maambukizi ya UKIMWI Tanzania ambapo karibu kila kaya imeshapoteza mtu au watu na kuacha yatima wasiokuwa na idadi.

> Lakini matumizi ya kondomu yamesaidia sana kupunguza kasi ya ueneaji wa UKIMWI katika wilaya ya Makete. Kama sio matumizi ya kondomu tungekuwa sote tumekwisha na nchi hii ingebaki kuwa hame. Hivyo, tusidanganyane kwamba, kondomu sio kinga ya UKIMWI bali ni kinga tena mathubuti kabisa isiyo na shaka ndani yake.

Mawao haya yanaonekana kupingana na yale ya mshairi aliyoyatoa hapo juu ambayo yanaonesha kwamba, wananchi wanatakiwa wasiamini matumizi ya kondomu kwa sababu si kinga imara na thabiti ya kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Kwa maoni yetu, tunaona kwamba, kinga sahihi ya ugojwa wa UKIMWI ni kuacha uzinzi na uasherati na kuheshimu na kutekeleza mafundisho ya dini katika maisha ya kila siku ya jamii.

Kimsingi, tumetoa maelezo ya kina kuhusu na sitiari katika mashairi ya magazetini kiasi cha kutosheleza madhumuni yetu ya kufanya utafiti huu. Kwa hali hiyo, tunaona ni vema sasa tutafiti kipengele kingine cha tamathali za usemi ambacho ni takriri. Maelezo na ufafanuzi kuhusiana na takriri yanatolewa hapa chini kama ifuatavyo:

### 4.2.3 Takriri

Takriri ni tamathali ya usemi inayoonesha kitendo cha mtunzi kurudiarudia maneno, sauti, wazo au vifungu fulani katika kazi yake. Kutokana na aina tofauti za urudiaji tunaweza kuwa na aina za takriri kama vile, takriri wazo, takriri neno, takriri mistari, takriri irabu, takriri konsonanti n.k. Watunzi hutumia takriri ili kutia uzito maneno yanayorudiwarudiwa na kuweka msisitizo ili msomaji aweze kupata ujumbe uliokusudiwa na mtunzi (Ntarangwi 2004, Wamitila 2003). Wamitila (2008)

anaeleza kwamba, uhusiano uliopo baina ya sauti na ushairi ni mkubwa sana. Sauti zinazotumika katika utungo wa kishairi zina mchango mkubwa katika kuendeleza dhamira ya utungo huo. Je, kuna uhusiano gani kati ya athari inayotokana na maneno fulani na sauti za maneno hayo? Je, sauti hizo za maneno zinahusiana vipi na maana za maneno yenyewe? Wamitila (ameshatajwa) anaendelea kueleza kwamba matumizi ya takriri ndio hasa yawasilishayo mbinu ya matumizi ya kisauti katika ushairi na kazi nyingine za kifasihi.

Mashairi ya magazetini yanatumia takriri kwa kiasi kikubwa kwa kuwa mengi kati yake yanafuata mtindo wa kimapokeo wa kutunga mashairi. Kama ilivyoelezwa hapo awali, matumizi ya takriri katika ushairi na kazi nyingine za fasihi hufanywa kwa ajili ya kutoa msisitizo juu ya jambo ambalo mshairi anataka jamii ilielewe vizuri. Ili msomaji au msikilizaji aelewe shairi hilo vizuri ni lazima akutane na takriri fulani kila mara anaposoma beti au aya katika kazi za riwaya, tamthilia na hadithi. Katika shairi la "UKIMWI Hauna Dawa", kuna matumizi ya takriri silabi kama ifuatavyo:

Sindano za sirisiri, mitaani zakemewa
Si njema zina dosari, ni tiba za kulipua
Hazichemshwi vizuri, kama inavyotakiwa
UKIMWI hauna dawa, kinga ni kujihadhari

Kina mama na vigori, ndugu zangu kina HAWA
Kutoga tusikithiri, masikioni na puwa
Vinapunguza umuri, vitu tunavyotogea
UKIMWI hauna dawa, kinga ni kujihadhari
**(MZALENDO, Oktoba 29, 1989. Salama Yusuph)**

Katika beti hizi mbili za shairi tunaona mshairi akitupatia shairi lenye vina kati na mwisho, ambalo bila shaka yoyote ni shairi la kimapokeo. Vina kati katika shairi hili ni silabi "ri" na vina mwisho ni silabi "wa na a" katika baadhi ya mishororo. Katika kituo cha shairi vina kati ni silabi "wa" na vina mwisho ni silabi "ri". Matumizi ya

takriri vina katika beti hizi mbili za shairi yanatoa msisitizo kwa msomaji kupata uzito, kwamba UKIMWI ni ugonjwa hatari na hivyo kila mtu anapaswa kujikinga na kujihadhari nao kama inavyotakiwa. Silabi "ri" ni silabi yenye kuashiria hatari hivyo msomaji anapokutana nayo mara kwa mara katika usomaji wake wa shairi husika, basi anapata ile dhana halisi ambayo mtunzi ameikusudia. Yaonekana kwamba, mtunzi anataka msomaji wake ajenge hali ya kuuogopa UKIMWI katika maisha yake, ndio maana anairudia silabi "ri" katika mshororo wa mwisho wa kila ubeti wa shairi husika. Tulipofanya usaili na Mohamed Omari wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kuhusiana na matumizi ya takriri katika mashairi kwa ujumla, alikuwa na haya ya kusema:

> Mwaka 2009 nilipokuwa ninahudhuria mihadhara ya shahada ya Uzamili, katika Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam nilipata kumsikia profesa Euphrase Kezilahabi akisema kwamba, ukitaka kulielewa zaidi shairi basi tazama matumizi ya sauti yalivyo katika beti za shairi husika. Matumizi ya sauti hasa takriri katika mashairi yanasaidia sana kujenga dhamira mbalimbali katika shairi. Zipo sauti zitumiwazo kwa makusudi ya kuashiria mapenzi, huzuni, simanzi, hatari, hofu, ukali, chuki, njaa, mashaka, upendo na kadhalika. Hivyo basi, kwa kulielewa hili hakuna hata mtu mmoja ambaye atasoma shairi fulani akatoka kapa bila ya kuelewa ni dhamira gani zinazozungumzwa katika shairi husika na kisha kulalama kwamba, ushairi ni mgumu na kwamba haueleweki kirahisi. Mshairi anapoteua sauti fulani na kuirudiarudia katika beti zake za shairi hufanya hivyo kwa makusudi ya kumtaka msomaji kutafakari jambo kwa kina na kisha kupata dhamira zinazojitokeza katika shairi husika.

Tunakubaliana na mawazo ya Mohamed Omari aliyoyatoa hapo juu kuhusiana na matumizi ya takriri katika ushairi na fasihi kwa jumla. Kwa bahati mbaya sana, watu wengi huchukulia matumizi ya takriri katika ushairi kama sehemu ya kupendezesha shairi, yaani pambo la shairi na si sehemu ya kusaidia wasomaji kupata dhamira katika shairi husika. Kwa mfano, katika miaka ya 1970 kulitokea mgogoro wa

ushairi wa Kiswahili ambapo jambo kuu lililoleta mabishano kati ya wanamapokeo na wanausasa lilikuwa ni matumizi ya vina na mizani (Njogu na Chimerah, 1999: Mayoka, 1984; Mulokozi na Kahigi, 1979). Wanamapokeo walidai kwamba, vina na mizani ni uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili, huku wanausasa wakidai kwamba, shairi la Kiswahili halitambuliki kwa vina na mizani kwa kuwa hizo ni sifa za jumla za ushairi duniani kote. Mambo yanayoutofautisha ushairi wa Kiswahili na aina nyingine za ushairi duniani ni lugha yake, utamaduni wake na masuala ya kijamii na kisiasa unayoyaeleza (Kezilahabi, 1983).

Kimsingi, maelezo haya yanaonesha kwamba, ushairi wa Kiswahili unayo sifa ya kutumia vina na mizani kama mashairi ya sehemu nyingine yoyote ile duniani inavyofanya. Jambo lisilokubalika ni kudai kwamba, kama shairi halina vina na mizani basi haliwezi kuwa shairi la Kiswahili. Kwa kutumia vina na mizani shairi la Kiswahili linakuwa na matumizi makubwa ya takriri ambayo huifanya hadhira kutafakari na kulifuatilia jambo lisemwalo na mwandishi kwa karibu na hatimaye akaweza kujenga dhamira mbalimbali kutoka katika shairi. Kezilahabi (1983) anaonya kwamba, wale wanaotunga mashairi kwa kutumia takriri silabi mwishoni mwa mishororo ya beti za mashairi yao kwa kulazimisha, huyafanya mashairi husika kutovutia na kushindwa kuibua dhamira mbalimbali kama ilivyotegemewa na wasomaji wa mashairi. Hivyo, mtunzi anayetaka shairi lake liwe na takriri zenye kuleta tija kwa wasomaji wake, ni lazima atunge shairi hilo kwa kuteua takriri husika kwa makini ili aweze kuleta athari kwa msomaji.

Kwa hakika mashairi ya magazetini hayaishii katika kutumia takriri silabi peke yake, yanakwenda mbali zaidi na kutumia takriri neno. Takriri neno ni marudiorudio ya

neno katika msitari wa shairi, ubeti au katika beti zote za shairi. Katika shairi la "Tujihadhari na UKIMWI", tunapata matumizi ya takriri neno:

Sitaki kuna UKIMWI, gonjwa limesambatika
Sitaki wenda siumwi, akinijali Rabika
Sitaki nisiwe zimwi, kwa kushindwa kutibika
Muache akina kaka, chamoto kunisakama
**(UHURU, Januari 7, 1991. Magreti Clemens).**

Katika ubeti huu wa shairi kuna matumizi ya takriri neno "sitaki" ambalo limejirudia mara tatu. Matumizi ya takriri hii yanatoa msisitizo kuwa, UKIMWI ni ugonjwa hatari ambao haupaswi kupewa nafasi ya kuingia katika mwili wa mwanadamu kwa namna yoyote ile. Neno hili linawataka wanajamii wote kuuchukia ugonjwa wa UKIMWI na kuhakikisha mapambano dhidi yake hayakomi mpaka ugonjwa huo utokomee na kumalizika kabisa. Vile vile, matumizi ya neno hili yanatoa msisitizo kwa kila mwanajamii kujifunza na kufahamu njia za kupambana na kukabiliana na UKIMWI pasipo kusubiri kufundishwa na serikali au mashirika yasiyokuwa ya serikali. Hii inaonesha, jukumu la kujikinga na kupambana na UKIMWI ni la kila mwanajamii na kwamba wao ndio wadau muhimu katika kuhakikisha kuwa, ugonjwa huu unakuwa sio tishio la maisha kwa wanadamu. Hili litawezekana kama kila mwanajamii atasema "sitaki" kuupata UKIMWI na hivyo akachukua tahadhari ya kutosha.

Vile vile, katika mashairi ya magazetini kuna matumizi ya takriri sentensi, ambapo sentensi nzima hurudiwarudiwa katika beti za shairi. Mara nyingi, takriri sentensi hujitokeza kama kituo cha shairi. Matumizi ya takriri sentensi yanapatikana katika shairi la "Kupambana na UKIMWI ni Kupambana na Mungu". Zifuatazo ni baadhi ya beti za shairi hili:

Ni adhabu yake Mungu, UKIMWI ulimwenguni
Dhambi sasa ni ukungu, watanda ulimwenguni
Wamekwisha lewa kungu, Mungu hatambulikani
Kupambana na UKIMWI, ni kupambana na Mungu

Kamwe hamtamshinda, Muumba wetu Mbinguni
Mmeshampanda punda, mwendo wake taabani
Hamtapata matunda, Mungu ameshasaini
Kupambana na UKIMWI, ni kupambana na Mungu

Mtasagwa mpaka basi, UKIMWI binti shetani
Janga hilo la mkosi, tiba yake kaburini
Tumgeuze nyusi, mtubu kwa Rahamani
Kupambana na UKIMWI, ni kupambana na Mungu
**(NIPASHE, Juni 5, 2001. Mwl. R. Khalfan).**

Katika beti tatu za shairi hapo juu tunaona takriri sentensi ikijitokeza katika kila ubeti na kusomeka “Kupambana na UKIMWI, ni kupambana na Mungu”. Matumizi ya takriri hii yanamfanya msomaji kupata tafakuri kila mara anapomaliza kusoma ubeti mmoja wa shairi kwa kina na hivyo kuelewa jambo linalokusudiwa na mtunzi wa shairi. Si hivyo tu, bali pia, hata msomaji anaweza kupata maana nyingine tafauti na ile iliyokusudiwa na mtunzi wa shairi analolisoma. Tunasema kwamba, msomaji anavuta tafakuri ya kina kwa sababu ni sentensi ile ile ndiyo anakutana nayo kila mara anapomaliza kusoma ubeti mmoja wa shairi kwenda mwingine. Msomaji makini atajiuliza maswali, kama vile, hivi ni kwa nini mshairi anarudiarudia sentensi fulani kila mara mwishoni mwa beti zake za shairi. Kutokana na kujiuliza swali kama hilo ndipo anapopata dhamira kutoka katika shairi hilo.

Baada ya kutoa maelezo ya kina juu ya takriri katika mashairi ya magazetini, tunaona ni vema sasa tugeukie kipengele kingine cha tamathali za usemi kinachojitokeza katika mashairi hayo. Kipengele hicho si kingine bali ni tafsida.

### 4.2.4 Tafsida

Tafsida ni tamathali ya usemi ambayo hutumiwa katika kazi za ushairi yakiwemo mashairi ya magazetini kwa nia ya kuficha ukali wa maneno hasa yale ambayo hayapaswi kutamkwa hadharani (Wamitila, 2008). Utamaduni wa Mwafrika na Mtanzania kwa jumla, umeweka tafsida katika kufanya mazungumzo fulani yenye dhamira za aibu kutotamkwa hadharani, kwa misingi ya kuheshimu, kujenga na kukuza maadili katika jamii. Miongoni mwa mambo ambayo yanahusishwa na matumizi ya tafsida ni yale yanahusu viungo vya siri vya mwanadamu pamoja na kazi inayofanywa na viungo hivyo. Viungo hivyo, pamoja na mambo yanayohusika navyo, hutafutiwa lugha ya kuvitaja, lugha ambayo ina stara na huweza kutamkwa katika hadhara ya watu (Njogu na Chimerah, 1999).

Mashairi ya magazetini husomwa na hadhira yenye rika tafautitafauti jambo ambalo huwalazimu watunzi wa mashairi, kutunga mashairi yao kwa kutumia lugha ya tafsida. Katika shairi la "UKIMWI", kuna matumizi ya tafsida yanayojibainisha kama ifuatavyo:

> Isigezwe dhamana, mipira ya asherati
> UKIMWI ukitubana, matokeo ni mauti
> Wa masomoni vijana, elimu hawatafuti
> Ustawi wa Jamii, tokomezeni UKIMWI
> **(UHURU, Juni 30, 1992. WA Pachoto, H. Kamuge).**

Katika ubeti huu mshairi anatumia tafsida, "mipira ya asherati" akiwa na maana ya kondomu. Kondomu ni aina ya mpira ambao huvaliwa na mwanamume au mwanamke katika uume au uke wakati wa kujamiiana kwa nia ya kujikinga na magonjwa ya zinaa pamoja na UKIMWI. Katika miaka ya mwanzo ya kugundulika UKIMWI ilikuwa si kazi rahisi kutamka neno "Kondomu" hadharani kutokana na

sababu za kimaadili. Kimsingi, hata mtu alipokwenda dukani kwa nia ya kununua kifaa hiki alipata shida kulitamka "Kondomu." Baadhi ya watu waliahirisha kununua "Kondomu" na kununua kitu kingine afikapo katika duka liuzalo dawa baridi na "Kondomu." Hii hutokea pale mnunuzi anapokuta katika duka la dawa kuna wateja au watu wengine waliojikalia dukani hapo tafauti na muuzaji. Hivyo, msanii anapotumia "mipira" badala ya "Kondomu," anapunguza ukali wa neno husika na neno hili la kitafsida linaweza kutumika katika mazingira tafautitafauti ya hadhara ya watu.

Si hivyo tu, bali pia, katika kuonesha "Kondomu" ni neno kali kwa mujibu wa utamaduni wa Mwafrika na Mtanzania, mshairi mwingine wa shairi liitwalo "UKIMWI", naye anatumia lugha ya tafsida kuelezea "Kondomu." Anasema:

Tamatini nipo kibo, UKIMWI tuepukeni
Tusiamini vizibo, vya kuvalia mwilini
Tulitunze letu pambo, hadhi yetu kuthamini
Anayepata UKIMWI, duniani ni buriani
**(UHURU, Oktoba 23, 1990. Isaya Kibona)**

Katika shairi hili, "Kondomu" inaitwa kwa jina la kizibo. Hii inaonesha, "Kondomu" ni jina ambalo likitamkwa katika hadhara linaleta ukakasi na kumfanya mtamkaji wa neno hilo kuonekana kuwa ni mtu asiyekuwa na maadili ya kijamii. Ni kutokana na ukweli huu ndio maana tunapata maneno ya kitafsida yenye kurejelea "Kondomu." Tulifanya usaili na Bi. Pascalina Kiruay; muuzaji katika duka liuzalo dawa baridi eneo la Mwananyamala Komakoma jijini Dar es Salaam kuhusu matumizi ya tafsida zihusuzo "Kondomu," akatueleza kuwa:

> Ndugu mtafiti ninapenda nikueleze kwamba, tangu nilipoanza kuuza katika duka hili, yapata miaka mitatu sasa na wateja wengi

> wanaokuja kununua “Kondomu” wanapata shida kulitamka neno hili waziwazi na badala yake wanatafuta maneno mengine yenye kupunguza ukali wa neno hilo. Kwa mfano, wengi kati ya wateja wangu hutumia neno “salama” au “kinga” wakirejelea kondomu. Ingawa kuna aina ya “Kondomu” iitwayo “Salama,” lakini neno hili huonekana kuwa na staha zaidi pale linapotumika kurejelea aina nyingine za “Kondomu” kama DUME na nyinginezo. Vile vile, baadhi ya wateja huona aibu wanaponunua kondomu kiasi kwamba ukiwatazama machoni, utaona wanatazama chini au pembeni. Hii inaonesha, kitu wanachokihitaji kitawafanya watazamwe na jamii kuwa wanakwenda kukitumia katika jambo ambalo si jema katika jamii-uzinifu, ingawa wakati mwingine hawatumii kondomu kufanya zinaa bali wanatumia katika ndoa zao. Nionavyo, wanavyotumia maneno yanayoficha ukali wa kondomu basi wanaonekana kuwa ni wastaarabu na pengine, kama kuna wateja wengine waliokuja kununua dawa hawatashangaa kusikia jina la tafsida kurejelea “Kondomu,” likitumiwa na mteja mwenzao.

Mawazo haya yanaonesha kwamba, matumizi ya lugha ya tafsida kwa ajili ya kurejelea vitu ambavyo kwa kawaida si rahisi kutamkwa waziwazi katika jamii ni sehemu muhimu kwa ajili ya kutunza na kudumisha maadili na utamaduni wa jamii. Hata hivyo, baada ya miaka kadhaa kupita, tangu UKIMWI ulipogundulika “Kondomu,” imekuwa si jambo la aibu kutamkwa mbele za watu ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Neno hili limekuwa ni la kawaida mno na hutamkwa kama lilivyo katika vyombo vya habari, katika masomo darasani, katika makongamano na warsha za UKIMWI za kitaifa na kikanda.

Pia, washairi wa magazetini wanatumia lugha ya tafsida kurejelea tendo la kujamiiana ambalo kwa kawaida huwa halitamkwi hadharani kulingana na maadili ya jamii ya Watanzania. Tafsida hii tunaipata katika shairi la “Utaukwaa UKIMWI,” kuwa:

Tafadhali muepuke, japokuwa anang’aa
Ninahisi damu yake, mdudu kesha shupaa
Anangoja siku zake, aende ahera kukaa
Hadhari utaukwaa, ni UKIMWI wanasema

Ngoja nikuambie siri, kubali au kataa
Yule ni mtu hatari, amejawa na tamaa
Yuko ndani ya kaburi, mmoja alomvaa
Hadhari utaukwaa, ni UKIMWI wanasema
**(UHURU, Aprili 16, 1994. Isaa Majid).**

Katika ubeti wa kwanza, mshairi ameanza kueleza juu ya mwanamke ambaye tayari ameshaathirika kwa ugonjwa wa UKIMWI kwa kuutahadharisha umma wa wanaume wasithubutu kumsogelea mwanamke huyo kwani nao wataukwaa UKIMWI. Katika ubeti wa pili msitari wa tatu, anasema: "Yuko ndani ya kaburi, mmoja alomvaa". Msitari huu wa ubeti wa pili hapo juu una matumizi ya lugha ya kitafsida kwa maana kwamba, "mmoja alomvaa" inamaanisha mwanamume aliyemwingilia mwanamke huyo kimwili bia shaka naye ameathirika kwa ugonjwa wa UKIMWI na hatma yake ni kifo. Shairi hili linaweza kusomwa au kusikilizwa na hadhira ya rika lolote pasipo shaka kwa sababu limetumia lugha ya tafsida.

Baada ya kutoa maelezo ya kutosheleza juu ya tafsida, yafaaa sasa tutazame kipengele kingine cha lugha ya kitamathali. Kipengele hicho ni tashibiha ambacho kinawasilishwa kwa ifuatavyo:

### 4.2.5 Tashibiha

Tashibiha ni tamathali ya usemi ambayo hutumiwa kwa minajili ya kulinganisha vitu viwili ambavyo vina sifa tofauti kwa kutumia maneno kama vile, mithili ya, kama, sawa sawa na kadhalika (Njogu na Chimerah, 1999). Tamathali hii hutumika kwa minajili ya kumpatia msomaji au msikilizaji wa kazi ya fasihi hisia muafaka juu ya jambo linaloelezwa na mtunzi. Baada ya kuzipata hisia hizo, anaweza kubainisha dhamira zinazojengwa katika kazi hiyo. Wamitila (2008) anaeleza kwamba,

tamathali hii ya usemi ina sifa ya kuifanya kazi ya fasihi kuwa hai kwa kuwa inafananisha vitu viwili ambavyo havina sifa zinazofana lakini vitu hivyo huonekana kama vinafanana kabisa baada ya kulinganishwa kwa kutumia tashibiha.

Washairi wa magazetini huitumia tamathali hii ya usemi kwa madhumuni mbalimbali lakini kubwa likiwa ni kuwasilisha dhamira kwa jamii iliyokusudiwa na kwa namna iliyokusudiwa. Katika shairi liitwalo "UKIMWI hauna dawa," mshairi amesheheneza matumizi ya tashibiha kama ifuatavyo:

Mzinzi jua maiti, tena ni wa kuugua
Mwisho hatoi sauti, kuwa mwepesi wa buwa
Mwili kuwa kama jiti, motoni wende kutiwa
UKIMWI hauna dawa, dawa kuacha uzinzi
**(MAJIRA, Juni 30, 1995. A. J. Mwinyimkuu).**

Katika ubeti huo wa shairi, Mwinyimkuu anatuambia kwamba, "mwili kuwa kama jiti, motoni wende kutiwa". Hapa kuna matumizi ya tashibiha yenye kuonesha kwamba, mgonjwa wa UKIMWI hukonda kiasi cha mwili wake kuisha kabisa na kuwa kama kijiti. Bila shaka kijiti sote twakifahamu na sifa zake pia tunazitambua. Hivyo, mwili wa binadamu kufananishwa na kijiti bila shaka, inajenga taswira na ishara kuwa, UKIMWI ni ugonjwa hatari sana na kila mmoja katika jamii anapaswa kujihadhari nao. Tashibiha hii inajenga dhana ya hofu kwa wanajamii, kwamba UKIMWI si kitu cha kuchezea hata kidogo kwa kuwa kina madhara makubwa katika maisha ya mwanadamu. Mwanadamu ambaye alikuwa na mwili wenye afya nzuri, yenye kumvutia kila amtazamaye lakini leo afya hiyo imeporomoka na mwili kufanana na kijiti. Hili ni jambo hatari na lenye kumtisha kila alisikiaye na hasa alishuhudiaye kwa macho yake.

Mshairi wa shairi lililopo hapo juu, anaendelea kutumia tashibiha nyingine yenye sifa ya kuporomoka kwa afya ya muathirika wa UKIMWI katika msitari wa pili. Anaposema: "mwisho hatoi sauti, kuwa mwepesi wa buwa." Tashibiha hii inatupatia picha kwamba, muathirika wa UKIMWI hupungua uzito wa mwili wake kwa kiwango kikubwa kiasi cha kukosa nguvu za kuweza kusimama na kutembea kama ilivyokuwa hapo awali kabla ya kuupata ugonjwa huo. Buwa, liwe la mahindi, mtama, ulezi, mpunga, uwele, ngano, alizeti au rangaranga kwa kawaida huwa ni jepesi na halina uzito wa maana. Mwili wa binadamu ambao hufikia kilogramu mia moja na zaidi leo umeporomoka na kuwa na wepesi wa buwa! Jambo hili linahofisha na kutisha sana. Kwa hiyo, jamii inapaswa kujihadhari na maambukizi ya ugonjwa UKIMWI.

Kimsingi, suala la athari za UKIMWI kwa mgonjwa kiasi cha kumfanya muathirika kuishiwa nguvu na mwili wake kuwa dhoofu tena uliokondeana kupita kiasi lilitufanya tuulize watafitiwa wetu kuwa wao wana mtazamo gani kuhusiana na tashibiha hii. Fatuma Ally wa Mtoni kwa Azizi Ally alitueleza kwamba:

> UKIMWI ni ugonjwa wa hatari sana ambao unamtafuna mtu mpaka mwili wake unaisha kabisa. Jambo linalosababisha hali hii ni ile mgonjwa kushambuliwa na magonjwa mengi kwa wakati mmoja. Kwa bahati, nimewahi kumuuguza ndugu yangu ambaye aliugua ugonjwa huu kwa muda mrefu. Mwili wake ulikwisha kiasi akilala kitandani haonekani na badala yake unaona shuka tu. Mtu asiyefahamu kwamba katika kitanda alichokuwa akilala kuna mtu angeweza kumkalia akifikiri ni shuka tu hazijakunjwa au kutandikwa vizuri katika kitanda hicho. Jambo hili lilinihofisha mimi binafsi pamoja na wenzangu wengine waliokuwa karibu na mgonjwa huyo kiasi cha kufikia kuwa makini sana nasi tusije tukaambukizwa UKIMWI. Ninakueleza mtafiti, ugepata fursa ya kumuona mgonjwa huyo usingeamini macho yako, unaweza ukafikiri ni mtoto mdogo aliyezaliwa punde. Jambo ambalo pengine litakufahamisha kuwa ni mtu mzima ni kichwa chake kuwa kikubwa na mifupa yake ya mikono na miguu ni mirefu. Kwa hiyo, kinachoelezwa na washairi

> wa magazetini kuhusiana na kukonda kwa mwili wa mwathirika wa UKIMWI ni jambo la kweli na wala halina ubishi.

Maelezo ya Bi. Fatuma yanashadidia tashibiha ambayo tumeieleza hapo juu kwa kutupatia mfano halisi kabisa ambao yeye binafsi alikumbana nao na kushiriki kwa vitendo. Hata hivyo, ni vema ikaeleweka kwamba, katika kipindi hiki ambapo kumegundulika dawa za kurefusha maisha ya mwathirika wa UKIMWI hali haiko hivyo tena. Waathirika wa UKIMWI ambao wanatumia dawa hizo ni vigumu kuwatambua kuwa ni waathirika, kwa sababu dawa hizo huwapatia nguvu na mwili hunawiri kama ilivyo kwa mtu yeyote ambaye hajaugua ugonjwa wowote ule. Hii haina maana kwamba, katika kipindi hiki huwezi kukumbana na mgonjwa wa UKIMWI ambaye amedhoofika na kuwa na hali mbaya kama ile inayeelezwa katika tashibiha za mashairi ya magazetini. Tunasema hivi kwa sababu, wapo baadhi ya watu ambao hawataki kwenda kupima afya zao ili ijulikane kama wameambukizwa UKIMWI au la, hata kama dalili za wao kuwa na UKIMWI zinaonekana bayana. Watu hawa hudhoofika na kufikia katika hali mbaya ambayo tumeisherehesha hapo juu.

Mshairi mwingine aitwaye kwa jina la Mohamed Mwanambaya anatupatia tashibiha ambayo pia inaeleza hali ya mgonjwa ambaye ameathirika kwa UKIMWI. Katika ubeti wa shairi lake “Kinga kuacha Zinaa”, anaeleza:

> Kifo cha ugonjwa huu, mtu wa kunyanyapaa
> Baadaye mabega juu, wasinzia kama taa
> Hapo hupati nafuu, umbile kama kichaa
> Kinga kuacha zinaa, gonjwa hili la UKIMWI
> **(MAJIRA, Disemba 10, 2001. Mohamed A. Mwanambaya).**

Msahiri huyu anatueleza kwamba, mgonjwa wa UKIMWI anaponyanyapaliwa hujisikia vibaya na kukata tamaa ya kuendelea kuishi tena. Baada ya kunyanyapaliwa anaanza “kusinzia kama taa,” tashibisha yenye kuonesha mwisho wa uhai wa muathirika huyo. Mara nyingi taa ya kibatari, chemli, karabai au hata taa ya umeme inaposinzia mara nyingi huishia kuzimika. Kusinzia huko kunatokana na mambo mengi kama vile kuishiwa mafuta au upepo mkali hasa kwa upande wa taa zisizo za umeme. Kwa zile za umeme huweza kusinzia kutokana na hitilafu au tatizo la kiufundi katika vyanzo au hata katika nyumba ya mtumiaji wa umeme. Maelezo haya yanaonesha kwamba, kusinzia kwa taa husababishwa na mambo kadhaa na haisinzii tu bila sababu ya msingi. Kwa hali hiyo, mgonjwa wa UKIMWI naye husinzia kutokana na Upungufu wa Kinga Mwilini sambamba na kunyanyapaliwa. Tashibiha hii inaonesha kwamba, mgonjwa wa UKIMWI huwa na hali mbaya zaidi baada ya kutengwa na wale ambao aliwategemea kwamba ndio watakao mjali na kumtunza. Jambo hili humsababisha kuathirika kisaikolojia na kumsababishia kufariki dunia mapema. Hata hivyo, suala la unyanyapaa kwa wagonjwa wa UKIMWI si kubwa sana katika kipindi hiki kwa sababu jamii imeshapata elimu ya kutosha kuhusu namna ya kumtunza na kumhudumia mgonjwa wa UKIMWI pasipo kupata maambukizi kutoka kwake. Vile vile, jamii imekwisha elewa kwamba, UKIMWI ni ugonjwa ambao unaweza kumpata mtu yeyote yule na kwa njia mbalimbali zisizokuwa za zinaa na hivyo hakuna haja ya kumnyanyapaa mgonjwa UKIMWI.

Baada ya kutoa maelezo toshelevu juu ya tashibiha ni vema sasa tutazame aina nyingine ya tamathali ya usemi. Tamathali hii si nyingine bali ni ishara. Maelezo ya kina kuhusiana na tamathali hii yanatolewa hapa chini kama ifuatavyo:

### 4.2.6 Ishara

Ishara ni tamathali ya usemi ambayo hutumiwa na watunzi wa kazi za fasihi kufanya uashiriaji ambao hujenga na kuwasilishwa dhamira kwa hadhira iliyokusudiwa na kwa namna ambayo imekusudiwa (Kahigi, 1995). Lugha ambayo husaidia kujenga ishara ni ile iliyoshehenezwa picha na misimbo ambayo kutokana na misimbo hiyo ndipo ishara mbalimbali hupambanuliwa na wasomaji. Omary (2011) anaeleza kwamba, matumizi ya lugha ya ishara yanapatikana kwa kiasi kikubwa katika mashairi ya Kezilahabi ambaye licha ya kutumia misimbo katika kujenga ishara pia hutumia sauti kuashiria dhamira mzomzo kwa wasomaji wake.

Washairi wa magazetini wamekuwa wakitumia lugha ya ishara kwa nia ya kuwasilisha dhamira zinazohusiana na masuala ya UKIMWI kwa jamii. Mfano mzuri ni mshairi Mohamed Limbetembe kupitia shairi lake la "Tujikinge na UKIMWI," anasema:

Kama ukiwa muhuni, hujajaliwa kuoa
Huna vyombo salimini, kondomu ukatumia
Kinyume hapa amini, sanda unajikatia
Tujikinge na UKIMWI, kulinda wetu uhai

Wanawake yafuateni, sharti kinga tumia
Mpenzi uso mwamini, kondomu kuitumia
Magonjwa ya hatari, ya zinaa jikingea
Tujikinge na UKIMWI, kulinda uhai wetu
**(MAJIRA, Machi 27, 1997. Mohamed Limbetembe).**

Katika msitari wa tatu, mshairi anatumia lugha ya ishara pale anaposema, "kinyume hapa amini, sanda unajikatia", hii ina maana kwamba, mtu ambaye anafanya mapenzi bila kutumia kinga basi anahatarisha maisha yake na kwamba, kifo ndio suluhisho lake. Sanda ni nguo ambayo huvalishwa marehemu tayari kwenda

kuhifadhiwa katika kaburi. Hapa, neno hili limetumika kiishara kuashiria mauti na kila asomaye shairi hili hupata ishara kwamba, UKIMWI ni ugonjwa usio na tiba na kifo ndio hitimishi lake.

Mshairi mwingine ambaye naye ana matumizi ya lugha ya ishara katika shairi lake ni Breik S. Breik, kupitia shairi lake la "Kilo mbili ni hatari," anaeleza:

> Ninapanga tungo yangu, pembe zote za dunia
> Niwaeleze wandugu, wasaa wanotumia
> Na kuvipanga mafungu, vitendo visojalia
> Zana bora si hakika, ushauri ni kuacha
>
> Haitaleta hakika, njia nyingi kupita
> Maafa yatawafika, pembe nne kuingia
> Na kubebwa kama paka, uzito usotimia
> Zana bora si hakika, ushauri ni kuacha
> **(NIPASHE, Machi 17, 1998. Breik S. Breik).**

Katika shairi hili, mshairi anajenga ishara ya kaburi anapozungumza juu ya "pembe nne kuingia." Kaburi kwa kawaida huchimbwa katika umbo la pembe nne na kumsitiri marehemu. Ishara hii inaonya kuwa yeyote anayekwepa kupatiwa ushauri nasaha ana hatari kubwa ya kupoteza maisha. Hii ina maana kwamba, mtu yeyote ambaye ameathirika kwa ugonjwa wa UKIMWI anaweza kuishi maisha marefu zaidi kwa kupatiwa ushauri nasaha kutoka kwa mtaalamu wa kazi hiyo. Kuhusiana na washairi kujenga ishara, kwamba mtu akipata UKIMWI basi suluhisho lake ni kifo, tulipata msukumo wa kufaya usaili na mtafitiwa mmoja aliyejulikana kwa jina la Changaa wa Gongo la mboto na kutueleza kwamba:

> Hakuna mtu asiyefahamu kuwa mtu akipata UKIMWI, kaburi linamsubiri kwa sababu UKIMWI hauna tiba mpaka kufikia leo. Tangu UKIMWI ulipogundulika mpaka leo ni karibu miaka thelathini sasa na hakuna tiba iliyogundulika. Kwa hiyo washairi wa magazetini hawajakosea kueleza kwamba, mtu akiupata UKIMWI hana cha kusubiri zaidi ya kifo. Ninasema hivi kwa sababu hata wale

> ambao wanatumia dawa za kurefusha maisha huwa hawaponi kwani baada ya muda dawa hizo hukosa nguvu nao hufariki dunia. Kwa maoni yangu, UKIMWI hauna kinga wala tiba na yeyote atakaye upata basi ajue kwamba atafariki dunia.

Maelezo haya yanawiana na yale yaliyowasilishwa na mshairi katika shairi lake hapo juu kwamba, mtu akiambukizwa UKIMWI basi suluhisho lake ni kifo na kuingizwa kaburini. Kwa maoni yetu, tunayaona mawazo haya kuwa yana ukweli kwa kiasi fulani hasa tukirejelea pale tu ugonjwa huu ulipogundulika kwa mara ya kwanza. Katika kipindi hicho, watu wengi walipoteza maisha kutokana na UKIMWI kwa sababu kwanza ugonjwa wenyewe ulikuwa haujafahamika vizuri na namna za kupambana nao pia ilikuwa haijafahamika. Hata hivyo, katika kipindi tulichonacho hivi sasa, mawazo ya Changaa hapo juu, yanaonekana kukosa mashiko kwa sababu sasa hivi kumegundulika mbinu nyingi za kupambana na ugonjwa huo. Kutokana na kugundulika kwa mbinu hizo, muathirika wa UKIMWI anaweza kuishi maisha kama wale ambao hawajaathirika na kisha akafa kifo cha kawaida kisicho na mateso makubwa kama ilivyokuwa kwa waathirika wa miaka ya mwanzo.

Mshairi mwingine wa magazetini anayefahamika kwa jina la Emmanuel Mkondoa, anatupatia aina ya ishara ambayo inaeleza mwenendo wa tabia yenye kusababisha maambukizi ya UKIMWI. Katika shairi "UKIMWI kubwa balaa," anaeleza:

Tuzibadili tabia, za mambo ya mapokezi
Kuwa na wapenzi mia, kamwe hupati pongezi
Ni bure utaumia, kwa jambo la kishenzi
UKIMWI kubwa balaa, tukamilishe ulinzi

Sasa nakunja zuria, zinatosha beti hizo
Kwani nimekushinda, kuwaasa kwa utenzi
Hayo msije puuzia, mkaja laumu walozi
UKIMWI kubwa balaa, tukamilishe ulinzi

**(MTANZANIA, Januari 9, 2001. Emmanuel Mkondoa).**

Katika shairi hili msanii anatupatia ishara kwamba, tabia za mapokezi ndio hasa chanzo kikubwa cha kuukwaa ugonjwa wa UKIMWI. Tabia za mapokezi ni ishara inayorejelea watu ambao wanapenda kuwa na wapenzi wengi pasipo kutambua kuwa wanajipalia mkaa wa moto mwilini mwao na hivyo kuhatarisha maisha yao. Ilizoeleka katika miaka ya hivi karibuni, kwamba mtu akiwa na wapenzi wengi, hupewa sifa, kuwa yeye ni kidume cha mbegu na hivyo kuzidisha kasi ya kutafuta wapenzi wengine zaidi jambo ambalo linahatarisha maisha yao. Hili linathibitika pale mshairi anaposema kwamba, “Kuwa na wapenzi mia, kamwe hupati pongezi.” Hii inaonesha, watu walikuwa wakipewa pongezi kwa kuwa na mpenzi zaidi ya mmoja. Katika usaili wetu na Joseph Mwanahewa msomaji wa mashairi ya magazetini eneo la Kawe alitueleza kwamba:

> Ninakumbuka katika miaka ya 1990 na mwanzoni mwa miaka ya 2000, vijana wengi wa kiume waliona ufahari kuwa na mahusiano ya kingono na wanawake wengi na kwa hili baadhi ya vijana wenzao waliwasifu kuwa wao ni madume ya mbegu. Vile vile, waliwapatia sifa kuwa, mwanamume aliye na wapenzi wengi ni mtanashati na ana fedha za kutosha kuwapatia wanawake wote anaohusiana nao kimapenzi. Hali hii ilisababisha vijana wengi kupotea maisha kwa kuambukizwa UKIMWI. Kwa upande wa vijana wa kike, wao walikuwa wakiwaita wanamume hao kuwa ni mabuzi. Mwanamke aliyekuwa na mabuzi wengi naye bila shaka alisifiwa kuwa yeye ni mzuri sana ndio maana ana uwezo wa kuwatamanisha wanaume wengi na kisha wakamtaka. Hata hivyo, baadhi ya watu walimuona mwanamke mwenye tabia hii kuwa ni malaya na hafai kabisa katika jamii huku mwanaume mwenye tabia kama hizo akipata sifa nzuri badala naye pia kuitwa malaya.

Mawazo haya yanatoa picha ya kwamba, ishara iliyotolewa na mshairi ina ukweli ambao hauwezi kupingwa mahali popote. Mawazo haya yanaonesha kwamba, jamii ilikuwa bado haijauelewa vizuri UKIMWI ndio maana baadhi ya wanajamii walikuwa na tabia za uasherati uliokithiri. Hivyo, ishara inayojengwa na mshairi, inaitaka jamii kubadili tabia na mienendo yao kuhusu mahusiano ya kimapenzi ili

waepuke maambukizi ya UKIMWI. Baada ya kushughulikia lengo mahususi la kwanza lililohusu kuchunguza tamathali za usemi katika mashairi ya UKIMWI ya magazetini, sehemu inayofuata inachambua lengo mahususi la pili.

## 4.3 Dhamira katika Mashairi ya Magazetini

Dhumuni mahususi la pili katika utafiti huu lilikuwa ni kubainisha dhamira zinazojengwa na lugha ya kitamathali katika mashairi ya magazetini. Kimsingi, kama inavyojibainisha katika matokeo ya utafiti juu ya dhumuni mahususi la kwanza la utafiti huu, lugha ya kitamathali katika mashairi ya magazetini ina mchango muhimu katika kujenga na kuwasilisha dhamira kwa hadhira na jamii iliyokusudiwa. Hata hivyo, katika dhumuni hilo la kwanza dhamira hazikuchambuliwa bali baadhi yake zilidokezwa tu katika harakati za kukamilisha dhumuni hilo. Uwasilishaji na uchambuzi wa data juu ya dhumuni mahususi la pili unafanywa hapa chini kama ifuatavyo:

### 5.3.1 UKIMWI na Umalaya

Mashairi ya magazetini yanaifafanua na kuiwasilisha dhamira hii kwa umakini mkubwa kupitia lugha ya kitamathali inayopatikana katika mashairi hayo. Umalaya ni hali ya mtu kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wapenzi zaidi ya mmoja hali ya kuwa mtu huyo tayari ana mwenzi wake ambaye anatambulika kisheria, yaani kupitia ndoa (Arinaitwe, 2011). Fasili hii ya Arinaitwe (ametajwa) tunakubaliana nayo kwa kiasi fulani kwa sababu inadokeza juu ya dhana nzima ya umalaya. Hata hivyo, ni vema ikafahamika kwamba, umalaya hauwahusu watu ambao tayari wapo katika ndoa peke yake, bali hata wale ambao hawajaingia katika mahusiano ya ndoa lakini wanapokuwa na mahusiano ya kimapenzi na wapenzi zaidi ya mmoja nao

hutambulikana kwa jina la malaya. Washairi wa magazetini wanaeleza, chanzo kikubwa cha maambukizi ya UKIMWI ni umalaya na kusisitiza, kama jamii haitajihadhari kutokana na umalaya basi itaangamizwa kwa ugonjwa wa UKIMWI. Mshairi Nzinku kupitia shairi lake la "UKIMWI," analeza kuwa:

> Ulianzia Kagera, na mikoa ya jirani
> Ukawashika wakora, wanaoishi mijini
> Ukafika na Tabora, hadi kwetu mikoani
> UKIMWI kweli tishio, kwa maisha yetu sote
>
> Chanzo chake umalaya, tembea huku na huku
> Watu kutoka Ulaya, ulikotoka ni huko
> Kuchangia damu mbaya, nazo nyembe kupeana
> UKIMWI kweli tishio, kwa maisha yetu sote.
> **(MAJIRA, Oktoba 30, 2002. Nziku, A.L.M).**

Katika ubeti wa pili wa shairi lililodondolewa hapo juu, inaonesha kuwa chanzo cha UKIMWI ni umalaya. UKIMWI ulianzia Kagera na ukaeenea kwa kasi kubwa katika sehemu mbalimbali nchini kutokana na umalaya. Anafafanua katika ubeti wa kwanza, baada ya UKIMWI kuwapata watu wa Kagera na baadaye ukawapata wakora wa mijini, akiwa na maana ya wanawake malaya. Tulifanya usaili na Bi Mwantumu Selemani wa Tandika Dar es Salaam kuhusiana na suala hili, naye akatueleza kwamba:

> Umalaya ni chanzo kikubwa cha maambukizi na kuenea kwa ugonjwa wa UKIMWI katika jamii yetu. Tazama, hapa Tandika, yapo madanguro ya wamama na wasichana ambao hawana kazi ya kufanya na badala yake wanajiuza. Huu ni umalaya uliovuka mipaka. Malaya hawa wanasababisha kuenea kwa ugonjwa wa UKIMWI kwa kasi ya ajabu na kulifanya taifa kupoteza nguvu kazi kwa sababu wengi wanaopata UKIMWI ni vijana. Sisemi kwamba, watu wazima hawaupati UKIMWI la hasha! Ila, nimetoa mfano wa vijana kwa sababu wao ndio nguvu kazi ya taifa.

Maelezo haya yanaonesha kwamba, chanzo kikubwa cha UKIMWI ni umalaya na hasa ule unaosababishwa na akina mama wanaojiuza. Watu hawa wanafanya

biashara ya ngono na hivyo kila mwanamume ambaye atawataka hukubaliwa baada ya kutoa fedha. Kutokana na umalaya huo UKIMWI unaenea kwa sababu akinamama wanaojiuza wameweka bei maalumu, kwa wanaume wenye kutumia na wasiotumia Kondomu (Low, 2011). Kwa mantiki hii ni dhahiri kwamba, uwezekano wa kuambukizwa UKIMWI ni mkubwa mno kwa sababu ya kufanya ngono zembe.

Kimsingi, umalaya haufanywi na akina mama wanaojiuza peke yao bali wakishirikiana na wanamume ambao baadhi yao wameoa na wana familia zao. Jambo hili kwa hakika linasababisha kuongezeka kwa maambukizi ya UKIMWI kwa kasi kubwa kwa sababu huyu mwanamume ambaye anafanya umalaya na wakora anaweza kupata maambukizi ya UKIMWI na yeye akamwambukiza mkewe. Ikatokea bahati mbaya huyu mwanamke naye ana mwanamme mwingine basi naye anamwambukiza na mtandao unazidi kukua zaidi na zaidi (Arinaitwe, 2011).

Naye Asanterabi Sufiani, kupitia shairi lake la “AIDS”, anaeleza kwamba, umalaya ndio chanzo kikubwa cha maambukizi ya UKIMWI. Katika ubeti wake mmoja anasema:

> Gonjwa hili maradufu, chimbuko uhayawani
> Katika mambo machafu, kuchezeana mwilini
> Halileti usumbufu, kama kidonda mwilini
> Kuepukana UKIMWI, tuepuke umalaya
> **(MZALENDO, Mei 22, 1988. Asanterabi Sufiani).**

Katika shairi hili tunaelezwa kwamba, chanzo cha UKIMWI ni umalaya na kwamba ili jamii iweze kuepukana na UKIMWI, inapaswa kuacha umalaya. Kimsingi, jambo linaloelezwa na washairi hawa kuwa linasababisha kuenea kwa UKIMWI lina ukweli ambao unaweza kuaminiwa kitaaluma na wanajamii wengi wamepata ugonjwa huu

kutokana na umalaya wa aidha mpenzi mmoja au wote wawili. Tunaungana mkono na mshairi kutoa wito kwa jamii kuachana na vitendo vya uasherati ili kuepukana na UKIMWI kwa nia ya kuendeleza na kuimarisha nguvu kazi ya taifa.

### 5.3.2 Chanzo Cha UKIMWI

Maelezo hapo juu yanaonesha kwamba, chanzo cha UKIMWI ni umalaya, ingawa yapo maelezo mengine ambayo yanasema, chanzo cha UKIMWI ni Ulaya ikiwa na maana kuwa, Wazungu ndio walioleta UKIMWI katika bara la Afrika. Dhana hii imegusiwa hapo juu kidogo wakati tukiwa tunafafanua baadhi ya tamathali za usemi lakini haikuelezwa kwa kina kama ilivyofanyika katika sehemu hii. Washairi wa magazetini wanatupatia dhamira kwamba, chanzo cha ugonjwa wa UKIMWI ni Wazungu ambao waliuandaa ugonjwa huo kwa ajili ya kukiteketeza kizazi cha Mwafrika kisha warudi tena kulitawala bara hili kama ilivyokuwa katika kipindi cha Ukoloni. Miongoni mwa washairi hao ni John Coster Mpunga ambaye anaeleza kwamba:

> Chanzo sio Afrika, bara letu la heshima
> Nchi za Ulaya peka, walikoanza kukwama
> Ndipo walipanganika, ili raha kutunyima
> UKIMWI shida hatari, huua mamilioni
> Wazungu walitamka, Afrika ya Wanyama
> Jaa la kutupa taka, lenye wingi wa vilema
> Mabinti wakawasaka, nia wapate kukwama
> UKIMWI shida hatari, huua mamilioni
> **(UHURU, Januari 5, 1990. John Coster Mpunga).**

Katika beti hizi mbili za shairi, tunaelezwa kwamba chanzo cha UKIMWI ni Ulaya ikiwa na maana kwamba ni Wazungu ndio waliouleta UKIMWI katika bara la Afrika kwa sababu wanawachukia sana watu weusi. Mshairi anasema, Bara la Afrika ni bara la heshima kwa hiyo UKIMWI hauwezi kuanzia hapa jambo linaloashiria kwamba,

Ulaya ni bara la watu ambao daima hawawatakii mema Waafrika. Mshairi anasema kwamba, Wazungu walitamka kwamba bara la Afrika ni la Wanyama kwa hivi wanastaili kupatiwa janga ambalo litawasambaratisha wamalizike kabisa.

### 4.3.3 Unyanyapaa

Unyanyapaa ni hali ya kumtenga mtu au jamii ya watu kutokana na mtu au jamii husika kupatwa na jambo ambalo ni hatari kwa afya yake yeye mwenyewe, lakini pia hatari ya kuwaambukiza watu wengine ikiwa watashirikiana naye katika masuala mbalimbali ya kimaisha na kijamii kwa jumla. Unyanyapaa ni dhana inayokaribiana sana na ubaguzi lakini kuna tofauti kidogo. Tofauti yenyewe ni kwamba, ubaguzi unaweza kuwa wa rangi, jinsia, kabila, dini na kiwango cha elimu (Mutembei, 2009). Katika miaka ya mwanzoni ambapo UKIMWI uligundulika, ndugu na jamii iliwanyanyapaa ndugu zao walioathirika kwa UKIMWI kwa madai kwamba ni watu hatari sana na kwamba, watasababisha hata wale ambao hawajaambukizwa nao kuambukizwa na kisha kuleta maafa makubwa zaidi katika jamii. Mutembei (2009) anaeleza kwamba, unyanyapaa dhidi ya waathirika wa UKIMWI ulikwenda mbali zaidi mpaka ikafikia mahali baadhi ya wanajamii wakaanza kupendekeza kuwa waathirika wa UKIMWI waandiliwe mahali maalumu pa kuishi tafauti na makazi ya kawaida ya jamii. Baadhi ya wanajamii walipendekeza kwamba, waathirika wa UKIMWI waandaliwe kisiwa maalumu kuwa ndio mahali pao pa kuishi na mtu yeyote ambaye ataupata UKIMWI basi naye atapelekwa katika kisiwa hicho. Washairi wa magazetini kama ilivyo kawaida yao, wameisawiri dhamira hii katika mashairi yao kwa kutumia tamathali mbalimbali za usemi. Mshairi Magret Clemence kupitia shairi lake la “Tujihadhari UKIMWI”, anaeleza kwamba:

Sitaki kuna UKIMWI, gonjwa limesambatika
Sitaki wenda siumwi, akinijali rabika
Sitaki nisiwe zimwi, kwa kushindwa kutibika
Muache akina kaka, chamoto kunisakama
**(UHURU, January 7, 1991, Magreti Clemence)**

Katika shairi hili tunaona mshairi akitumia sitiari ya zimwi kujenga dhamira ya unyanyapaa dhidi ya waathirika wa UKIMWI katika jamii. Mshairi anaeleza kwamba, baadhi ya wanajamii waliwatazama waathirika wa UKIMWI kama watu waliolaaniwa na wasio na thamani yoyote katika jamii kiasi cha kufananishwa na zimwi. Katika hali ya kawaida, zimwi ni aina ya mnyama ambaye huwa haonekani kwa macho ya mwanadamu na hufikirika mawazoni tu. Mnyama huyu huwa anaogopeka sana kwa sababu ana tabia ya kuwadhuru wanaadamu-kwa misingi ya wale wanaoamini suala hili. Kwa mantiki hii, kumfananisha mgonjwa wa UKIMWI na zimwi ni unyanyapaa wa hali ya juu sana unaonesha kwamba, muathirika wa UKIMWI amekuwa ni mnyama na si mwanadamu tena anastahili kuogopwa na kuepukwa. Unyanyapaa wa aina hii ulifikia mahali baadhi ya wanafamilia kuwakimbia watu wao na watu hao wakabaki wenyewe jambo lililosababisha asilimia kubwa ya waathirika kupoteza maisha mapema na kuziacha familia nyingi zikiwa yatima (Low, 2011).

Mshairi mwingine kwa jina la Abdalla Mkumbila anatupatia shairi “Amebainika” ambalo linaeleza mambo yanayohusiana na unyanyapaa kwa waathirika wa UKIMWI. Anasema:

Hakika ameumbuka, sasa amebainika
Mafichoni ametoka, hadharani kesha fika
Sasa kesha haribika, nani anayemtaka
Ameoza ananuka, yupo kama takataka

Mwanzoni alitukuka, heshima alijitwika
Tulidhani kaongoka, kiongozi msifika
Tulimwona hana shaka, na tena ameongoka
Ameoza ananuka, yupo kama takataka.

Yake siku imefika, tena amegundulika
Hayawani kasifika, mbaya kabainika
Ugonjwa umemshika, kwenye geti akitoka
Ameoza ananuka, yupo kama takataka

Thamani imeondoka, sifa zimeshamtoka
Watu wengi walifika, kumuona msifika
Kuhara na kutapika, yupo chini kaanguka
Ameoza ananuka, yupo kama takataka
**(UHURU, Januari 7, 1999. Abdalla Mkumbila).**

Katika shairi hili, tunaona matumizi ya tashibiha yakitupatia dhamira ya unyanyapaa dhidi ya waathirika wa UKIMWI hasa katika msitari wa mwisho pale anaposema "ameoza ananuka, yupo kama takataka". Unyanyapaa wa aina hii umevuka mipaka ya kibinadamu na kumuona mwathirika wa UKIMWI sawa na takataka-jambo lenye kusikitisha na kuhuzunisha sana. Kutokana na miiko ya Kiafrika yenye kuthamini utu wa mwanadamu, hata kama maiti kwa mfano, alifariki akiwa mwenyewe na hakuna mtu yeyote anayefahamu na hivyo akutwa akiwa katika hali isiyo ya kawaida, husemwa kwamba, maiti imeharibika lakini sio maiti imeoza. Kwa mantiki hiyo, kumuita mwanadamu kuwa ameoza eti kwa sababu amepata UKIMWI ni unyanyapaa wa hali ya juu sana.

Katika kuisawiri dhamira hii ya unyanyapaa mshairi anaoesha hali aliyokuwa nayo mwathirika wa UKIMWI kabla ya kuupata ugonjwa huo kuwa alikuwa ni mtu mwenye afya nzuri tena msifika katika jamii. Hata hivyo, baada ya kuupata UKIMWI na hali yake ya afya kudhoofika basi anaonekana kuwa si mwanadamu

tena kiasi cha kuambiwa ameoza na ananuka. Unyanyapaa wa aina hii huwafanya baadhi ya walioambukizwa UKIMWI kuwa na hasira kali na hivyo kuamua nao kuusambaza ugonjwa huo kwa watu mbalimbali ambao kwa namna moja au nyingine hawana hatia yoyote.

Dhamira hii inaonesha kwamba, elimu kwa umma kuhusu UKIMWI inahitajika kutolewa kwa kiasi kikubwa ili jamii iepukane na unyanyapaa dhidi ya waathirika wa UKIMWI. Kwa kiasi kikubwa elimu hiyo imetolewa na suala la unyanyapaa si kubwa katika jamii ya leo ikilinganishwa na ilivyokuwa huko nyuma. Hii haina maana kwamba, elimu ya kutokomeza unyanyapaa inatakiwa ikome na isitolewe tena la, bali inapaswa kuendelea kutolewa kwa sababu zipo jamii ambazo bado zinawanyanyapaa wagonjwa wa UKIMWI hasa wanapokuwa katika hali ambayo hawawezi kujimudu wao wenyewe (Arinaitwe, 2011). Si hivyo tu, bali pia, unyanyapaa wa waathirika wa UKIMWI umebadilika kwa aina tu, lakini bado upo hasa katika nafasi za ajira na kulipiwa gharama za masomo hasa yale ya nje ya nchi. Hutokea katika taasisi nyingi hasa zile zisizo za serikali kuwapima kwanza UKIMWI wale walioomba kazi katika taasisi hiyo kabla ya kuwapatia kazi na yeyote atakayebainika kuwa na UKIMWI hawezi kuajiriwa. Huu nao bado ni unyanyapaa dhidi ya waathirika wa UKIMWI.

### 4.3.4 Kinga ya UKIMWI

Dhamira inayohusu kinga ya UKIMWI imeelezwa kwa kiasi kikubwa katika mashairi ya magazetini. Washairi wa magazetini wanaeleza kwamba, matumizi ya kondomu ni muafaka katika kuzuia ugonjwa huo hatari hasa kama itatumiwa vizuri na wale ambao wanataka kujikinga dhidi ya UKIMWI. Miongoni mwa washairi

wanaoelezea suala hili ni Mohamed Limbetembe katika shairi lake la "Tujikinge na UKIMWI" anaeleza kwamba:

Kama ukiwa muhuni, hujajaliwa kuoa
Huna vyombo salimini, kondomu ukatumia
Kinyume hapo amini, sanda unajikatia
Tujikinge na UKIMWI, kulinda wetu uhai

Wanawake yafateni, sharti kinga tumia
Mpenzi uso mwamini, kondomu kuitumia
Magonjwa ya hatari, ya zinaa jikingea
Tujikinge na UKIMWI, kulinda wetu uhai
**(MAJIRA, Machi 27, 1997. Mohamed Limbetembe).**

Katika shairi hili, tunaoneshwa kwamba, kinga ya UKIMWI ni kutumia Kondomu hasa kwa yule ambaye hajaoa au kuolewa anapoamua kufanya mapenzi na mwanamke au mwanaume ambaye hamwamini kuwa ni mwaminifu na mwadilifu. Mshairi anaendelea kueleza kwamba, Kondomu ni kinga imara kwa magonjwa mengine ya zinaa, kwa hivyo ni vema kila mja akajikinga magonjwa hayo kwa kutumia kondomu. Kwa maoni yetu, tunaona kwamba, maelekezo ya mshairi yanapingana na kile anachokiamini yeye. Mshairi anaamini kwamba, Kondomu ni kinga ya UKIMWI halafu tena anatoa uhuru kwa mtumiaji kuitumia katika kujamiiana na mtu ambaye hamwamini. Tulidhani kwamba, ingekuwa vema akaeleza bayana kwamba, kila mara huyu ambaye anaitwa na mshairi kwa jina la muhuni anapofanya tendo la ndoa ni lazima atumie kondomu kwa sababu huyu mwenza aliyenae hajamuoa na hivyo anaweza kuchukuliwa na mwanaume mwingine wakati wowote. Kwa hivi suala la kumwamini mtu kuwa ni mwaminifu huku hujamuoa au hajakuoa lina hatari kubwa ya kusababisha maambukizi dhidi ya UKIMWI. Hata hivyo, haya ni maoni yetu tu, na suala hili linaweza kujadiliwa kwa mapana zaidi na wanataalimu wengine wanaohitaji kufanya hivyo.

### 4.3.5 Hitimishi

Katika sehemu hii tumechambua kuhusu lengo mahususi la pili ambalo lilihusu kubainisha dhamira zinazojengwa na matumizi ya lugha ya kitamathali katika mashairi ya magazetini. Miongoni mwa dhamira ambazo tumezieleza katika sehemu hii ni asili ya UKIMWI, UKIMWI na umalaya, unyanyapaa na kinga ya UKIMWI. Kwa harakahara msomaji anaweza akadhani kwamba, dhamira zilizoelezwa ni chache lakini kwa hakika ni nyingi sana. Ni nyingi kwa maana kwamba, tulipokuwa tunawasilisha dhumuni mahususi la kwanza katika utafiti huu tumebainisha pia dhamira mbalimbali. Ni ukweli usiopingika kwamba, unapoeleza juu ya tamathali fulani ya usemi kama inavyojitokeza katika shairi ni lazima pia utaeleza tamathali hiyo inaelezea jambo gani. Kwa kufanya hivyo utakuwa umeainisha dhamira za aina mbalimbali, na bila shaka tumefanya hivyo.

## 4.4 Dhima ya Tamathali za Usemi katika Kujenga Dhamira

Dhumuni mahususi la tatu la utafiti huu ni kuchunguza dhima ya tamathali za usemi za mashairi ya magazetini katika kuwasilisha dhamira kwa wasomaji na wasikilizaji wa mashairi. Katika kujibu dhumuni mahususi la kwanza la utafiti wetu, tumeweza kubainisha tamathali za usemi katika mashairi ya magazetini yaliyoteuliwa. Tamathali za usemi katika mashairi ya magazetini zina dhima za kimaudhui na kifani.

### 4.4.1 Dhima za Kimaudhui

Tamathali za usemi katika mashairi ya Kiswahili zina dhima kubwa ya kuwasilisha dhamira na maudhui kwa ujumla kwa wasomaji wake. Tumeona katika dhumuni

mahususi la pili la utafiti wetu dhamira mbalimbali zikiwasilishwa na tamathali za usemi.

#### 4.4.1.1 Kumfikirisha Msomaji

Ili kuweza kuwasilisha dhamira kwa jamii iliyokusudiwa tamathali za usemi zina dhima ya kumfikirisha msomaji juu ya kile anachokisoma ndipo aweze kupata dhamira zinazozungumzwa na mwandishi wa shairi husika. Kwa mfano, wasanii wa mashairi ya magazetini wanapotumia taswira mbalimbali kama vile “kiroba”, “soksi” au “zana” ambayo hutumika kurejelea Kondomu humhitaji msomaji kutafakari kwa makini ili aweze kuelewa dhamira mbalimbali zinazowasilishwa kwake na mtunzi wa shairi. Msomaji atazitafakari taswira hizi kwa makini huku akizihusianisha na uzoefu wake wa mambo katika mazingira na kisha akaweza kupata dhamira nyingi zilizojificha.

Kwa hakika, ukweli huu unamfanya msomaji kuwa ni mzalishaji wa maana tafautitafauti ziwakilishwao na taswira katika mashairi ya magazetini badala ya kuwa mtu wa kutafuniwa chakula na kisha kukimeza tu. Kezilahabi (1983) anaeleza kwamba, kazi ya fasihi kama ilivyo riwaya na ushairi zinahitaji kutungwa kwa namna ambayo itamfikirisha msomaji kidogo ili aweze kupata maana au dhamira katika kazi anayoisoma na huo ndio uhai wa kazi ya fasihi. Anaendelea kueleza kwamba, ukiona kazi inayodaiwa kuwa ni ya kifasihi halafu haimfanyi msomaji kutafakari ndipo aipate maana basi kazi hiyo itakuwa na mapungufu kisanaa. Kwa msingi huo, msomaji wa mashairi ya magazeti tuliyoyateua katika utafiti wetu anaposoma na kukutana na taswira ambazo tumeziainisha hapo juu anapata kufahamu kwamba, zinazungumzia kujikinga na UKIMWI. Tulifanya usaili na Bi.

Jasmini Ayubu wa Manzese Dar es Salaam kuhusiana na suala hili akatueleza kwamba:

> Mimi ni mpenzi wa mashairi ya magazetini, na daima huwa ninanunua gazeti la UHURU kwa ajili ya kusoma mashairi kwa sababu gazeti hili huandika mashairi kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na magazeti mengine ya hapa nchini. Ninaposoma shairi kisha nikakutana na matumizi ya lugha ya taswira huwa ninavutiwa sana kwa sababu lugha ya aina hiyo hunifanya nielewe vizuri kazi husika. Vile vile matumizi ya lugha ya kitamathali hunifanya kuipata dhana husika vizuri na kwa undani kabisa kuliko inavyotumika lugha ya kawaida kurejelea jambo. Mshairi anapotumia lugha ya kawaida hunifanya mimi kuliona shairi lake kuwa ni la kawaida mno na hivyo ninakosa hamu ya kulisoma shairi hilo tena na tena. Pia, matumizi ya lugha ya kitamathali, hutoa uwanja mpana kwa mshairi kujenga dhamira tafautitafauti kutoka katika msitari au ubeti mmoja tu wa shairi.

Maelezo ya mtafitiwa wetu hapo juu yanaungana mkono na mawazo yetu kuhusiana na dhima ya matumizi ya tamathali za usemi katika kujenga dhamira za mashairi ya magazetini. Mtafitiwa anaendelea kueleza kwamba, matumizi ya tamathali za usemi katika mashairi ya magazetini ni kitu ambacho kinamvutia sana na hivyo kulazimika kununua gazeti la UHURU kila toleo linapotoka. Mtafitiwa anadokeza kwamba, matumizi ya lugha ya kawaida katika mashairi ya magazetini huwafanya wasomaji kutovutiwa kuyasoma mashairi hayo kwa sababu yanaonekana ni ya kawaida mno na kutokuwa na tafauti na maandishi mengine ya makala au habari yoyote katika gazeti. Matumizi ya lugha ya aina hii huwavunja moyo wasomaji wa mashairi ya magazetini kwa kutovutiwa kuyasoma.

Si hivyo tu bali pia, matumizi ya lugha ya kitamathali katika mashairi ya magazetini humsaidia msomaji kujenga dhamira mbalimbali kutokana na kuihusianisha lugha hiyo na uhalisia katika jamii. Taswira zinazorejelea Kondomu tulizoziainisha hapo

juu ni maneno ambayo wanajamii huyatumia katika mawasiliano yao ya kila siku. Maneno kama “kiroba”, “soksi” na “zana” ni maneno ambayo yanatumiwa na vijana wanapokuwa vijiweni. Maneno haya yamezoeleka katika jamii na yanafahamika kwa makundi ya wazee, akina mama na wasichana. Kutokana na kufahamika kwa maneno haya katika jamii, na wasomaji wanapokutana nayo katika mashairi ya magazetini inakuwa ni rahisi kwao kupata dhamira kwa namna iliyokusudiwa na mwandishi.

#### 4.4.1.2 Kuhamasisha Jamii

Tamathali za usemi zinazotumika katika mashairi ya magazetini zina dhima ya kufanya uhamasishaji wa jambo katika jamii. Omary (2011) alipotafiti masuala ya kisiasa katika ushairi wa Kezilahabi alieleza kwamba, uhamasishaji ni kitendo cha kuitaka jamii kufanya jambo fulani na kuacha kufanya jambo jingine kwa nia ya kuepuka madhara yanayoweza kupatikana kama hawatasikiliza maelekezo ya muhamasishaji. Anaendelea kueleza kwamba, jamii inaweza kukosa faida ambazo inaweza kuzipata kama haitasikiliza maelekezo ya muhamasishaji ikiwa jambo analohamasisha lina masilahi ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Tamathali za usemi katika mashairi ya magazetini hufanya kazi ya kuhamasisha jamii katika mambo mbalimbali moja wapo likiwa ni juu ya kujikinga na UKIMWI. Kwa mfano, mshairi Mbasa Tumwimbile, katika shairi lake, “Kupima UKIMWI sheria”, anaeleza kwamba:

Ni vita kufa kupona, kupima iwe sheria
Wote hata waungwana, washikao bibilia
Kwa waheshimiwa sana, bungeni wanasheria
Kupima iwe sheria, UKIMWI watumaliza

Ubaladhuli acheni, waeneza na UKIMWI
Busu zenu ulimini, ute ovyo wa UKIMWI
Mnasinyaa maishani, kuchakazwa na UKIMWI
Kupima iwe sheria, UKIMWI watumaliza
**(MAJIRA, Januari 5, 2002. Mbasa Tumwimbile).**

Tunapolitazama shairi hili kwa makini tunabaini kwamba, limesheheni tamathali tafautitafauti za usemi zenye nia ya kuhamasisha jamii kupima damu ili kufahamu hali ya afya zao kama wameathirika au la. Mshairi anasema kwamba, kupima UKIMWI na kufahamu afya ni njia mojawapo ya kupambana na UKIMWI, kwa kuwa wale ambao watagundulika kuwa wameathirika basi hawatawaambukiza watu wengine kwa makusudi. Anatumia lugha ya kiuhamasishaji pale anaposema kwamba, "ni vita kufa kupona" akiwa na maana kwamba, mapambano dhidi ya UKIMWI hayatakiwi kukoma hata mara moja. Vile vile, anatumia tamathali aina ya taswira ambayo inaonesha kwamba, UKIMWI kwa kawaida humfanya muathirika kudhoofika sana na hivyo ni vema kila mtu akapima na pale atakapotambua kuwa ameathirika basi atachukua hatua ambazo zitamwezesha kuwa na afya nzuri daima na kutotambulikana kirahisi katika jamii kuwa ameathirika kwa UKIMWI. Taswira hii inapatikana pale anaposema kwamba, "Mnasinyaa maishani, kuchakazwa na UKIMWI".

Si hivyo tu, bali pia, katika msitari huu wa shairi tunaona mshairi akitumia tamathali ya usemi ijulikanayo kama tashihisi pale anaposema kwamba, "kuchakazwa na UKIMWI" akiwa na maana kwamba, UKIMWI ni ugonjwa hatari sana ambao unaleta madhara makubwa kwa muathirika wa ugonjwa huo. Dhana hii ya kuchakazwa na UKIMWI inakwenda mbali zaidi na kueleza madhara ambayo familia au jamii ya muathirika inaweza ikayapata kutokana na aidha baba au mama

au mtu yeyote anayetegemea katika jamii akiupata UKIMWI. Kwanza itatumika fedha nyingi kwa ajili ya kumtunza na kumlea mgonjwa huyo na pale atakapofariki familia yake watakosa msaada wa kuendeshea maisha yao waliokuwa wanaupata kutoka kwa muathirika huyo.

Maelezo yaliyotolewa katika aya mbili za hapo juu yanaonesha kwamba, tamathali za usemi zina dhima kubwa ya kufanya uhamasishaji kwa jamii ili ihakikishe kwamba, inafanya kila linalowezekana kwa nia ya kupambana na UKIMWI. Tamathali hizi za usemi zinamtaka kila mwanajamii kuchukua hatua stahiki katika kupambana na UKIMWI kwa nafasi yake bila kumwachia mtu mmojammoja au taasisi fulani au serikali kufanya hivyo yenyewe. Vilevile, tamathali hizi za usemi zina dhima kubwa ya kuihamasisha jamii kuuogopa UKIMWI na kuoona kama ni kikwazo kikubwa cha maendeleo ya mwanadamu, kwa kuwa, hukatisha maisha ya mtu akashindwa kutimiza na kutekeleza ndoto zake. Kwa msingi huu, ni dhahiri kwamba, kila mwanajamii akiusikiliza na kuutekeleza uhamasishaji unaofanywa na tamathali za usemi za mashairi ya magazetini dhidi ya UKIMWI basi maambukizi yatapungua na kuufanya UKIMWI kutochukuliwa kama janga la kitaifa tena.

#### 4.4.1.3 Kufafanua Jambo

Tamathali za usemi katika mashairi ya magazetini zina dhima ya kufafanua masuala mbalimbali yenye masilahi kwa wananchi na taifa lao. Kufafanua jambo ni kulitolea maelezo ya kina ili liweze kufahamika vizuri mbele ya wale wanaopaswa kulifahamu jambo hilo kwa nia na makusudio yaliyolengwa na mtunzi wa shairi. Katika utafiti huu tunaona kwamba, tamathali za usemi zina dhima ya kufafanua njia ambazo

zinaweza kumfanya mtu akaambukizwa UKIMWI. Mshairi Yusuf R. R. Mfalme kupitia shairi lake la “Kuenea kwa UKIMWI,” anaeleza kwamba:

Wale wapenda zinaa, kondomu wanotumia
Wakizoea kuvaa, siku zikisha titia
Hatima wanazitwaa, mbali wanaziachia
Wenyewe huwa wasema, kwamba wamezoweana

Zile mila za kigeni, ndizo zinatusumbua
Ushamba uafukani, mila zetu hutibua
Wazazi nambari mbili, lawama kwenu natua
Ati mwaishi uzunguni, watoto kuvaa uchi!
**(UHURU, Mei 14, 2003. Yusuf R. R. Mfalme).**

Katika beti hizi mbili za shairi tunamuona mshairi akifafanua kwa kutumia tamathali ya usemi ya taswira baadhi ya mambo ambayo yanachangia maambukizi ya UKIMWI katika jamii zetu. Katika ubeti wa pili msitari wa tatu anaeleza kwamba, “watoto kuvaa uchi,” katika hali ya kawaida mtu hawezi kuvaa uchi, ni hali ya mtu kuwa utupu pasipo kuvaa nguo. Mtu anapokuwa hajavaa nguo ndio anakuwa yupo uchi na anapovaa nguo anakuwa amejisitiri. Kwa hakika, matumizi ya taswira hii yanatoa ufafanuzi kwamba, uvaaji wa nguo ambazo zinaonesha maungo na mapambo ya mwili hasa ule wa mwanamke basi huwatamanisha wanaume na kuwataka wanawake hao kimapenzi, jambo ambalo, huchangia maambukizi ya UKIMWI. Tulifanya usaili na Mzee John Mwasakija, mkazi wa Ilala Sharifu Shamba kuhusiana na suala hili naye akatueleza kwamba:

> Siku hizi dunia imeharibika sana mwanangu. Siku hizi mwanamke anavaa nguo ambazo zinamwacha uchi bila ya kuona haya yoyote mbele za wanaume na hata wanawake wenzake. Hali hii kwa kiasi kikubwa inachangia kuongeza maambukizi ya UKIMWI kwa jamii. Kama inavyofahamika, mwili wa mwanamke hasa wa Kiafrika umeumbwa na Mwenyezi Mungu kwa namna ambayo humvutia mwanamume yeyote rijali, anapoona maungo ya mwanamke hasa mapaja na makalio. Baadhi ya wanaume wanapoona maungo hayo huchanganyikiwa na kufanya kila wanaloweza mpaka ampate

> mwanamke huyo. Kwa kufanya hivyo, mwanamke huyo anaweza kukutana na vishawishi mbalimbali vya wanaume ambao tayari wameshaambukizwa UKIMWI. Vilevile, wanaume wote ambao pia watavutiwa na mwanamke huyo na kufanya nae mapenzi wanakuwa katika hatari ya kuambukizwa UKIMWI.

Maelezo haya yanathibitisha ufafanuzi unaoelezwa na mshairi juu ya mambo yanayochangia maambukizi ya UKIMWI katika jamii. Suala la wanawake na wasichana kuvaa mavazi ambayo yanaonesha maungo yao si utamaduni wa Mwafrika bali ni wa wageni hasa Wazungu. Kuiga utamaduni wa kigeni na kuufanya kama sehemu ya utamaduni wa jamii yetu hasa hili la mavazi limechangia katika kuongeza maambukizi ya UKIMWI katika jamii hasa katika kipindi kile ambacho jamii ilikuwa haina ufahamu mkubwa kuhusu UKIMWI.

#### 4.4.1.4 Kufanikisha Mawasiliano

Tamathali za usemi katika mashairi ya magazetini zina dhima ya kufanya mawasiliano katika jamii juu ya jambo au mambo ambayo mshairi anataka yaifikie jamii yake. Mawasiliano ni hali au kitendo cha kupashana habari kati ya mtu na mtu, mtu na kikundi, kikundi na kikundi, taasisi na mtu, jamii na jamii na kadhalika. Tamathali za usemi katika mashairi ya magazetini zina dhima ya kufanya mawasiliano kati ya mtunzi wa shairi na wadau wa masuala ya UKIMWI kwa nia na makusudio tafautitafauti. Kwa mfano, mshairi Camdulla Msimbe kupitia shairi lake la “Kitumbua,” Anaeleza kuwa:

Hata kwa kunywea chai, Sasa hakitamaniki
Kula tena hakifai, na wala hakiuziki
Mdomoni hakikai, mkononi hakishikiki
Kitumbua hakiliki, kimeingia mchanga

Afadhali ya chapati, bajia, donati na keki
Nile kwa huu wakati, roho juu siiweki
Mazingaombwe sipati, maungo hayachongeki

Kitumbua hakiliki, kimeingia mchanga
Nikikute kitumbua, nakipiga ovateki
Kisije kuniumbua, nikawa sieleweki
Watu nikawasumbua, shida kwao sipeleki
Kitumbua hakiliki, kimeingia mchanga

Katika beti tatu za shairi hapo juu, mshairi anatumia tamathali za usemi kwa nia ya kufanya mawasiliano na jamii kuhusu UKIMWI. Kitumbua ni neno ambalo limetumika kiishara kuashiria tendo la ngono ambalo utamu wake unafananishwa na ladha ya kitumbua. Kwa kawaida kitumbua kinapoanguka chini na kupatwa na mchanga basi hupoteza thamani na ladha yake kwa mlaji, atakula kitumbua hicho kwa hofu na mashaka asije akaumiza meno yake. Matumizi ya tamathali hii ya usemi yana dhima ya kuipasha jamii kuwa, tendo la ngono ambalo lina utamu sawa na kitumbua na pengine zaidi yake sasa ni hatari kufanywa hovyo hovyo bila ndoa na kuaminiana baina ya wapenzi wawili, kwa sababu mwisho wake ni kupata UKIMWI. Msomaji yeyote atakayekutana na shairi hilo atakuwa amepata taarifa, kwamba UKIMWI ni hatari na hivyo ajiepushe kufanya ngono zembe ambazo ni hatari kwa afya na maisha yake kwa jumla.

Katika ubeti wa tatu mshairi anajenga taswira kwamba, mwanamke wa barabarani yaani mwanamke asiyekuwa wa kwake anamuona kama mtu hatari. Akikutana naye barabarani atampita kwa kasi kubwa na kamwe hataki kuwa karibu na mwanamke huyo. Dhima ya ishara hii ni kuitaka jamii kutokuwa na mahusiano na wanawake au wanaume ambao wanakutana nao barabarani kwa sababu wanaweza kuambukizwa UKIMWI na kisha kuyaweka maisha yao rehani. Ishara hii pia inajenga picha kwamba, si jambo jema kwa mtu yeyote awe mwanaume au mwanamke kujenga

mazoea yanayoweza kumsababishia kuwa na uhusiano wa kingono na mtu huyo, jambo ambalo linaweza kumfanya apate UKIMWI.

### 4.5 Dhima za Tamathali za Usemi Kifani

#### 4.5.1 Kupamba Lugha

Tamathali za usemi ni mojawapo kati ya vipengele vya matumizi ya lugha ambapo matumizi ya lugha kwa ujumla ni kipengele cha kifani. Hivyo ni sawa na kusema, tamathali za usemi ni kipengele cha kifani. Kipengele hiki kina mchango mkubwa katika kupamba lugha kwa wasomaji wake. Matumizi ya lugha ya kitamathali yana mchango mkubwa katika kuifanya lugha kuwa yenye kuwavutia wasomaji wa mashairi. Mfano mzuri wa shairi ambalo linaonesha namna tamathali za usemi zilivyo pambo la lugha ni shairi lifuatalo:

Hizi zama za UKIMWI, ogopa kila mmoja
Usije dhani haumwi, unene sasa si hoja
Utaparamia Zimwi, na kufa kirejareja
Ogopa kila mmoja, hizi zama za UKIMWI

Vipimo vya macho yako, kwa sasa havina tija
Usitishwe miondoko, na ukubwa wa mapaja
Dunia yote mnuko, kila mtu anavuja
Ogopa kila mmoja, hizi zama za UKIMWI

Usidanganywe haiba, ya mtu mwenye daraja
Kitambi alichobeba, kisije kupa faraja
Utatwishwa msalaba, na wewe uwe mteja
Ogopa kila mmoja, hizi zama za UKIMWI

Usivutwe na mapambo, vidani na makoja
Vipodozi vya maumbo, vyeusi vinavyochuja
Dunia ya leo kombo, usije mwamini mja
Ogopa kila mmoja, hizi zama za UKIMWI

Viongozi na wasomi, wa bara au Unguja
Wote waone vichomi, wafanyie makharaja
Niogope hata mimi, kwa uzinifu nikija
Ogopa kila mmoja, hizi zama za UKIMWI
**(NIPASHE, Januari 27, 1999. Yusuf Marare).**

Katika beti hizi tano za shairi, yapo matumizi ya lugha ya kitamathali yenye dhima ya kupamba lugha na jamii hujenga dhamira mbalimbali baada ya kusoma shairi husika. Maneno kama vile, kitambi, vichomi, vipodozi vya maumbo, vyeusi vinavyochuja, utatwishwa msalaba na wewe uwe mteja, dunia yote mnuko, kila mtu anavuja ni baadhi tu ya maneno ambayo yanapatikana katika beti za hapo juu na kwazo lugha imepambika. Maneno haya yanajenga tamathali za usemi kama ishara, taswira, mafumbo, sitiari na kadhalika. Ukiyatazama maneno haya unaweza kuona ni ya kawaida mno, lakini yalivyotumika yanaonekana kuwa na upekee fulani. Maneno haya yanamtaka kila mtu kutomwamini mtu mwingine kuwa hajaathirika na UKIMWI kwa sababu tu kwamba amepambika, amenenepa, amejipodoa na kunawiri vizuri. Upo uwezekano mkubwa huyo anayedhaniwa hayaathirika kwa UKIMWI kwa kumuona tu kwa macho akawa ameathirika. Hivyo, tamathali za usemi zina dhima ya kuipamba lugha, na wakati wasomaji wanafurahika na uzuri wa lugha hiyo wanapata dhamira zilizokusudiwa na mtunzi wa shairi.

### 4.5 2 Tamathali za Usemi na Vipengele Vingine vya Kifani

Fani ya ushairi wa Kiswahili imeundwa kwa vipengele kama muundo, mtindo, wahusika, mandhari na matumizi ya lugha (Njogu na Chimerah, 1999). Matumizi ya tamathali za usemi katika mashairi ya magazetini yana dhima ya kumuwezesha mshairi kuchagua muudo au mtindo wa shairi lake. Hii ni sawa na kusema kwamba, tamathali za usemi humuelekeza msanii atumie muundo gani katika kuwasilisha ujumbe wake kwa jamii aliyoikusudia. Mshairi Danny A. Sanya katika shairi lake la “UKIMWI unamaliza,” anaeleza:

Nguo fupi wamevaa, kuwashawishi vijana
Jamii inakataa, na hao kuambatana
Sikia Mtanzania, UKIMWI tutaubana
UKIMWI unamaliza, ndugu uwe mwaminifu

Nguo zao zaangaza, zayaonesha maungo
Biashara watangaza, wameanza huko bongo
Mikoa waelekeza, wamefika na Ilongo
UKIMWI unamaliza, ndugu uwe mwaminifu
**(NIPASHE, Disemba 25, 2001. Danny A. Sanya).**

Kwa hakika, tunapotazama kwa makini kichwa cha shairi hili kisemacho “UKIMWI unamaliza,” tunakuta kuwa ni tamathali ya usemi ijulikanayo kama tashihisi. Tamathali hii ya usemi imeongoza vema uteuzi wa maneno mengine katika beti mbili za shairi hapo juu. Tamathali hii ya usemi inaupa UKIMWI uwezo na urari wa kutenda kama kiumbe mwenye uhai. Kutokana na hilo tunamuona mshairi akiteua muundo wa tarbia wenye kufuata urari wa vina na mizani. Vina vya kila mshororo vina uhusiano wa moja kwa moja na tamathali ya usemi iliyopo katika kichwa cha shairi. Vina kati “za” na mwisho “ngo” vinashadidia vizuri namna UKIMWI unavyoambukizwa katika jamii na baadae UKIMWI huo unavyoweza kuiangamiza jamii. Vile vile, tamathali hii ya usemi imemfanya mshairi kutumia tamathali nyingine ya usemi katika shairi lake kwa nia ya kueleza vizuri tashihisi inayojengwa katika kichwa cha shairi. Tamathali hiyo ya usemi ni taswira au ishara inayosema, “UKIMWI tutaubana,” katika msitari wa tatu wa ubeti wa kwanza wa shairi lililopo hapo juu.

### 4.5.3 Hitimishi

Dhumuni mahususi la tatu katika utafiti huu lililenga kubainisha dhima ya tamathali za usemi za mashairi ya magazetini kimaudhui na kifani katika kuwasilisha ujumbe

kwa jamii. Kwa upande wa dhima za kimaudhui tumeona kwamba, tamathali za usemi zina dhima ya kufikirisha, kuhamasisha, kufafanua na mawasiliano. Kwa upande wa fani tumeona kwamba, tamathali za usemi katika mashairi zina dhima ya kupamba lugha na kusaidia kujenga vipengele vingine vya kifani na kisha kujumuishwa katika shairi ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHI NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii tumefanya kazi ya kuwasilisha muhtasari, hitimishi na mapendekezo ya utafiti mzima ambao tumeufanya. Katika muhtasari tumewasilisha maelezo mafupi kwa kila sura huku tukianisha mambo au vipengele vikuu vilivyozungumzwa katika kila sura hizo. Baada ya hapo tumefanya uwasilishaji wa hitimishi la utafiti kwa kueleza matokeo ya utafiti kulingana na madhumuni mahususi ya utafiti. Mwishoni mwa sura hii, tumewasilisha mapendekezo kwa wadau wa mashairi ya magazetini pamoja na maeneo ya utafiti wa baadaye. Muhtasari wa utafiti huu ni kama ifuatavyo:

## 5.2 Muhtasari wa Tasinifu

Utafiti huu una jumla ya sura kuu tano ambazo zina mada kuu na mada ndogo ndogo ndani yake. Sura ya kwanza imewasilisha vipengele vya usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti; lengo kuu, madhumuni mahususi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mipaka ya utafiti. Vipengele vingine ni vikwazo vya utafiti, utatuzi wa vikwazo vya utafiti na mpangilio wa utafiti. Vipengele hivi ndivyo ambavyo vimemsaidia mtafiti kubainisha nia na ari ya kufanya utafiti huu. Sura ya pili ndio iliyofuatia na imeeleza yafuatayo:

Sura ya pili ya utafiti huu ilihusika na uwasilishaji wa kazi tangulizi ambazo zimetusaidia kupata ufahamu juu ya watafiti wengine wamezungumzia nini kuhusiana na mada ya utafiti huu. Katika kukamilisha lengo la sura hii tumewasilisha ufafanuzi wa dhanna za ushairi, ushairi wa Kiswahili, shairi, sitiari, ishara, na

taswira. Vipengele vingine ni ushairi wa Kiswahili kwa jumla na mashairi ya magazetini. Kwa ujumla kazi tangulizi zinaonesha kwamba, ushairi wa magazetini unamchango mkubwa sana katika kujenga na kuimarisha maadili ya jamii kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, mpaka kufikia sasa bado hakuna utafiti wa kina ambao tayari umekwishafanywa mpaka kufikia sasa kwa nia ya kuchambua matumizi ya lugha ya kitamathali katika mashairi ya magazetini. Utafiti huu umefanywa ili kuziba pengo hili la utafiti. Pia katika sura hii kumewasilishwa mkabala wa kinadharia. Nadharia hizo ni Mwitiko wa Msomaji, Simiotiki na Ufeministi. Sura ya tatu ndiyo iliyofuatia na imewasilisha yafuatayo:

Sura hii ya tatu imewasilisha vipengele vya eneo la utafiti, umbo la utafiti, watafitiwa, uteuzi wa watafitiwa, vyanzo vya data; data za msingi na upili, mbinu za ukusanyaji wa data; uchambuzi wa kimaudhui na usaili. Vipengele vingine ni mbinu za uchambuzi wa data; mkabala wa kimaelezo, usahihi wa mbinu za utafiti, kuaminika kwa matokeo ya utafiti na maadili ya utafiti. Sura iliyofuatia ni ya nne ambayo imewasilisha matokeo ya utafiti.

Sura ya nne imefanya uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa matokeo ya utafiti kwa namna iliyosaidia kujibu maswali ya utafiti wetu. Uwasilishaji huo ulifanywa kwa kuzingatia madhumuni mahususi ya utafiti kwa kuanza na dhumuni mahususi la kwanza. Vipengele vilivyowasilishwa kwa ajili ya kutimiza dhumuni hili ni tamathali za usemi za taswira, sitiari, takriri, tafsida, tafsida, tashibiha na ishara. Dhumuni mahususi la pili lilihusu dhamira ziwasilishwazo na tamathali za usemi, ambapo dhamira za UKIMWI na umalaya, Chanzo cha UKIMWI, unyanyapaa na kinga ya UKIMWI zimechambuliwa. Dhumuni mahususi la tatu lilihusu kubainisha dhima ya

tamathali za usemi katika kujenga dhamira ambapo dhima za kimaudhui na kifani zimeanishwa. Dhima hizo ni kuhamasisha, kufafanua na mawasiliano kwa upande wa kimaudhui na kupamba lugha na mahusiano ya tamathali na vipengele vingine vya kifani kwa upande wa kifani. Sura iliyofuatia ni ya tano inayowasilishwa muhtasari, hitimishi na mapendekezo.

## 5.3 Hitimishi

Utafiti huu ulifanywa kwa nia ya kukamilisha madhumuni mahususi matatu ili kwayo lengo kuu la utafiti liweze kukamilika. Dhumuni mahususi la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha tamathali za usemi zinazojitokeza katika mashairi ya magazetini. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, mashairi ya magazetini yana matumizi ya tamathali za usemi ingawa kwa minajili ya kukamilisha malengo ya utafiti huu tumeteua chache tu za kuzungumzia. Tamathali ya kwanza ni taswira, tumeona namna washairi wanavyotumia tamathali hii katika kuwasilisha mambo kadhaa yanayohusiana na UKIMWI. Katika utafiti wetu, tumebaini matumizi ya taswira kurejelea UKIMWI. Ugonjwa huu unafananishwa na mgeni ambaye hafahamiki katoka wapi lakini nia yake ni kuwadhuru wenyeji wake. Taswira hii ilijengwa pale mwanzoni UKIMWI ulipogundulika na wanajamii walipokuwa katika harakati za kutafuta maarifa juu ya UKIMWI.

Tamathali nyingine ya usemi ambayo imebainishwa katika utafiti huu ni sitiari. Matokeo ya utafiti yanaonesha, washairi wa magazetini wanatumia sitiari kwa nia ya kuonesha makali ya UKIMWI. Kwa mfano, tumeona UKIMWI ukifananishwa na moto, jambo linaloashiria kuwa ugonjwa huu ni hatari kwa maisha ya wanadamu na yeyote atakayeupata basi atapata mateso makubwa kabla ya kufariki dunia. Si hivyo

tu, bali pia, washairi wa magazetini wametumia sitiari kama “tusiamini vizibo,” kuitaka jamii isiamini matumizi ya Kondomu kama kinga dhabiti ya UKIMWI na kwamba kinga madhubuti ni kuacha umalaya na uzinzi.

Tamathali nyingine ya usemi ni takriri, watunzi wa mashairi ya magazetini wanatumia takriri silabi, neno na sentensi. Takriri zilizotumiwa na washairi wa magazetini zimekuwa na nia ya kutoa msisitizo juu ya mambo yanayohusu UKIMWI. Kwa mfano, tumemuona mshairi mmoja akisema, “kupambana na UKIMWI ni kupambana na Mungu,” na kuirudia sentensi hii katika kila mwisho wa ubeti wa shairi lake. Mshairi alikusudia kuielekeza jamii katika kuamini kwamba, Mungu ndiye aliyeuleta UKIMWI na hivyo jamii inapaswa kuacha uzinzi ili kuepukana na UKIMWI. Hata hivyo, katika mjadala wetu wa data tumeonesha kwamba, maelezo ya kwamba UKIMWI umeletwa na Mungu hayana ushahidi wa kisayansi na kwa mujibu huo tukaliacha suala hili katika mjadala ambao utaendelezwa na wataalamu wengine.

Tafsida nayo ni miongoni mwa tamathali ya usemi ambayo tumeijadili kwa kina katika utafiti huu. Washairi wa magazetini wanatumia tafsida kwa nia ya kuficha ukali wa baadhi ya maneno ambayo hayapaswi kutamkwa hadharani kwa mujibu wa utamaduni wa Kintanzania. Kwa mfano, tumeona wakitumia “vizibo” na “mipira,” kurejelea Kondomu. Katika miaka ya mwanzoni ya kugundulika kwa UKIMWI ilikuwa si jambo la kawaida kumsikia mtu anatamka neno Kondomu hadharani. Kwa hiyo, ilitafutwa lugha ambayo ilificha ukali wa maneno husika ndio maana kukaibuka maneno ya kitafsida. Hata hivyo, katika kipindi tulichonacho hivi sasa

neno hili linatamkwa bayana bila taabu, ingawa bado kuna aibu kidogo kwa baadhi ya wanajamii katika kulitaja neno hilo.

Dhumuni mahususi la pili la utafiti huu lilihusu kubainisha dhamira ambazo zinajengwa na tamathali za usemi katika mashairi ya magazetini. Washairi wa magazetini wanatueleza kwamba, chanzo kikubwa cha UKIMWI ni umalaya. Wanasema, umalaya na ukahaba katika kipindi hiki limekuwa ni suala la kawaida kiasi cha baadhi ya watu kufanya biashara ya ngono hadharani bila aibu yoyote. Kutokana na hali hiyo, imekuwa ni rahisi kwa watu wengi kuambukizwa UKIMWI katika jamii. Washairi wa magazetini wametoa rai kuwa, njia pekee ya kukabiliana na UKIMWI ni wanajamii kubadili tabia na mienendo yao kuhusiana na masuala ya kingono-kuuacha umalaya na ukahaba.

Vile vile, washairi wa magazetini wanaendelea kueleza dhamira juu ya chanzo cha UKIMWI kwamba ni Ulaya kwa maana kwamba, Wazungu ndio waliouleta UKIMWI katika bara la Afrika. Walifanya hivyo kwa sababu hawapendi kuwaona Waafrika wanaishi katika dunia hii ili kizazi chao kiishe na baadaye wao warudi na kutawala tena Afrika. Katika mjadala tulioufanya hapo juu tumeeleza kwamba, jambo hili halina mashiko ambayo yanaweza kuaminiwa kitaaluma ingawa pia jambo hili tumeliaacha wazi kwa ajili ya mjadala zaidi.

Dhamira nyingine inayojadiliwa na washairi wa magazetini ni ile ya unyanyapaa dhidi ya waathirika wa UKIMWI. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, baadhi ya wanajamii huwanyanyapaa waathirika wa UKIMWI na wakati mwingine kudai kwamba, waathirika wanapaswa kutengwa na kupelekwa katika kisiwa maalumu

ambako huko wataishi wao tu. Baadhi ya ndugu ya wale ambao wameathirika waliwakimbia ndugu zao na kuwaacha wenyewe bila msaada wowote. Jambo hili linajionesha pale baadhi ya washairi walipoandika mashairi yenye kueleza kwamba, waadhirika wa UKIMWI walioza wakanuka. Huu ni unyanyapaa wa hali ya juu dhidi ya waathirika wa UKIMWI.

Pia, washairi wa magazetini wamewasilisha dhamira inayohusu kinga ya UKIMWI. Baadhi ya washairi wanaeleza, Kondomu ni kinga madhubuti dhidi ya UKIMWI, huku baadhi yao wakipinga kuwa si kinga ya UKIMWI na kuacha uzinzi na kufuata mafundisho ya dini ndio kinga ya UKIMWI.

Dhumuni mahususi la tatu la utafiti huu, lilihusu dhima ya tamathali za usemi katika kujenga dhamira za mashairi ya magazetini. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, mashairi ya magazetini yana dhima ya kufikirisha, kufafanua, kuhamasisha na kufanya mawasiliano juu ya dhamira kwa hadhira iliyokusudiwa. Vile vile, tamathali za usemi zina dhima ya kupamba lugha na pia kumuongoza mtunzi katika uteuzi wa vipengele vingine vya kifani katika utunzi wake wa mashairi.

## 5.4 Mapendekezo

Katika utafiti huu tunatoa mapendekezo kwa wadau wa ushairi wa magazetini na maeneo kwa ajili ya utafiti wa baadaye.

### 5.4.1 Mapendekezo kwa Watunzi wa Mashairi

Tunapendekeza kwamba, watunzi wa mashairi ya magazetini waendelee kutunga mashairi yenye nia ya kuelimisha na kuburudisha jamii katika nyanja mbalimbali ikiwemo hii ya UKIMWI. Tunafahamu, kutunga shairi ni kazi ambayo inahitaji

muda na kujitoa kwa mtunzi na huwa haina malipo ya kueleweka. Hivyo, wasivunjike moyo kwa kuwa kazi wanayoifanya ni ya kuelimisha jamii.

### 5.4.2 Mapendekezo kwa Wachapaji

Tunatoa mapendekezo kwa wachapaji wa mashairi ya magazetini, kuchapa mashairi yanayopelekwa kwao na watunzi bila kupuuzia au kuwadai watoe fedha ndio kazi zao zichapwe. Ni gazeti la *Uhuru* pekee ndilo lililo na machapisho mengi ya mashairi ikilinganishwa na magazeti mengine. Tunatoa mapendekezo kwa magazeti mengine nayo kutoa mashairi katika matoleo yao ya kila siku. Pia, tunawashauri wachape mashairi ambayo yana nia safi katika kujenga na kuendeleza maadili ya jamii.

### 5.4.3 Mapendekezo kwa Tafiti za Baadaye

Utafiti zaidi unaweza kufanywa katika mashairi ya magazetini katika kipengele cha falsafa zinazojengwa na washairi kuhusiana na suala la UKIMWI na masuala mengine ya kijamii.

Pia, utafiti juu ya vipengele vingine vya kifani vinavyojitokeza katika mashairi ya magazetini vinaweza kufanyiwa utafiti wa kina na watafiti wengine.

Mashairi ya magazetini yana utajiri mkubwa wa dhamira za kisiasa, utamaduni, uchumi na kijamii. Hivyo, utafiti zaidi unaweza kufanyika katika maeneo haya.

## MAREJELEO

Alhabib, M. (2012), "Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Taarabu," Tasinifu ya M.A Kiswahili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Aronson, J. (1992), "A Pragmatic View of Thematic Analysis," In The *Qualitative Research Methods in Nursiny*. Orlando FL: Grune& Stratton, Pp (37-73).

Babbie, E. (1999), *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Barthes, R. (1994), *The Semiotic Challenge*. Berkely: University of Califonia Press.

Benner, P. (1985), "Quality of Life: A phenomeno logical perspective on explanation, prediction and Understading in Nursing Science", *Advanees in Nursing Science*, 8(1), 1-14.

Bogdan, R. and Biklen, S.K. (1992), *Qualitative Research of Education: An introduction to Theory and Methods*, (Edrs), Boston: Allyn and Bacon.

Bulaya, J. (2010), "Bongo Fleva na Siasa: Uchambuzi wa Ndiyo Mzee na Siyo Mzee za Profesa Jay", katika *Mulika,* Namba 29&30. TATAKI.

Chaligha, E. (2011), "Ujinsia katika Katuni Mnato za Magazetini," Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Chandler, D. (1992). *Semiotics: The Basics,* London: Routledge Press.

Cohen, L, na Wenzake (2000) *Research Methods in Education*, 5$^{th}$ edition. London: Rutledge Falmer.

Creswell, J.W. (2009), *Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publications.

Eisenstein, Z. (1979). “Capitalist Patriarchy and Case for Socialist Feminism in New York,”Monthly Review.

Frolova, N. (2003). “Euphrase Kezilahabi: The Renewal of Kiswahili Poetry”. In *Kiswahili*, Vol. 66 Dar es salaam. IKR.

Good, G.V. (1966), *Essentials of Educational Research.* New York: Maridith Publications Co.

Haries, L. (1962), *Swahili Poetry*, London: OUP.

Ismail, J.H. (2010), “Nafasi ya Nyimbo za Bongo Fleva katika Uelimishaji wa Haki katika Jamii”. Katika *Mulika.* Namba 29&30, Dar es Salaam: TATAKI.

Jilala, H. (2008). The Artistic Uses of Metaphors in Constructing Meanings and Messages in New Generation Songs in Tanzania. MA Dissertation (Unpublished), University of Dar es Salaam.

Kahigi K.K. (1995). Lugha Katika Vitabu Vya Watoto. Katika *Kioo cha lugha: Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi*. Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Juzuu, Na. 1. (uk. 21-36).

Kandoro, S. A. (1972), *Mashari ya Saadan* Dar es Salaam: NPL.

Kandoro, S. A. (1978), *Ushahidi wa Mashairi ya Kiswahili na Lugha Yake*. Dar es Salaam: Longman Ltd.

Kezilahabi, E. (1974), *Kichomi*. Nairobi: Heinnemen

Kezilahabi, E. (1977), “Mashari ya Saadan,” Katika *Mulika*, Namba 14. Dr es Salaam: TUKI. Kur. 32-40.

Kezilahabi, E. (1983), "Uchambuzi katika ushari wa Kiswahili". Katika *Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandsihi wa Kiswahili,* Dar es Salaam: TUKI, Kur. 145-165.

Kezilahabi, E. (1988), *Karibu Ndani* Dar es Salam: DUP.

Kezilahabi, E. (2008), *Dhifa*, Dar es Salaam: Vide-muwa.

Khalifa, A.I.S. (2012), "Usawiri wa Masuala ya Kijinsia katika Lugha ya Mashairi. Mifano Kutoka Mashairi ya Bongo Fleva Tanzania", Dar es Salaam. Tasnifu ya *M.A. Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Khalifan, M. Y. (2013), "Masuala ya Kisiasa katika Ushairi wa Kandoro: Mifano kutoka Katika Mashairi Yake," Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Khatibu, M. S. (1987), "Jinsi Washairi wa Kiswahili walivyoliona Azimio la Arusha," Katika *Mulika,* Namba 19, Dar es Salaam: TUKI.

Kimani, R. (1983), "Suala la Ushairi wa Kiswahili," Katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili Namba 3*, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 127-144.

Kitogo, S. A. (2002), "The Poets Contribution to Political Development: A case of Saadan Abdul Kandoro", Unpublished *M.A. Thesis* UDSM.

Kothari, C. R. (2009), *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Limited.

Kothari, C. R. (2008*), Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

Kumar, R. (1999), *Research Methodology: A Step-by-Guide for Geginners*. New Delhi: SAGE Publication.

Leacock, E. (1981). “Myth of Male Dominance in New York,” Monthly Review Press.

Low, N.R., (2011), “Athari ya Lugha Katika Kuibua Dhamira: Mifano kutoka Nyimbo za Kizai Kipya zinazohusu UKIMWI”, Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kiukuu cha Dar es Salaam.

Leininger, M. M. (1985), “Ethnography and Ethnonursing: Model and Modes of Qualitative Data Analysis”. In. M.M. Leininger (Ed.). *Qualitative Research Methods in Nursiny*. Pp (37-73). Oro lando FL: Grune& Stratton.

Macknnon, C.A. (1991), *Toward A Feminist Theory of State*. London: Havard University Pess.

Madaso, “Ng’wanza (2009), Serikali yafanya Kufuru”, Katika http://www.jamii frums.com/habari- na-hoja-mchanyiko/40975 - serikali-yafanya-kufuru print. html. imesomwa tarehe 15/02/2010.

Mansour, A. A. H. (2013), “Kuchunguza Vipengele vya Fani katika Mashairi ya Kiswahili: Ulinganuzi na Ulinganishi wa Mashairi ya Euphrase Kezilahabi na Haji Gora Haji,” Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Massamba, D. P. B. (1983), “Suala la Ushairi wa Kiswahili,” Katika Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili-Fasihi namba 3. Dar es Salaam: TUKI.

Mayoka, J., (1984), *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*. Nairobi: EALB.

Moore, H. (1988). *Feminism and Anthropology*. Mimepolis: University Press of Minnesota.

Msokile, M. (1993), *Uchambuzi na Uhakiki: Karibu Ndani,* Dar es Salaam: DUP.

Mulokozi, M. M. (1982), “Protest and Resistance in Swahili Poetry: 1600– 1885,” In *Kiswahili Vol. 49/1.* Dar es Salaam: IKR, pp. 25-51.

Mulokozi, M. M na K. K. Kahigi (1979), *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: TPH.

Mulokozi, M. M. na T. S. Y. Sengo (1995), *History of Kiswahili Poetry* [AD 1000-2000]. Dar es Salaam: TUKI.

Msuya M.B. na A.P. Lupokela, (2010), “Dhima ya Bongo Fleva katika Maadili na Malezi kwa Jamii”, Katika *Mulika,* Namba 29&30, Dar es Salaam: TATAKI.

Mutembei, A. K. (2009), *UKIMWI katika Fasihi ya Kiswahili 1982- 2006*, Dar es Salaam: TATAKI.

Newman, W.L. na Wenanzake, (2006), *Social Research*. Sixth Edition, Boston: Pearson.

Njogu, K. na C. Rocha (1999), *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi, JKF.

Ntarangwi, M. (2004), *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustana College.

Omari, S. (2008), “Mtindo na Matumizi ya Lugha katika Muziki wa Kizazi Kipya Tanzania”, Katika *Kiswahili,* Juzuu 69. TUKI. Kur. 73-92.

Omari, S. (2009), "Tanzanian Hip hop Poetry as Popular Literature," Unpublished Ph.D Dissertation, university of Dar es Salaam.

Omary, M. (2011), "Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008)," Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Oslon, S. H. (1975), "Philosophical Implications of Some Swahili Idioms", In *Kiswahili* Vol. 45/2, Dar es Salaam: IKR. Pp. 32-37.

Raffel, B., (1984), *How to Red a Poem*. New York: Penguin Publishers. *Report*. Vol. 2, No. 1.

Robson, C., (2007), *How to do a research project: A guide for Undergraduate Students*, Cariton Victoria: Blackwell Publishing.

Samwel, M. (2010), "Masuala ya Kisiasa katika Mashairi ya Mapenzi ya Muziki wa Bongo fleva", Katika *Mulika*, Na. 29&30. Dar es Salaam: TATAKI.

Sengo, T.S.Y. (2009), *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: AKADEMIYA.

Sanka, S.M. (1994), "Semantic Deviation in Iraqu Oral Poetry". Unpublished *M.A Dissertation*, UDSM.

Senkoro, F.M.E.K. (1982), *Fasihi*. Dar es Salaam: DUP.

Senkoro, F. E. M. K. (1988), *Ushairi: Nadharia na Uhakiki*, Dar es Salaam: DUP.

Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi.* Dar es Salaam: KAUTTU Limited.

Topan, F. (1974), "Utangulizi" katika *Kichomi*, Nairobi: Heiremann.

Taylor, S. J. & R. Bogdan (1984), *Introduction to Qualitative Research Methods: The Search for Meanings*. New York: John Wiley& Sons.

Wamitila, K.W., (2002), *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wafula, R. M na Njogu, K (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta foundation.

Wamitila, W. (2003), *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wamitila, K.W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi: PPL.

Wamitila, K.W. (2008), *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide Muwa.

Warren, A. and Wellek. R., (1985), *Theory of Literature*, London: Penguin Group: London.

Young, P.V., (1984). *Scientific Social Surves and Research*, Enalewood Chiffs: Prentice Hall. Inc.

Yin, R. K. (1994), *Case Study Research: Design and Methods*, (2nd eds.) thousand Oaks Calif: SAGE Publishers.

## MAREJELEO YA MAGAZETI

Breik, B. S. (1998), “Kilombili ni Hatari,” katika *Nipashe*, Machi 17.

Clemence, M. (1991), “Tujihadhari na UKIMWI,” katika *UHURU*, Januari 7.

Kamunge, P. H. (1992), “UKIMWI,” katika *UHURU*, Juni 30.

Khalfan, R. (2001), “Kupambana na UKIMWI ni Kupambana na Mungu,” katika Nipashe, Juni 5.

Kibona, I. (1990), “Tuepukeni UKIMWI,” katika *UHURU*, Oktoba 23.

Limbetembe, M. (1996), “Tujikinge na UKIMWI,” katika *Majira*, Machi 27.

Mfalme, Y. R. R. (2003), Kuenea kwa UKIMWI,” katika *UHURU*, Mei 14.

Majid, I. (1994), “Utaukwaa UKIMWI,” katika *UHURU*, April 16.

Marare, Y. (1999), “Ogopa Kila Mmoja,” katika *Nipashe*, Januari 27.

Mkondoa, E. (2001), “UKIMWI Kubwa Balaa,” katika *Mtanzania*, Januari 9.

Mkumbila, A. (1999), “Amebainika,” katika *Uhuru*, Januari 7.

Manyama, B. (1993), “UKIMWI Tishio,” katika *UHURU*, January, 27.

Mpunga, J. C. (1990), “UKIMWI Shida Hatari,” katika *UHURU*, Januari 5.

Mwanambaya, M. A. (2001), “Kinga Kuacha Zinaa,” katika *Majira*, Disemba 10.

Mwinyimkuu, A. J. (1995), “UKIMWI Hauna Dawa,” katika *Majira*, Juni 30.

Mziwanda, M. M. S. (1990), “Nimejikwaa Kisiki,” katika *UHURU*, Novemba 21.

Nzinku, A. L. M. (2002), “UKIMWI,” katika *Majira*, Oktoba 30.

Tumwimbile, M. (2002), “Kupima UKIMWI Sheria,” katika *Majira*, Januari 5.

Sanya, D. A. (2001), “UKIMWI Unamaliza,” katika *Nipashe*, Januari 25.

Sufiani, A. (1988), “AIDS,” katika *Mzalendo*, Mei 22.

Yusuph, S. (1989), “UKIMWI Hauna Dawa,” katika *Mzalendo*, Oktoba 29.

# VIAMBATANISHO

## KIAMBATISHO A

## DODOSO KWA WASOMAJI WA MASHAIRI YA MAGAZETINI

**Utangulizi**

Mimi ninaitwa Omari Mtunguja Kombo mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili katika Kiswahili Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Kwa sasa ninafanya utafiti huu kama sharti pekee la kukidhi vigezo vya kutunukiwa shahada hiyo. Kwa heshima na taadhima ninaomba nikufanyie usaili kwa nia ya kunipatia data zitakazosaidia kukamilika kwa utafiti huu.

**Maswali ya Kiutambulisho**

Jina………………………………………………………………….

Elimu……………………………………………………………….

Kuoa/kuolewa……………………………………………………….

Kazi………………………………………………………………….

Eneo Unaloishi…………………………………………………………

**Maswali kuhusu Mada yaUtafiti**

1. Unapenda kusoma magazeti gani ya Kiswahili ya hapa nchini?
2. Magazeti yapi huadika mashairi katika matoleo yake ya kila siku?
3. Unapenda kusoma mashairi yanayoeleza mambo gani?
4. Umeshawahi kusoma mashairi yanayoelezea masuala ya UKIMWI.
5. Nini kinachokuvutia katika mashairi hayo yaelezayo UKIMWI.
6. Eleza dhamira mbalimbali zinazohusu UKIMWI zinazojitokeza katika mashairi hayo.
7. Unafikiri kwa nini washairi hao wanasawiri dhamira hizo.

**Asante kwa Ushirikiano Wako**

## KIAMBATISHO B

## DODOSO KWA WATAALAMU WA FASIHI

**Utangulizi**

Mimi ninaitwa Omary Mtunguja Kombo mwanafunzi wa Shahada ya Uzamili katika Kiswahili Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Kwa sasa ninafanya utafiti huu kama sharti pekee la kukidhi vigezo vya kutunukiwa shahada hiyo. Kwa heshima na taadhima ninaomba nikufanyie usaili kwa nia ya kunipatia data zitakazosaidia kukamilika kwa utafiti huu.

**Maswali ya Kiutambulisho**

Jina…………………………………………………………………….

Elimu…………………………………………………………………….

**Maswali kuhusu Mada yaUtafiti**

1. Eleza mchango wa mashairi ya magazetini katika maendeleo ya jamii kwa ujumla wake.
2. Tamathali za usemi katika mashairi ya magazetini zina dhima gani katika kujenga dhamira na maudhui?
3. Kwa nini washairi wengi wa mashairi ya magazetini wanaandika mashairi ya Kimapokeo?

**Asante sana kwa Ushirikiano Wako**